SUPA JACKPOT
TZS.1,046,433,814
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SERIKALI** yasitisha uwekaji wa hereni mifugo kwa muda




UKURASA 13


# Nipashe

Ijumaa Novemba 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581119

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# POLISI MBARONI

## **WATUHUMIWA** kushiriki kusafirisha wahamiaji haramu...

*Endelea Ukurasa wa 2*



Mkuu wa Jeshi la Uhamiaji Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACI), Kigongo Shile (kulia) na maofisa wengine wakiwa wamewaweka chini ya ulinzi wahamiaji haramu raia wa Ethiopia waliokamatwa wakisafirishwa na maofisa watano wa Polisi mkoani humo. **Picha ndogo:** Kamanda wa Polisi, ACP Benjamin Kuzaga, akionyesha gari aina ya Toyota Cresta inayomilikiwa na mmoja wa askari wa jeshi hilo, iliyotumika kusafirisha wahamiaji hao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

UKURASA WA 2

### NIT YANUNUA NDEGE KUFUNDISHA MARUBANI

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimenunua ndege mbili zitakazoanza kutumika kufundisha marubani wa ndani ili kupunguza gharama za kumsomesha rubani mmoja nje kwa Sh. milioni 200...

UKURASA WA 3

### MBUNGE ADAI WAKILI CHADEMA ALIMPANIA MDEE NA WENZAKE

MBUNGE wa Viti Maalumu kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Hawa Mwaifunga, amedai mahakamani kuwa wakili wa chama hicho, Peter Kibatala alimpania kumuuliza maswali...

UKURASA WA 7

### TANZANIA NA CHINA ZAKUBALIANA KUDUMISHA UHUSIANO KIUCHUMI

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa China, Xi Jinping, wamekubaliana kuendeleza uhusiano na ushirikiano baina ya nchi hizo mbili. Taarifa ya pamoja iliyotolewa...

## Wabunge washangazwa madudu ripoti NHIF, wabababa kujifungua

UKURASA 2

## RIPOTI MAALUM: Ukame ulivyoathiri maisha ya wanakijiji

UKURASA 4

**MICHEZO** **NABI MGUU NDANI, MGUU NJE YANGA** UK. 32

**KATUNI** UK. 6



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Rais wa China, Xi Jinping mjini Beijing jana, akiwa katika ziara ya kikazi nchini humo. **PICHA: IKULU**

# Askari polisi 5 watuhumiwa kusafirisha wahamiaji haramu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASKARI watano wa Jeshi la Polisi mkoani hapa wametiwa mbaroni kwa tuhuma za kuwasafirisha wahamiaji haramu sita raia wa Ethiopia waliokuwa wakielekea nchi jirani ya Malawi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema askari hao walikamatwa Oktoba 20, mwaka huu, wakiwa maeneo ya Uyole jijini hapa, wakipanga njama za namna ya kuwasafirisha wahamiaji hao kwenda wilayani Kyela ambako wangevuka mpaka na kuingia Malawi.

Alisema wahamiaji hao pamoja na askari walikamatwa wakiwa na gari dogo aina ya Toyota Cresta lenye namba za usajili T 946 BTT mali ya mmoja wa askari waliokamatwa kuwasafirisha wahamiaji hao haramu. Kamanda Kuzaga aliwataja askari waliokamatwa kuwa ni Mrakibu wa Polisi (ASP), Thomas Bwire, ambaye ni ofisa wa jeshi hilo na askari wengine wanne ambao ni F.3132 SGT. Beda Moriss, F.8497CPL. Saimon Billia, G.3146 CPL. Mohamed Ndunguru na G.6364 CPL. Joseph Manumbu.

"Tuliwakamata askari hawa sisi wenyewe baada ya kupata taarifa kutoka kwa mmoja wa wasiri wetu, kazi hii ni moja kati ya shughuli za kulisafisha jeshi letu kama tulivyoelekezwa na Mkuu wetu wa Jeshi la Polisi nchini," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema askari hao wameshaanza kuchukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na baada ya kukamilika kwa taratibu hizo jeshi hilo litatoa tena taarifa kwa umma.

Kamanda Kuzaga aliwataja wahamiaji waliokamatwa kuwa ni Hasabe Mwaramdo (22), Yonas Like (15), Duwyi Dumis (20), Moges Adese (30), Lapiso Mishamo (54) na Dagfu Ayele (22), ambao wote ni raia wa Ethiopia.

Alisema wataendelea kuchukua hatua hizo ili kuhakikisha wanatembea kwenye kaulimbiu iliyotolewa na IGP, Camilius Wambura ambayo ni 'Nidhamu, Haki, Weledi na uadilifu, ndio msingi wa mafanikio yetu'. Aliwataka askari kuacha kufanya vitendo viovu kwa maelezo kuwa wataendelea kuchukuliwa hatua za kinidhamu kama inavyotokea kwa raia wa kawaida na hata watumishi wengine ambao sio askari.

# NIT yanunua ndege kufundisha marubani

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimenunua ndege mbili zitakazoanza kutumika kufundisha marubani wa ndani ili kupunguza gharama za kumsomesha rubani mmoja nje kwa Sh. milioni 200.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zakaria Mganilwa, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya NIT kwa waandishi wa habari jijini jijini hapo.

Alisema, lengo la kununuliwa kwa ndege hizo mbili ni kukiwezesha chuo hicho kuanza kutoa mafunzo ya urubani nchini.

"Ndege hizi mbili za injini moja zinazoweza kubeba abiria wanne zimegharimu Shilingi bilioni nne, ambazo tumezinunua nchini Marekani, zitakuwa zinatumika kwa ajili ya kujifunza, lakini baadaye zitanunuliwa nyingine mbili za njini mbili kwa kuwa ni lazima rubani aendeshe ndege ya injini moja na injini mbili ili aweze kuajiriwa na mashirika ya ndege," alisema Prof. Mganilwa.

Pia alisema kutokana na chuo hicho kuanza kutoa mafunzo ya urubani nchini kutasaidia kupunguza gharama kubwa za kusomesha watu nje ya nchi.

"Hivi sasa nchini tuna ndege 400, lakini marubani asilimia 60 wote ni kutoka nje ya nchi hali hii inachangia gharama kubwa kwa mashirika ya ndege, wakija hapa wanakuwa na masharti magumu watataka uwaweke kwenye hoteli ya nyota tano na masharti mengine magumu," alisisitiza.

Pia alisema kutokana na serikali kuwekeza fedha nyingi katika miradi mkubwa ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa ya (SGR), chuo hicho kimeanza kutoa kozi zitakazosadia rasilimali watu wa kutosha katika fani mbalimbali.

"Katika mradi wa SGR, tumeanzisha kozi ambazo zitawezesha mradi huu kuwa na wataalamu hapa nchini ambao watatumika kuuhudumia ikiwamo mafundi na wahandisi wa reli na tunatoa mafunzo kulingana na mahitaji ya miradi," alisema.

Prof. Mganilwa alisema chuo hicho pia kimeanza kutoa kozi ya ufundi wa kutengeneza na kusanifu meli ili kuepuka changamoto iliyowahi kujitokeza hapo awali ya kufa kwa shirika la meli nchini.

"Hivi sasa vijana wapo katika mafunzo ya kutengeneza meli panoja na usanifu wa meli na hii inamaanisha kuwa hadi mwakani tutakuwa na vijana wengi waliohitimu mafunzo na wenye ujuzi huu ambao watatumika kutoa huduma katika mashirika ya meli nchini," alisema.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema chuo hicho kitakuwa msaada mkubwa katika uzalishaji wa rasilimali watu.

"Hivi sasa shirika la ndege nchini tunazo ndege 11, lakini mwakani zinaingia zingine tano na kuwa na jumla ya ndege 16, ambazo zitahitaji wahandisi, wahudumu pamoja na marubani," alisema.

# Wabunge washangaa madudu ripoti NHIF

**Na Richard Makore,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wamezidi kushangaa madudu yaliyoibuliwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 ikiwamo taarifa za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuonyesha wanaume walijifungua katika vituo vya afya.

Akichangia hoja wakati wa mjadala kuhusu ripoti tatu za CAG zilizowasilishwa bungeni juzi jijini hapo, Mbunge wa Viti Maalum, Ritha Kabati, alisema kuna madudu katika NHIF huku akistaajabu kusikia ripoti ikisema kulikuwa na majina ya wanaume waliopata huduma ya kujifungua katika vituo vya afya.

Kabati alisema taarifa hiyo inazua maswali mengi kwa kuwa anayejifungua ni mwanamke na si mwanamume kama ilivyoonekana katika ripoti hiyo.

Pia alisema ana ushahidi wa mbunge mwenzake aliwahi kutibiwa kwa kupewa dawa na kisha akaondoka siku hiyo hiyo, lakini alipigiwa simu na kuambiwa alilazwa hospitalini kwa wiki moja.

Alisema ni ajabu kwa hospitali mbalimbali na vituo vya afya nchini kushindwa kumwambia mgonjwa anayetibiwa kupitia NHIF ametumia kiasi gani ili atoke pale akiwa anajua.

Mbunge huyo alishangaa kusikia kuna baadhi ya vituo vya afya nchini vinateketeza dawa kutokana na kuisha muda wake, wakati wananchi wakihangaika kutafuta dawa lakini hawapati.

Aliomba serikali kuangalia suala hilo kwa kuwa halifai kutokea kwa kuwa Watanzania wana uhitaji mkubwa wa dawa, lakini huku upande wa pili kuna watu wanachoma wanateketeza dawa.

Mbunge wa Hai, Saashisha Mafuwe, alisema halmashauri nyingi zimekuwa vichaka vya kuficha fedha za serikali na kuzitumia katika mambo yasiyojulikana.

Alisema ripoti ya CAG inaonyesha fedha nyingi zinazotolewa na halmashauri kwa ajili ya kukopesha wanawake, vijana na wenye ulemavu hazirudi badala yake zinapotea. Pia alishangaa kusikia halmashauri kubakiza fedha walizotengewa kwa mwaka husika, huku wananchi wakihitaji maendeleo.

Naye Mbunge wa Mlimba, Godwin Kunambi, alishangaa majiji makubwa hapa kushindwa kujenga hata kituo cha afya kupitia mapato ya ndani.

Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Kasheku (Msukuma) alisema halmashauri nyingi zina madudu ya wizi wa fedha huku akisema kama tatizo ni sheria zibadilishwe.

"Kama wenzetu walikosea kutunga sheria basi tuzibadilishe ili kutoa adhabu kwa wezi wa fedha hizi za halmashauri," alisema huku akishauri kama wakurugenzi wa halmashauri ndio tatizo, basi nafasi hizo zitangazwe ili watu waombe tofauti na sasa wanapoteuliwa na Rais.

HABARI KITAIFA

## KESI KINA MDEE

# Mbunge adai wakili wa CHADEMA alimpania

**Na Grace Gurisha**

MBUNGE wa Viti Maalumu kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Hawa Mwaifunga, amedai mahakamani kuwa wakili wa chama hicho, Peter Kibatala alimpania kumuuliza maswali kama yeye alivyompania kumjibu.

Mwaifunga alidai hayo jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama ya Kuu, Masjala Kuu, wakati wa kusikiliza kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama wabunge 19 wanawake iliyofunguliwa na Mbunge wa Viti Maalumu, Halima Mdee na wenzake 18 baada ya kutokea mvutano kati ya Kibatala na Mwaifunga. Na mahojiano yalikuwa kama ifuatavyo:

Kibatala: Katika kikao cha Baraza Kuu la CHADEMA kilichofanyika Mei 11, 2022, ulipewa nafasi yoyote kuzungumza kwenye kikao hicho?

Mwaifunga: Nilipewa nafasi ya kuomba msamaha na sio kuzungumza chochote (huku akikataa kujibu swali hilo kwa kunukuu ajenda za kikao hicho akidai anajibu kutokana na hati ya kiapo).

Kibatala: Kweli au si kweli kwenye ajenda za kikao hicho inaonesha ulipewa nafasi ya kuzungumza chochote Mwaifunga: Sijaelewa swali hilo, kwa hiyo jitahidi nilielewe swali.

Kibatala: Ni kweli au si kweli kwamba nafasi hiyo ilitolewa kabla ya wajumbe hawajapiga kura?

Mwaifunga: Nilipewa nafasi ya kuomba msamaha.

Baada ya majibu hayo, Jaji Mkeha alimtaka Mwaifunga kujibu swali aliloulizwa na Mwaifunga alidai Kibatala analazimisha azungumze anachotaka yeye wakati alipewa nafasi ya kuomba msamaha.

Kutokana na majibu hayo, Jaji Mkeha alisema kwa namna hiyo hawataweza kuelewana na kuwataka wasonge mbele.

Msimamo wa Kibatala ni kwamba walipewa nafasi, Mwaifunga anadai kilichotokea ni kupewa nafasi ya kuomba radhi.

Hata hivyo, Kibatala alidai hana msimamo wowote, anamuuliza kwa mujibu wa ajenda kama ni kweli alipewa nafasi hiyo.

Mwaifunga alijibu kwa mujibu wa kiapo chake nafasi iliyotolewa ni kuomba msamaha.

Kutokana na mvutano huo, Jaji Mkeha alimtaka Mwaifunga ajibu swali kama anavyoulizwa kwa sababu mawakili wake (Ipilinga Panya) watapata nafasi ya kumuuliza maswali ya ufafanuzi, hivyo ajibu maswali.

Jaji Mkeha aliwauliza wawili hao kwanini wanakuwa wagomvi na Mwaifunga alidai wakili Kibatala alimpania.

Kutokana na jibu hilo na Jaji alimuuliza kama na yeye alimpania pia.

Mwaifunga alidai kuwa na kusababisha mvutano huo uldumu kwa dakika kadhaa.

Alidai katika kiapo chake hakueleza kama Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu John Mnyika, walikuwapo katika kikao cha Baraza Kuu kilichowafukuza uanachama.

Mdee na wenzake 18 walifungua kesi hiyo Julai 21, mwaka huu mahakamani hapo dhidi ya CHADEMA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wakipinga uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kuwavua uanachama, Mei 11, mwaka 2022.

Katika shauri hilo namba 36 la mwaka 2022, wabunge hao pamoja na mambo mengine, wanaiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi huo wa CHADEMA kuwafukuza, kisha itoe amri tatu.

Wabunge hao wanaomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na amri ya zuio dhidi ya Spika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kutokuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
03/11/2022

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 04/11/2022 kampuni ya **ICHEETAH LOGTECH TANZANIA LTD** itasafirisha Gari zenye vipimo vikubwa kutoka Dar es Salaam kuelekeaa Kigoma Gari hizo zenye namba za usajili: **T507DZD/T907DZE , T148EAF/T630EAJ , T163EAF/T624EAF na T150EAF/T631EAF**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **I. T507DZD/T907DZE Urefu-20m Upana -5.5m ,Kimo-4.8m**
   **II. T148EAF /T630EAJ Urefu-20m Upana -4m ,Kimo-4.8m**
   **III. T163EAF/T624EAF Urefu-20m Upana -3.9m ,Kimo-4.8m**
   **1V. T150EAF/T631EAF Urefu-20m Upana -4m ,Kimo-4.8m**

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam hadi Kigoma Kupitia Dodoma** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

117132202


# Serikali yasitisha utambuzi mifugo kwa hereni

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imetangaza kusitisha kwa miezi mitatu utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki, ili kutoa muda wa kufanya tathmini ya kazi hiyo, baada ya kupokea malalamiko ya utekelezaji wa utaratibu huo.

Hatua hiyo imechukuliwa ikiwa ni siku nne baada ya Nipashe kuchapisha habari ya wafugaji wilayani ya Longido mkoani Arusha kulalamikia suala hilo huku wakiomba kuongezwa muda.

Gazeti hili liliripoti namna wafugaji hao walivyokwama kulipia gharama za usajili wa mifugo yao, baada ya kuyumba kiuchumi kutokana na athari za ukame ambazo zimechangia mifugo yao kufa na mingine kukonda kwa kukosa malisho na hivyo kushindwa kuuzika.

Akitoa taarifa maalum kwenye maeneo mawili ya hereni kwa mifugo na moto Mlima Kilimanjaro jana bungeni jijini Dodoma, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema serikali imesitisha utambuzi wa mifugo kwa njia ya kielektroniki kwa muda wa miezi mitatu, wakati ikiendelea na tathmini ambayo itawezesha kutoa mwongozo wa namna bora zaidi ya kutekeleza kazi hiyo.

Majaliwa alisema bei elekezi ya kuweka hereni za kielektroniki iliyowekwa na serikali ya Sh. 1,750 kwa ng'ombe na punda na Sh. 1,000 kwa mbuzi na kondoo, zimekuwa zikilalamikiwa na wafugaji kwamba ni kubwa na ni tofauti na uhalisia.

"Serikali imesikia hoja za wafugaji kuhusu mapungufu ya kanuni, usimamizi wake na utekelezaji wake na gharama kubwa za uwekaji hereni za kielektroniki, hivyo inaona kuna haja ya kufanya upya tathmini ya mchakato huu," alisema.

Majaliwa alisema kazi hiyo ya utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki ilipaswa kukamilika Oktoba 31, mwaka huu, lakini hadi kufikia tarehe hiyo idadi ya mifugo iliyokuwa imetambuliwa na kusajiliwa ilikuwa 5,068,617 sawa na asilimia 11 ya lengo la kutambua mifugo 45,920,000.

"Serikali haijasitisha malipo kwa ajili ya huduma hii, imesitisha mchakato unaolalamikiwa ili kuipa nafasi serikali kupitia Wizara ya Mifugo, kufanya tathmini ya mapungufu ya kikanuni yaliyowekwa kwa ajili ya kufanikisha kazi hii vizuri kwa kushirikisha wadau wa mifugo," alisema.

Majaliwa aliziagiza Wizara za Maji; Mifugo na Uvuvi pamoja na mamlaka za serikali za mitaa kwa kushirikiana na wadau wa mifugo, kuhakikisha miradi mikubwa ya maji inayotekelezwa kwenye maeneo yenye shughuli za wafugaji inafanyiwa tathmini na kupewa kipaumbele cha kutengeneza miundombinu.

Alisema miundombinu hiyo ni kwa ajili ya mifugo ikiwamo maeneo ya kunyweshea badala ya kuwaacha kwenda kwenye mabonde yaliyohifadhiwa.

Akijibu swali la Mbunge wa Kilwa Kusini (CCM), Ally Kasinge, aliyetaka kufahamu mkakati wa serikali wa kudhibiti migogoro inayosababishwa na wafugaji baada ya kusitisha kazi hiyo ya utambuzi wa mifugo, Waziri Mkuu alisema imesitishwa ili kuipa nafasi serikali kuweka mikakati thabiti katika kuendesha kazi hiyo.




RIPOTI MAALUM

# Ukame ulivyoathiri maisha ya wanakijiji

## Wananchi, mifugo wachangia maji ya kunywa

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa**
MPWAPWA

UMBALI wa takribani kilomita 46 Kusini Magharibi mwa mji wa Mpwapwa mkoani Dodoma, kunapatikana Kijiji cha Sazima kilichoko Kata ya Mima ambacho ndani mwake kuna Kitongoji cha Mgogo.

Kipindi hiki cha ukame unaoripotiwa kuyaathiri maeneo mengi nchini kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, ndani ya kitongoji hicho Nipashe inashuhudia wakazi wake wakichangia na mifugo maji ya kunywa yanayopatikana kwenye visima.

Uongozi wa kisiasa katika eneo hilo unabainisha ni kadhia inayoyakumba maeneo mengine mengi ndani ya Kata ya Mima inayokadiriwa kuwa na wakazi 12,600, huku Mgogo kukiwa na wakazi wapatao 400 na mifugo zaidi ya 2,500 inayotegemea maji kutoka visima 20 vilivyoko kijijini Sazima.

Kijijini huko, Nipashe inashuhudia namna wanyama, hususan ng'ombe na mbuzi, wanavyogombea maji huku wananchi nao wakiyachota kwa ajili ya kunywa na matumizi mengine ya nyumbani.

Kwa macho maji hayo yana mwonekano usiopishana na rangi ya chai ya maziwa, baadhi ya wananchi wakiyachota na kuyanywa hapo hapo na wanapoulizwa na Nipashe 'kulikoni?', Mrejesho wao ni "Mungu anatupenda ndiyo maana hatupati magonjwa ya mlipuko".

Ni hali inayokinzana na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 - 2025 inayoielekeza serikali kuhakikisha wananchi wanaoishi katika umaskini wanawezeshwa kupata huduma muhimu za kijamii ili kuwafanya waishi katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, pia Sera ya Maji iliyotumika sasa ambayo pamoja na mambo megine, inaelekeza huduma za majisafi ziwafikie wananchi, tena ndani ya mita 400 kutoka kwenye makazi yao.

Elisi Paganzi, Mkazi wa Kitongoji cha Igoji kijijini huko, anasema wanapofika katika visima hivyo vya maji, baadhi yao wanachota pamoja na mifugo na wengine husubiri imalize kunywa maji ndipo wachote.

Anasema waathirika wakubwa wa kero hiyo ni wanawake kwa kuwa desturi zao, ni wajibu wa wanawake kuchota maji pasi na kujali vikwazo vilivyoko katika kuipata huduma hiyo.

"Wapo ambao wanafuata maji usiku kwa kuwa muda huo yanakuwa hayajachafuliwa na mifugo na wakati mwingine hukutana na wanyama wakali kama fisi kutokana na hili pori unavyoliona," anafafanua.

Elisi anaeleza uzoefu wake kijijini kuwa kutokana na umbali mrefu uliopo kati ya makazi ya wananchi na visima viliko, wengi wao hutumia punda kubeba maji, akibainisha familia yake huchota madumu 10 ya maji ambayo huyatumia kwa siku mbili.

"Unatembea umbali wa kilomita tano na punda wenye madumu ya maji tunachoka sana, unafika nyumbani hoi na mujukumu mengine yanakusubiri ikiwamo kupika na hata shughuli za kilimo.

"Kuna wakati maji hayapatikani kwa wakati, inakulazimu kusubiri kwa zaidi ya saa tatu ili yaongezeke. Mifugo ikifika kama hujachota hayo maji huwezi kuyachota na kama unavyoona tunagombea maji na mifugo.

"Kuna visima vingine maji yake yanaonekana meupe, hivi vingine ni kama unayaona, ni machafu lakini ndiyo tunakunywa na kupikia haya haya," Elisi alisema katika mazungumzo na Nipashe kisimani huko Jumanne ya wiki iliyopita.

**MTIHANI KWA MUME**

Mbali na vikwazo vilivyoko katika kuyapata maji hayo, Elisi anabainisha kuna shida nyingine anapofika nyumbani kwa kuwa mara kadhaa amegombezwa na mumewe kutokana na kutumia muda mwingi kisimani na hata kuangushiwa tuhuma za usaliti katika ndoa.

"Hata nikimweleza kulikuwa na shida kupata maji kisimani, hataki kunielewa, ananikazania 'ulikuwa wapi?' Ninajitahidi kueleza ukweli, hananielewi, anahisi nilikuwa na mwanamume akanichelewesha kufika nyumbani," Elisi anasimulia na kubainisha mara kadhaa amekumbana na kipigo kutoka kwa mume, sababu kuu ikiwa kuchelewa kurejea nyumbani kutoka kisimani.

Yunus Fundi, mkazi mwingine wa kijiji hicho, anasema ugumu katika kuyapata maji, unachangia kushindwa kufanya shughuli za kiuchumi kwa kuwa muda mwingi anautumia kusaka maji.

"Nikikosa maji ina maana shughuli zangu zinakwama, hata chakula siwezi kupika. Hebu niambie, hauna maji utapika kwa kitu gani, hii pombe utaitengeneza na nini?" anahoji Yunus anayejishughulisha na utengenezaji wa pombe za kienyeji kijijini huko.

**UZOEFU KIJIJINI**

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Chihanga, Henry Sudani, anasema maji hayo yanayopatikana umbali kutoka kwenye makazi yao, siyo salama kiafya lakini wanayatumia kwa kuwa hawana namna nyingine ya kupata majisafi na salama.

"Kama ulivyojionea, mifugo inakunywa kisimani na wananchi wanachota maji hayo hayo, labda kungekuwa na utenganisho wa binadamu na wanyama ingesaidia, lakini sasa mifugo inakunya hapo hapo kisimani, yaani mazingira sio mazuri," anasema.

Sudani anasema mbali na uharibifu wa mazingira, visima hivyo ni hatari kwa sababu havijajengwa katika mazingira bora, akikumbusha kuwa kuna wakati watu huteleza na kuanguka.

Mmoja wa wafugaji, Ernest Makali anaeleza kuwa wanapata shida katika upatikanaji wa maji na kujikuta wakitumia muda mwingi kisimani huko kuhakikisha mifugo yao inapata maji ili inywe na kuipeleka kwenye malisho.

"Eneo hili la visima sasa linakuwa na msongamano mkubwa wa mifugo inayoletwa kwa ajili ya kupata maji na wananchi wanahitaji huduma hiyo hiyo.

"Huu ukame umesababisha baadhi ya visima kukauka maji ndiyo maana unaona kuna ng'ombe wengi kwenye foleni ya kusubiri maji, hapa wanakuja ng'ombe zaidi ya 2,500 kwa siku," anabainisha.

Makali anasema visima hivyo vinamilikiwa na wananchi na utaratibu uliowekwa kwa wafugaji wanapotaka kuyatumia kwa ajili ya mifugo, wanalipia kulingana na ukubwa wa kundi la ng'ombe walionao.

"Kwa mwaka unaweza kulipa laki moja (Sh. 100,000) na kama una kundi dogo la wanyama, utatakiwa kulipa Sh. 50,000. Kwa hiyo, wananchi inawabidi wasubiri mifugo ipate huduma hiyo kwanza kwa sababu wao hawalipii maji haya.

"Ukiamua kutafute maji eneo lingine tofauti na hapa, inabidi ufunge safari ya umbali wa Km tisa, ni safari ndefu, hivyo inatulazimu kuendelea kubaki hapa.

"Mifugo mingi inaletwa hapa kupata maji. Kuna siku tunakosa maji, tunajikuta tunapanga foleni na mifugo yetu kusubiri kupata maji," Makali anabainisha.

Juma Monyo, mmoja wa wasimamizi wa visima hivyo, anasema wananchi wachota maji bila malipo lakini wafugaji huyalipia kulingana na wingi wa mifugo waliyonayo.

"Ukame umechangia maji kukauka, kile kisima changu maji yanakauka mapema. Nimewaambia hawa wafugaji tuchimbe, wapo kimya, nipo hapa ninaangalia atakayechota na kunyweshwa mifugo yake anipatie fedha yangu," anasema.

**HATARI KIAFYA**

Diwani wa Mima, Bezarery Mnyambwa anasema mazingira ya mwingiliano wa mifugo na binadamu katika utumiaji wa maji hayo ya visima, yanawaweka hatarini kupata magonjwa ya mlipuko.

Kwa kutambua hatari hiyo, diwani huyo anasema kuna haja kuwapatia huduma ya majisafi na salama wananchi ili waache kuchangia maji na mifugo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpwapwa, George Fuime, anasema kinachoshuhudiwa sasa katika maeneo yao, ni matokeo ya athari za mabadiliko ya tabianchi yaliyochangiwa na mazingira kuharibiwa huku akilalama shida hiyo kufumbiwa macho na baadhi ya viongozi, hasa wa ngazi za chini.

"Watendaji wetu wanapokwenda, kazi ya usimamizi wa mazingira haifanyiki vizuri, watu wanakata misitu ndiyo maana uona hakuna maji, hii imetuathiri kwa kiwango kikubwa," anasema.

Fuime anabainisha kuwa hivi karibu kuna operesheni imefanyika ya kuwaondoa wale wote waliovamia maeneo ya vyanzo vya maji na ya hifadhi ili kuacha kuharibu mazingira.

Ria yake kwa serikali ni kutunga sheria kali, akiwa na ufafanuzi kwamba zilizoko anaziona ni za zamani na zinachochea wananchi kufanya uharibifu wa mazingira wakijua watalipa faini na kuendelea kuharibu mazingira.

"Mvua za vuli mpaka sasa hazijanyesha, ni matokeo ya uharibifu wa mazingira ndiyo maana tunaona maji yamekuwa ya shida na vyanzo vingi vya maji vimeanza kukauka," Fuime analalamika.

Kuhusu hali iliyoshuhudiwa na Nipashe kijijini Sazima, Fuime ananyooshea kidole anachokiita kutokuwapo usimamizi mzuri wa visima hivyo, hali inayochangia wananchi kuchangia maji na mifugo.

**HATUA SERIKALINI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mpwapwa, Mwanahamisi Ally, anakiri wananchi kuchangia maji na mifugo sio salama kiafya, akiuagiza Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani humo kuongeza miundombinu ili wananchi wapate majisafi na salama.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mpwapwa, Cyprian Warioba, anasema wana mradi wa maji wa muda mrefu katika Kijiji cha Sazima ambacho kinakabiliwa na shida katika kupata maji kutokana na idadi kubwa ya watu walioko huko.

Warioba anasema mkakati wao katika bajeti ya mwakani ni kuongeza ukubwa wa tangi na miundombinu ya maji ili kuwawezesha wakazi wa kijiji hicho kupata majisafi na salama.



TANGAZO

## SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
## MAMLAKA YA KUDHIBITI DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR

# Miaka miwili ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi madarakani na mafanikio ZDCEA

Ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi kuiongoza Zanzibar na kuunda Mamlaka ya kudhibiti dawa za kulevya, mamlaka hiyo inajivunia uwepo wa baadhi ya mafanikio.

Kamishna wa mamlaka hiyo Kanali Burhan Zuberi Nassor anasema miongoni mwa mafanikio hayo ni Kutungwa kwa Sheria mpya ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya Zanzibar ambapo mamlaka hiyo imepewa nguvu ya kupeleka kesi za dawa za kulevya mahakamani.

Anasema pia mafanikio mengine ni Kuanza kutumika kwa kituo cha kinga, tiba na marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya ambao wameamua kuacha matumizi ya dawa hizo huko kidimni

Pia anasema Kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa na kutoa taaluma ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya kwa jamii kupitia vyombo vya habari .

Anasema jumla ya kesi 254 zimeripotiwa ambapo watuhumiwa wake ni wanawake na wanaume na kati ya hizo kesi 150 zimeshafikishwa mahakamani .

Anasema mamlaka hiyo inashirikiana na taasisi zingine katika kupambana na kudhibiti biashara ya dawa za kulevya.

Aidha anasema mamlaka hiyo inashirikiana na taasisi zote, aidha mamlaka inamashirikiano na taasisis za kikanda, kitaifa na kimataifa katika kupambana na dawa za kulevya na inashirikiana na taasisi mbalimbali za ndani na nje katika kuwasaidia kuwatibu waraibu wa dawa za kulevya.

Akizungumzia changamaoto zilizopo anasema bado uamuzi wa mahakama hauendani na matakwa ya sheria, bado muitiko wa jamii ni mdogo katika kutoa taarifa za wahalifu wa dawa hizo, uwepo wa Zanzibar katika ukanda wa Afrika mashariki na uwepo wa bandari bubu ambapo baadhi ya wahalifu huzitumia kupitisha dawa za kulevya.

Anasema katika kutatua changamoto hizo mamlaka hiyo imepewa jukumu la kukabiliana na uhalifu wa dawa za kulevya kwa kuunda kamati za ulinzi za mikoa katika kukabiliana na uhalifu huo katika sehemu hizo.

Aidha alitaka jamii kushirikiana pamoja na mamlaka hiyo katika kuwafichua wahalifu wa dawa za kulevya ili kudhibiti uingizaji, utumiaji na usambazaji wa dawa za kulevya ambapo dawa hizo zinaliathiri taifa la baadae ambalo kundi kubwa ni vijana.

# SALAMU ZA PONGEZI

KISHINDO CHA
MIAKA
**OFISINI** **2**

**Kamishna Mkuu, Uongozi na Wafanyakazi wa mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya zanzibar wanaungana na Watanzania wote kumpongeza Mheshimiwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutimiza miaka miwili ofisini kwa mafanikio Makubwa .**

***ZANZIBAR BILA DAWA ZA KULEVYA INAWEZEKANA***



Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi

217132702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua ya serikali itapunguza kilio wananchi uhaba wa maji

**MAMLAKA** ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) hivi karibuni ilitangaza kuwapo kwa mgawo wa maji katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kutokana na kupungua kwa kina cha maji katika Mto Ruvu, hivyo kuathiri uzalishaji wa huduma hiyo muhimu.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya kamati za ulinzi na usalama za mikoa hiyo zikiongozwa na wakuu wa mikoa, kutembelea maeneo ya uzalishaji wa maji na kujionea upungufu mkubwa katika vyanzo hivyo. Katika kutekeleza hilo, DAWASA ilitoa ratiba ya mgawo ili kuhakikisha pamoja na upungufu huo, wananchi wanapata huduma hiyo muhimu kwa maisha ya kila siku.

Pamoja na kuwapo kwa ratiba hiyo, kumekuwa na vilio kutoka kwa wananchi kila kona wakilalamikia kutokufuatwa, hivyo makali ya upatikanaji wa maji kuzidi kuongezeka. Pia kumekuwa na 'maandamano' ya wananchi kusaka maji kila sehemu jambo linaloashiria kuwa shida ya maji inaongezeka.

Kuwapo kwa hali hiyo, kumesababisha serikali kuingilia kati ili kujaribu kupunguza makali ya ukosefu wa maji kwa wananchi wa mikoa husika kwa kutafuta vyanzo mbadala tofauti na kile cha Mto Ruvu ambacho kina cha mto kimepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ukosefu wa mvua uliosababisha pia ukame.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliingilia kati tatizo hilo kwa kutoa maagizo kwa Wizara ya Maji kushirikiana na sekta binafsi kutekeleza mradi wa kutoa maji Mto Rufiji ili kusambaza maji maeneo ya mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Sambamba na hilo, aliielekeza DAWASA kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uchimbaji wa visima zaidi ili kuongeza uzalishaji wa maji.

Majaliwa alitoa maagizo hayo baada ya kuelekezwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha anasimamia uunganishwaji wa maji kutoka Kigamboni kwenda maeneo mengine ya Dar es Salaam. Majaliwa alisema visima vya Kigamboni vina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 70 kwa siku, hali ambayo itasaidia kupunguza tatizo la maji katika mkoa wa Dar es Salaam.


Hatua ya serikali kuingilia kati kupunguza tatizo la maji mkoani Dar es Salaam imekuja wakati mwafaka hasa kutaka ushiriki wa sekta binafsi kutoa huduma kwa kutafuta vyanzo vya maji ikiwamo kutoa maji Mto Rufiji na kuyafikisha Dar es Salaam.

Ni imani kwamba ushiriki wa sekta binafsi katika uzalishaji maji utasaidia kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa maji badala ya kutegemea DAWASA pekee ambayo ni dhahiri inaonekana kushindwa kutimiza mahitaji. Hii inatokana na ukweli kwamba katika mkoa wa Dar es Salaam, mathalan, kuna ongezeko kubwa la watu lakini upatikanaji wa maji ni mdogo.

Suala la kutoa maji mto Rufiji ni la kupongezwa licha ya kwamba miaka nenda rudi kumekuwa na kilio cha kufanya hivyo kwa kuwa maji yanayotoka katika vyanzo mbalimbali na kuingia katika mto huo, yamekuwa yakiishia baharini huku wananchi wakiteseka.

Pamoja na hayo, ni vyema DAWASA ikaacha ukiritimba wa utoaji wa huduma ya maji huku ikiweka masharti magumu kwa watoa huduma binafsi wakiwamo wamiliki wa visima ambao kabla ya mtandao wa mamlaka hiyo kuenea, walikuwa wanawasaidia wananchi kupata maji. Baadhi ya wamiliki wa visima binafsi walikuwa wakiweka mtandao wa mabomba kwenye makazi ya watu, hivyo kufidia pengo lililokuwapo la upungufu wa maji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Sote wananchi tutumie maji kwa uangalifu kipindi hiki cha uhaba

Na Adam Fungamwango

**HIKI** ni kipindi kigumu kwa Watanzania, baada ya kuwapo uhaba mkubwa wa maji, kutokana na ukame sehemu mbalimbali za nchi hali iliyosababisha maji kupungua kwenye mito na mabwawa.

Pia ikumbukwe hata katika msimu uliopita, nchi yetu haikupata mvua ya kutosha, ambayo imechangia jambo hilo ambalo unaweza kuliweka kwenye matatizo ya tabianchi.

Ni wakati ambao viongozi wa serikali wanachukua hatua kadhaa kukabiliana na adha hiyo, ili kuwanusuru wananchi wao wasiendelee na adha hii ambayo imekuwa kero kubwa hasa kwa kinamama.

Siku zote ambazo maji yanakuwa ya shida, kwa asilimia 90 na zaidi wanaoteseka ni kinamama, kwani wao ndiyo wana matumizi makubwa ya maji kutokana na kuwa kiongozi wa familia.

Wanalazimika kuamka mapema kwenda bombani au visimani kwa ajili ya kuchota au kusaka maji, na huko wakati mwingine wasipate au wanakutana na foleni kubwa.

Wakati mwingine kutokana na kuamka alfajiri sana, wanakumbana na changamoto mbalimbali ambazo zinawakwaza na kuwasababisha matatizo mbalimbali.

Wanawake kuna wakati wanachelewa kurudi majumbani kutokana na kutafuta maji kwa umbali mrefu na kuwakuta waume zao wamenuna, au wamefura kwa hasira ambazo wanakuwa hawaamini kama kweli kipindi chote hicho alikuwa bombani, kisimani au alikuwa amepatia sababu.

Kutokana na hayo yote, niliyoainisha na mengine, imefika wakati sasa kuwa na matumizi bora ya maji kwa wakati wa kipindi hiki cha ukame. Maji yanapatikana, lakini kwa shida. Hivyo, kwa sasa matumizi yawe ya bajeti na si kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

Ni sawa tu na wakati wa njaa, au uhaba wa chakula ambao familia inalazimika kupika kwa bajeti, ili kuweka akiba kinachobaki kwa ajili ya kutumika kwa muda mrefu.

Kama familia inakula mchana saa sita na saa mbili usiku, wakati wa njaa, inaweza kuamua sasa watakuwa mara moja. Wakishakunywa chai asubuhi, basi wanaweza kula saa 10 jioni hadi kesho yake mpaka kipindi hicho cha mpito kitakapopita.

Sitegemei kwa sasa mtu akipata ndoo moja, basi yote anakwenda kuoga mtu mmoja. Angalau basi ndoo moja aoge baba na mama, ili kumpa nafuu mwanamke ambaye, kila kukicha adamke asubuhi kusaka maji.

Kuna wakati mwingine maji yanapotea kwenye mabomba kwa ajili ya kumwagia bustani tu. Huo nao pia ni upotevu wa maji bila ya sababu yoyote ya msingi.

Maji, hasa ya bomba, kwa sasa yanatakiwa yatumike kwenye sababu za msingi tu ambazo ni lazima yatumike. Mtu anatumia maji ya bomba kuloweka tu nguo chafu na kuziweka siku nzima, wakati kuna wenzake wanakosa hata maji ya kunywa.

Kuna baadhi ya familia huwa na hazina kupitia vyombo vya kuhifadhi maji, wenyewe akichota wakioga, kupikia na kufua basi yakiisha wanakwenda tena kuchota. Hiyo siyo sahihi hata kidogo.

Ifike wakati Watanzania tuwe na utaratibu au utamaduni wa kuwa na vitu vya kuhifadhia maji, ili ikitokea dharura kama hii basi angalau athari wenye familia zetu haziwi kubwa sana.

Ni sawa tu na wale wanaonunua vyakula kama mchele, unga sukari, mafuta ya kupikia na kuweka ndani, hawa hata kama siku hana pesa, au anayo kidogo hawatolala na njaa.

Kwa sababu wana akiba ya chakula ndani, tofauti na wale ambao wanatafuta pesa kila siku kwa ajili ya kununua unga nusu au kilo moja ili wapike ugali. Familia hii siku ikikosa pesa, italala na njaa.

Akiba na bajeti ni vitu muhimu sana. Siku hizi kuna matangi ya kuhifadhia maji kwa wale wenye uwezo, lakini kwa watu wa kipato cha kawaida kuna vyombo vya kuhifadhi maji vinaitwa 'majaba'.

Haya yanaweza kusaidia kipindi ambacho maji yanatoka kujaza ya kutosha ili ikitokea hali kama hii yanasaidia kuondoa presha ya kusaka maji kwa nguvu zote na mahali popote.

Kwa hili lililotokea sasa liwe funzo, kwanza Watanzania kuanza kutumia maji kwa uangalifu na maeneo muhimu tu na si kumwagamwaga ovyo, pia tuwe na utaratibu wa kuhifadhi maji.

## Mbunge awachongea DC, mwenyekiti wa CCM kwa madai ya kumkwamisha

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MBUNGE wa Nkasi, Aida Khenani, amemtuhumu Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali, kwa madai ya kushirikiana na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya kuwazuia madiwani kushirikiana naye katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Khenani alisema hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika eneo la stendi ya zamani ya mabasi mjini Namanyere wilayani humo, uliolenga kusikiliza na kutatua kero ya upatikanaji wa huduma ya maji katika mji huo.

Alisema kinachomsikitisha ni kuwa viongozi hao ambao walipaswa kutoa dira katika kushughulikia changamoto za maendeleo katika wilaya, wamekuwa mstari wa mbele kuwazuia madiwani wanaotokana na CCM kushirikiana naye.

"Mkuu wa Wilaya Lijualikali na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hawa wote walikuwa CHADEMA. Kinachonishangaza tangu wamejiunga CCM eti wanazuia madiwani kutoa ushirikiano kwangu. Sisi ndio wenyeji wa wilaya hii na lazima tushirikiane kwa ajili ya maslahi mapana ya maendeleo ya jimbo, wilaya na mkoa," alisema.

Alisisitiza kwamba wanachokifanya mkuu wa wilaya na mwenyekiti wa CCM ni sehemu ya kukiuka maridhiano ya kufanya kazi kwa ushirikiano yaliyofikiwa kati ya Rais Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

Mmoja wa Madiwani wa CCM katika halmashauri hiyo ambaye aliomba jina lake kuhifadhiwa, alisema ni kweli wamezuia kushiriki vikao vya mbunge huyo na iwapo watabainika kufanya hivyo watatozwa faini ya fedha kiasi ambacho hakuwa tayari kukitaja.

Alipohojiwa na gazeti hili jana, Lijualikali alisema hana ugomvi wowote na mbunge huyo amekuwa akishangaa kusikia anamlalamikia kupitia majukwaa ya kisiasa. "Mimi sijamkataza diwani yeyote asifanye kazi na mbunge huyo. Hata hayo malalamiko anayotoa Khenan sijui yanatoka wapi? Alihoji.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Nkasi, Aljabry Keissy, alipoulizwa kuhusu shutuma hizo, hakukataa wala kuthibitisha lakini alisema kuongoza kuna mbinu zake na mara kadhaa amekuwa akimwita mbunge huyo ili aende kuzungumza lakini amekuwa akikataa.

Khenan akiwa mbunge wa viti maalumu mkoa, aliwahi kuzuiwa na aliyekuwa mkuu wa wilaya hiyo, Said Mtanda, kukabidhi msaada wa mabati katika Shule ya Msingi Namanyere ambako amepata elimu yake ya msingi.

Badala yake, mkuu huyo wa wilaya alimtaka mbunge huyo kufika ofisini kwake ili kumkabidhi yeye mwenyewe msaada huo uliokuwa na thamani ya Sh. milioni 1.4 badala ya kupeleka shuleni hapo.




Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua mauzo ya vipande vya mfuko wa uwekezaji wa pamoja wa Faida Fund, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Kampuni ya Watumishi Housing Investments (WHI), Hosea Kashimba na (wa pili kushoto) ni Mkurugenzi Mtendaji wa WHI, Dk. Fred Msemwa. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Tanzania, China zakubaliana kudumisha uhusiano kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa China, Xi Jinping, wamekubaliana kuendeleza uhusiano na ushirikiano baina ya nchi hizo mbili.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa jana ilieleza kuwa viongozi hao walifikia makubaliano hayo kwenye mkutano baina yao uliofanyika Beijing, China.

Rais Samia yuko kwenye ziara ya siku mbili nchini China inayotarajiwa kumalizika leo na alikuwa na mazungumzo ya kina na mwenyeji wake kuhusu uhusiano na ushirikiano baina ya nchi hizo mbili.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, viongozi hao pia mbali na kuzungumzia kwa kina uhusiano wa China na Tanzania, walizungumzia uhusiano wa Afrika na China, masuala ya kimataifa na kikanda ambayo mataifa hayo yana maslahi ya pamoja.

Taarifa hiyo ilisema viongozi hao walisisitiza kuhusu uhusiano wa muda mrefu kwenye nyanja mbalimbali baina ya watu wa China na Tanzania na kuelezea mafanikio ambayo nchi hizo zimepata kwa miaka 58 tangu kuanza kwa uhusiano wa mataifa hayo.

Katika kukuza uhusiano wa nchi hizo mbili, viongozi hao walitangaza mikakati madhubuti ambayo utekelezaji wake utayasaidia kuendeleza ushirikiano na uhusiano walio nao kwa sasa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, viongozi hao walikubaliana kuendeleza diplomasia iliyopo na kubadilishana uzoefu katika utawala na ushirikiano wa serikali kuu na zile za mitaa, wabunge na vyama vya siasa katika ngazi zote.

Rais Samia alimpongeza Rais wa China kwa kufanikisha mkutano wa 20 wa chama tawala cha Kikomunisti (CPC) na kusifu mafanikio ambayo nchi hiyo imeyapata na mabadiliko ambayo imeyafanya kwenye nyanja mbalimbali chini ya uongozi wa CPC.

Kwa upande wake, Rais wa China aliipongeza serikali ya Tanzania kwa mafanikio ambayo imeyapata kwenye sekta mbalimbali chini ya uongozi wa Rais Samia na kuutakia mafanikio mkutano mkuu ujao wa 12 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aidha, pande hizo mbili zimekubaliana kuendelea kusaidiana katika masuala mbalimbali yakiwemo yanayohusu utaifa.

Taarifa hiyo ilisema mataifa hayo yamekubaliana kuendeleza ushirikiano kwenye uwekezaji ambapo China itahamasisha kampuni nyingi zaidi kutoka nchi hiyo kuwekeza Tanzania na kushiriki katika ujenzi wa miradi ya maendeleo kama reli, barabara, bandari, usafiri wa anga, umeme, mawasiliano na miundombinu mingine.

Tanzania kwa upande wake imeahidi kuendelea kuweka mazingira mazuri ya biashara na kuweka mazingira bora kwa makampuni ya China kuja kuwekeza Tanzania.

Rais Samia alielezea furaha yake kwa mapokezi makubwa aliyoyapata na ukarimu wa watu wa China na amemwalika Rais Xi Jinping kutembelea Tanzania mwaka 2024 katika sherehe za miaka 60 ya Muungano wa Tanzania.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
03/11/2022

**TANGAZO**


1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 04/11/2022 kampuni ya **LIUHE INTERNATIONAL LIMITED** itasafirisha Gari zenye vipimo vikubwa kutoka Dar es Salaam kuelekeaa Kigoma Gari hizo zenye namba za usajili: **T199DQG/T130DQG na T637DLY/T884DMJ**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   - **I. T199DQG/T130DQG Urefu 20 Upana 4.9 Kimo 4.8**
   - **II. T637DLY/T884DMJ Urefu 20 Upana 4.1 Kimo 4.8**
3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam hadi Kigoma Kupitia Dodoma,** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

117132302


## KABWELA

**Fadhili Mohamed**






Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Slyvester Mwakitalu (wa pili kulia), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa Mkuu wa Gereza la Mahabusu la Segerea, SSP Hamis Lissu, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya matumizi ya watoto wanaoishi katika vizuizi vya kisheria ambao wanatunzwa katika gereza hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makandarasi RUWASA malipo sasa kidigitali

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), unaandaa mfumo utakaowawezesha makandarasi wake kufuatilia malipo yao kwa njia ya kielektroniki.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Mhandisi Clement Kivegalo, wakati wa mkutano na wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari.

Alisema wanaandaa mfumo huo kwa kushirikiana na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maji na kwamba lengo ni kuondoa ukiritimba na ucheleweshaji wa malipo ya makandarasi.

Aidha, alisema imeamua kuja na mfumo huo baada ya malalamiko ya makandarasi kucheleweshewa malipo yao hali ambayo inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji na kusababisha malalamiko ya watu.

Alisema kupitia mfumo huo ambao uko kwenye majaribio, mkandarasi anaweza kuingia kwenye mfumo kupitia simu yake ya mkononi na kuangalia malipo yake yamefikia sehemu gani bila ya kufunga safari kwenda RUWASA au kupiga simu mara kwa mara.

"Tunataka mkandarasi akishakabidhi hati zake za madai RUWASA asilazimike kurudi tena au kupiga simu mara kwa mara. Kupitia mfumo huu ambao tunaufanyia majaribio kwenye mikoa mitano mkandarasi atakuwa na uwezo wa kuchungulia kupitia simu yake malipo yake yako sehemu gani," alisema.

Kivegalo alisema mfumo huo utampa muda maalum mtu anayehusika na malipo ya mkandarasi na muda huo utakapopita bila kufanya malipo utajifunga na hivyo mhusika hatakuwa na uwezo wa kuingia kwenye jalada la mkandarasi anayedai malipo hadi apate kibali cha bosi wake au Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA.

"Sasa kesi za kuchelewa kumlipa mkandarasi zikiwa nyingi tutajua huyu mtu tuliyenaye hatufai kwasababu moja ya wajibu wetu wa msingi RUWASA ni kuhakikisha tunawalipa kwa muda mwafaka ili watekeleze miradi kwa wakati na kwa viwango," alisema Kivegalo.

Alisema wameamua kufanya hivyo ili kuweka uwajibikaji kwa watumishi wa wakala wanaohusika na malipo kubaini atakayezembea kufanya malipo hayo kwa wakati uliopangwa aweze kuwajibishwa na kutoa maelezo kwanini ameshindwa kutimiza wajibu wake.

"Huu utaratibu wa mtu kuamua amlipe nani na wakati gani ni ukiritimba ambao unasababisha hisia za rushwa na umeleta malalamimko mengi lakini sasa mwarobaini wa haya yote ni mfumo huu mpya kwasababu mhusika hatalazimika amwone mtu ana kwa ana ndipo amlipe," alisema.

Alisema kwa muda mrefu kulikuwa na malalamiko kwa miradi mingi kujengwa kwa kiwango hafifu na kuharibika baada ya muda mfupi baada

# Wananchi Monduli walia upungufu chakula

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa** MONDULI

MKUU wa Wilaya ya Monduli, Frank Mwaisumbe, amesema wilaya hiyo inapitia wakati mgumu wa upungufu wa chakula na kuiomba serikali iwapunguzie zaidi bei waweze kumudu gharama.

Akizungumza na Nipashe, alisema uongozi wa wilaya hiyo umefanya jitihada mbalimbali kukabiliana na tatizo hilo.

"Ni kweli hata sisi katika wilaya yetu kuna maeneo ambayo yamekuwa na shida kubwa sana ya chakula na tumeongea na Wizara ya Kilimo na bahati nzuri waziri kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), wametuletea chakula cha bei nafuu," alisema Mwaisumbe.

Alisema mpaka sasa wilaya hiyo imepelekewa chakula cha bei nafuu tani 300 aina mbalimbali za nafaka.

"Lakini bado kuna uhitaji mkubwa sana, tutafurahi kama tutaongezewa kingine," alisema Mwaisumbe.

Alisema wamepeleka maombi ya kupunguziwa zaidi bei ya chakula hicho kutokana na hali mbaya ya kiuchumi inayowakabili wananchi wa eneo hilo.

Kwa sasa kilo moja ya mahindi ambayo hayajakobolewa inauzwa Sh. 2,000 kwa maduka ya reja reja.

"Hali ni mbaya kwa wananchi. Pamoja na serikali kuwaletea chakula hicho cha bei nafuu, wanaendelea kuomba ipunguzwe zaidi kwa sababu hali yao kiuchumi sio nzuri," alisema Mwaisumbe.

"Wananchi wengi katika wilaya hii wanategemea sana mifugo katika kuendesha maisha yao, kipindi hiki cha ukame imekufa sana na hiyo iliyopo haiuziki, imekonda kwa sababu ya kukosa malisho, kwa hiyo hata hiyo fedha ya kununulia hicho chakula baadhi wanakosa."

Mwaisumbe alisema tayari wamepeleka maombi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha na miongoni mwa maombi hayo ni suala la bei ya chakula cha dharura wanachopelekewa wananchi kuwanusuru na njaa.

"Bado tunasubiri majibu kutoka kwenye ofisi ya mkuu wa mkoa na uzuri ametuahidi kwamba analishughulikia," alisema Mwaisumbe.

Naseriana Meloki, mkazi wa kijiji cha Kilotorok, alisema kilio chao ni kuona serikali inawafikiria zaidi kwa kuwauzia kwa reja reja tofauti na sasa wanatakiwa kununua kuanzia kilo 50.

"Ukienda kwenye hicho chakula cha bei nafuu, kinauzwa kwenye viroba vya kilo 50 na hawakubali kununua chini ya hapo, kwa hiyo tunachofanya tunaungana tunachanga fedha ndio tunanunua, kama tukikwama kufikisha hicho kiwango inatulazimu tukanunue dukani kwa Sh. 2,200 kilo moja," alisema Naseriana.

Naomi Stephano, mkazi wa kijiji cha Nanja, aliiomba serikali kuwauzia chakula kuanzia kilo moja kutokana na hali ya uchumi waliyonayo kwa sasa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nanja, Yamati Lemomo, alikiri baadhi ya wananchi katika kijiji chake kushindwa kumudu kununua chakula hicho cha bei nafuu kwa kilo 50 na tayari wameomba serikali ilifikirie.

Kwa mujibu wa NFRA, chakula cha bei nafuu kinauzwa kilo moja kuanzia Sh. 1000 hadi 1,600 na mpaka sasa halmashauri zilizokwishapelekewa chakula hicho ni Monduli, Longido, Sengerema, Geita, Nzega, Liwale, Nachingwea, Liliondo, huku tani 3,000 ndizo zilizosambazwa katika maeneo hayo.

NFRA imesema wataendelea kusambaza chakula hicho cha bei nafuu kwa kadri ya uhitaji na kuhakikishia wananchi kipo cha kutosha.

# Bil. 13/- kunufaisha wakulima wadogo

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKA la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA), limeingia mkataba wa miaka minne wa zaidi ya Sh. bilioni 13 kwa ajili ya kuongeza thamani ya kilimo kwa wakulima wadogo.

Vilevile, mkataba huo utasaidia kuimarisha usalama wa chakula na lishe miongoni mwa wakimbizi na jamii zinazowahifadhi mkoani Kigoma. Mkoa wa Kigoma umekuwa ukiwahifadhi zaidi ya wakimbizi 200,000 kutoka nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Burundi.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya utiaji saini, Mkurugenzi wa KOICA nchini Tanzania, Kyucheol Eo, alisema mbali na kuwasaidia wakimbizi waliopo Kigoma, utatoa fursa kwa wakulima wa mazao mbalimbali mkoani humo na mikoa ya jirani.

Alisema zaidi ya wakulima wadogo 20,000 watasaidiwa kwenye kilimo chao na kuwainua kwa kipato pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi, kiufundi, kifedha na kilimo wa mashirika ya kijamii katika eneo hilo.

"Sina shaka kuwa mradi huu utaimarisha mnyororo wa thamani wa kilimo cha wakulima wadogo na kuboresha usawa wa kijinsia na amani katika wilaya zinazohifadhi wakimbizi mkoani Kigoma," alisema Eo.

Alisema kwa ushirikiano huo, wataendesha mradi wa pamoja wa 'Kilimo Tija Kigoma (KITIKI)' ambao utawafanya wakulima wadogo hapa nchini ambao wengi wao ni wanawake, kupata mafunzo ya mbinu bora za kilimo, utunzaji wa mazao baada ya kuvuna na kupata masoko.

Mkurugenzi wa WFP nchini Tanzania, Sarah Gordon-Gibson, alisema WFP itaunganisha wakulima na jamii za wakimbizi ili kuwapatia soko ambalo liko tayari kwa mazao yao.

"WFP inashukuru kwa msaada mkubwa kutoka serikali ya watu wa Jamhuri ya Korea, kupitia ushirikiano na KOICA, hatuwezeshi tu wakulima wadogo, bali pia tunachangia katika muunganiko wa vipengele vitatu vya misaada ya kibinadamu, maendeleo na ujenzi wa amani mkoani Kigoma," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema Julai mwaka huu, WFP ilianza utekelezaji wa mpango mkakati wake hapa nchini wa miaka mitano ambao utasaidia kuchangia maendeleo katika masuala ya kiuchumi, kijamii na kimazingira ya usalama wa chakula na lishe kwa wakimbizi.

Pia alisema mpango huo utasaidia wakulima wadogo wa kitanzania na kujenga jamii inayostahimili hali ya hewa, kukuza mshikamano wa kijamii na usawa wa kijinsia.

Alisema WFP itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali na aliishukuru serikali kwa ushirikiano wanaoutoa kufanikisha utendaji wa shughuli za WFP hapa nchini.

## Shekhe awa mbogo kuporomoka maadili

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHEKHE wa Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa, amejia juu wazazi na walezi kuhusu kushuka maadili ya watoto na kuwataka kujenga tabia ya kuhimiza kufuata na kufanya mambo yenye maadili mema.

Mtupa ameyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye Maulidi iliyoandaliwa na Waislamu wa mkoa wa Pwani kwa ajili ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad SAW yaliyofanyika Mailimoja, Kibaha.

Alisema ni wakati sasa wazazi kubadilika na kuongozana na watoto wao kila wanapokwenda kwenye mambo yanayowajenga kimaadili ambayo yatawasaidia kuepuka na kujiingiza katika makundi ya uhalifu.

Shekhe Mtupa alisema kuna baadhi ya wazazi wanaenda kwenye sehemu za ibada wenyewe bila kuambatana na watoto wao jambo linalowafanya watoto kujilea na kufuata njia zisizo sahihi na kujipangia maisha yao.

"Wazazi wengi katika mambo ya heri yenye ustawi wa jamii wanafanya wenyewe na kuwaacha watoto wao wakijiendesha watakavyo. Hili linachangia baadhi ya vijana kujiunga na makundi ya 'panya road'. Haya ni matokeo ya kuwaacha wenyewe," alisema.

Alisema tabia hiyo ya wazazi kutowashirikisha watoto katika mambo yenye ustawi wa jamii pia yamemfanya kijana kutopenda kufanya kazi na badala yake kujiweka kwenye mstari wa kupata mafanikio kwa njia zisizo za halali ambazo ziko katika mmomonyoko wa maadili.

Mtupa alisema katika Maulidi zitakazokuwa zinaendelea kufanyika kwenye mkoa, ngazi ya wilaya ajenda ya mtoto itapewa kipaumbele ili wazazi wabadili mfumo wa malezi na kuondoa uwapo wa vijana wanaojihusisha na makundi ya uhalifu.

Akizungumzia mpango mkakati ndani ya mwaka mmoja ambao ulizinduliwa mwaka 2021, Mtupa alisema tayari wamejenga msikiti mkubwa na sasa wako katika hatua za ukamilishaji wa kituo cha afya. Kwa mujibu wa Mtupa, kila wilaya utaratibu huo uliofanyika kwa ngazi ya mkoa utafika pia kwenye wilaya kuhakikisha zinakuwa na msikiti mkubwa mzuri pamoja na kituo cha afya kitakachotoa huduma kwa wananchi.

Kuhusu ukame ambao umesababisha kupungua kwa maji kwenye vyanzo, Mtupa alisema wana mpango wa kuombea mvua ili vyanzo vya maji vijae na kuondoa mgawo ambao unasambaa katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

# Tanzania na Korea Kusini zaingia mkataba kuimarisha sekta ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeingia makubaliano na Wizara ya Ardhi, Miundombinu na Usafirishaji ya Korea Kusini kuimarisha sekta ya ardhi.

Makubaliano hayo yalitiwa saini juzi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula na mwenzake wa Korea Kusini, Won Hee-ryong mjini Seoul, Korea Kusini, kupitia hati ya makubaliano (MOU) ya ushirikiano kwenye sekta ya ardhi na menejimenti ya taarifa za kijiografia.


Makubaliano ya nchi hizo mbili yanalenga kuweka mazingira rafiki kwa Watanzania kupata utaalamu na uzoefu kwenye nyanja za upimaji na ramani kupitia mipango na miradi ya mafunzo ya kuendeleza rasilimali watu kwa maendeleo endelevu ya sekta ya ardhi. Pia yanalenga kuwapo kwa fursa zaidi kwa Watanzania kupata mafunzo ya muda mrefu nchini Korea.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, lengo lingine ni kuimarisha ushirikiano ulioko kati ya Wizara ya Ardhi ya Tanzania na ile ya Korea Kusini katika kukuza matumizi ya teknolojia za kisasa kwenye sekta ya ardhi ili kuboresha utoaji huduma katika fani zote za utawala wa ardhi na kutimiza azma ya serikali ya kusajili ardhi yote nchini.

"Wizara inaona kuna umuhimu wa kuwa na makubaliano rasmi ya kukuza na kuimarisha ushirikiano wa nchi hizi mbili kupitia Wizara ya Ardhi na wenzetu wa Korea kupitia Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya ardhi na menejimenti ya taarifa za kijiografia," alisema Dk. Mabula.

Mbali na utiaji saini makubaliano hayo, Dk. Mabula akiwa nchini Korea Kusini atashiriki mijadala kwenye Maonyesho ya Maendeleo ya Teknolojia ya Taarifa za Kijiografia (Smart Geospatial Expo 2022).

Maonyesho hayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka sambamba na mikutano ya majadiliano ya kuanzisha na kukuza ushirikiano kwenye sekta ya ardhi inayowakutanisha viongozi wa juu wa serikali na kampuni za kimataifa zinazojihusisha na taarifa za kijiografia kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa ardhi.




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kulia) na Waziri wa Ardhi, Miundombinu na Usafirishaji wa Korea Kusini, Won Hee-ryong, wakionesha hati ya makubaliano ya ushirikiano kwenye sekta ya ardhi na menejimenti ya taarifa za kijiografia baada ya kutiliana saini, jijini Seoul Korea Kusini jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC abaini madudu ujenzi vituo vya afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MKUU wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Jerry Muro, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwachunguza watumishi watatu waliokuwa wanasimamia ujenzi wa kituo cha afya baada ya kubaini Sh. milioni 500 zilitolewa na serikali zimemalizika na mradi haujakamilika.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa kituo cha afya cha kata ya Irisya, Jimbo la Singida Magharibi ambacho serikali ilitoa Sh. milioni 500.

Muro alisema haiwezekani serikali imetoa kiasi hicho cha fedha lakini ujenzi umekwama kwa miezi mitatu sasa huku fedha zilizotolewa zikiwa zimekwisha.

Aidha, Mkuu huyo wa wilaya alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, kupeleka timu kwenda kuchunguza mienendo na tabia za watumishi hao ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi.

"Ukiona kwa nje unaweza kufikiria kazi imeisha ila ukiingia ndani utabaini maabara haijakamilika, vyoo vyote vya majengo yote havijakamilika, 'tiles' za chini hazijakamilika, jengo la mochwari ndani halijakamilika, vyoo havijafungwa vyote na masinki ya kunawia mikono hayajakamilika huku baadhi ya majengo yakiwa tayari na nyufa kitu ambacho hakiweza kufumbiwa macho," alisema.

Muro pia alibaini madudu katika mradi huo ambapo wasimamizi wa mradi walimpa kazi fundi ya kutengeneza kipande cha ngazi za kupandia jengo la mama na mtoto na kisha kutoweka baada ya kusikia kuna ziara ya mkuu wa wilaya.

Akizungumza na wananchi na watendaji, Muro aliagiza kukamilika kwa vituo vyote vya afya ambavyo serikali ilishatoa fedha na kusisitiza wasimamizi wa Iyumbu, Ntuntu na Iglanson kuwa tayari.

"Wananchi hawataki kusikia malumbano yenu kwenye ujenzi. Wao wanataka kuona fedha zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan zinatumika ipasavyo na miradi inamalizika pasipo visingizio," alisema.

# Tathmini kufanywa uhaba madaktari

WIZARA ya Afya inatarajia kufanya tathmini kwenye hospitali za rufani za mikoa kutokana na kuwa na idadi kubwa ya madaktari bingwa kuliko maeneo ya pembezoni.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akitoa ufafanuzi wa maswali mbalimbali ya wabunge walihoji upungufu wa madaktari hao kwenye maeneo yao.

Ummy alisema Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, ameshatoa kibali kufanyika tathmini hiyo na kama itabainika wamezidi, wahamishwe na kupelekwa maeneo yenye shida wakati wakisubiriwa wanaosomeshwa.

"Ndani ya miaka miwili itakuwa historia kutokana na mpango wa Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Pia alisema serikali ina mpango maalum wa kusomesha madaktari bingwa na madaktari bingwa bobezi na kwa mwaka wa fedha 2022/23, watasomeshwa 139 na kati yao 136 watasomeshwa nje ya nchi.

"Wanasomeshwa kwa seti yaani daktari bingwa, mtaalamu wa usingizi na mtaalamu wa radiolojia. Tuna madaktari bingwa 457 wanasomeshwa kwa seti moja moja," alisema.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Tecla Ungele, alihoji serikali lini itaona umuhimu wa kupeleka madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani na mifupa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Lindi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hadi sasa hospitali hiyo ina madaktari bingwa watano ambao ni daktari bingwa wa upasuaji, afya ya uzazi na mtoto wawili, daktari bingwa wa mionzi, na daktari bingwa wa dawa za usingizi.

"Katika kuongeza idadi ya madaktari bingwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi, wizara imepeleka kusoma jumla ya madaktari saba ambapo madaktari wawili wanasomea udaktari bingwa wa watoto, ubingwa wa upasuaji wawili, daktari bingwa wa mionzi mmoja, daktari bingwa wa mifupa mmoja na daktari bingwa wa afya ya uzazi na watoto mmoja," alisema.

Hata hivyo, alisema kuhusu daktari bingwa wa magonjwa ya ndani, serikali inakamilisha taratibu za uhamisho ili kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Lindi.



Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Kenani, akiuliza swali baada ya Waziri Mkuu kuwasilisha taarifa ya tukio la moto uliotokea Mlima Kilimanjaro pamoja serikali kusitisha uwekaji wa hereni kwa wanyama wa kufugwa hadi Januari 2023 Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Minara 2,600 kujengwa kuboresha mawasiliano

BUNGE limeelezwa kuwa kwa sasa serikali iko kwenye mchakato wa kutafuta fedha za ujenzi wa zaidi ya minara 2,600 ili kutatua tatizo la mawasiliano kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akitoa ufafanuzi wa maswali ya mawasiliano yaliyotolewa na wabunge baada ya Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, kusema nchi imefikia hatua ya kupanua mawasiliano Congo wakati maeneo mengine bado hayana.

Nnauye alisema suala la mawasiliano sasa litafika mwisho kutokana na mradi huo na kuwaomba wabunge wavumilie kwa kuwa michakato inaendelea vizuri.

"Serikali imedhamiria kumuunganisha kila Mtanzania alipo. Mradi huu ukikamilika hili litakwisha lakini kuna mradi wa zaidi ya minara 100 imejengwa haijawashwa kwa kuwa wakati inajengwa kulitokea tatizo la corona, hivyo kusababisha vipuli vingine kutokuja na sasa vipo nchini na hivi karibuni itawashwa," alisema na kuongeza kuwa suala la mawasiliano kwa sasa ni sehemu ya haki za binadamu.

"Bunge lilipitisha bajeti hapa ya ujenzi wa minara 728 ambayo zabuni yake imetangazwa Oktoba 22, mwaka huu, na inafunguliwa Desemba 2. Najua watu walitamani baada ya bajeti ujenzi uanze lakini kuna mchakato wa kutangaza zabuni na kupata makandarasi," alisema.

Alisema majimbo mengi yatafikiwa na kutoa wito kwa wabunge kuangalia orodha ya kata itakayojengwa minara hiyo ili kubaini ambazo hazina na hazijaorodheshwa.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Ludewa (CCM), Joseph Kamonga, alihoji lini serikali itajenga minara ya simu katika kata za jimbo hilo pamoja na kuongeza nguvu kwa minara iliyopo iwe 4G.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Andrea Kundo, alisema lina kata 26 na kati ya hizo kata 19 zina minara ya mawasiliano.

Aidha, alisema serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imetekeleza miradi ya ujenzi wa minara ya simu Ludewa ambapo mpaka sasa imefikisha huduma za mawasiliano katika kata sita ambazo ni Kata ya Ibumi, Kilondo, Lumbila, Lupingu, Makonde na Madope.

"Kutokana na changamoto katika upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Kata ya Lupingu, Mfuko wa UCSAF umetoa ruzuku kwa Kampuni ya Tigo kwa ajili ya kujenga minara mingine miwili katika Kata za Lipingu na Lupanga ambapo ujenzi wa minara hiyo bado unaendelea na hivyo Kata ya Lipingu itapata huduma za mawasiliano kwa teknolojia ya 2G na 3G," alisema.

Kadhalika, alisema serikali kupitia mfuko huo imezijumuisha kata tatu ambazo ni Ibumi, Kilondo na Mtumbati katika zabuni ya mradi wa Tanzania ya kidigitali ambapo kata tajwa zitaboreshewa huduma za mawasiliano kwa teknolojia za 3G /4G.

"Kata sita ambazo ni Kata za Iwela, Ludende, Lugarawa, Manda, Mawengi na Milo zimejumuishwa katika zabuni ya ujenzi wa minara mipya iliyotangazwa tarehe 24 Oktoba 2022 kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali. Hivyo, kata hizo zitapata huduma za mawasiliano kwa teknolojia za 2G, 3G na 4G kupitia zabuni hiyo inayotekelezwa kwa fedha za Benki ya Dunia,"alisema.

## Walioshindwa masharti ya umiliki mashamba kukiona

SERIKALI inaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wamiliki walioshindwa kutekeleza masharti ya umiliki wa mashamba makubwa ya uwekezaji.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM), Noah Saputu.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani juu ya mashamba makubwa yanayomilikiwa na wawekezaji na hayatumiki kuzalisha mali na ajira nchini.

Kikwete alisema serikali inatambua kuwa yapo mashamba makubwa nchini ambayo yamegawiwa kwa wawekezaji ambapo baadhi ya mashamba hayo yanatumika kwa uzalishaji mali na ajira na mengine hayatumiki kama ilivyokusudiwa.

"Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine imeanza kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili wawekezaji kwa kufanya ukaguzi na kuainisha changamoto zilizoko.

"Hatua inayofuata ni kufanya majadiliano na wawekezaji waliobainika kuwa na changamoto ili kuzipatia ufumbuzi kwa pamoja kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji," alisema.

Alisema kwa mashamba ambayo yametelekezwa, wizara imeendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wamiliki walioshindwa kutekeleza masharti ya umiliki.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Kibamba (CCM), Issa Mtemvu, alisema matokeo ya mwanzo ya sensa ya yameonyesha ongezeko la watu milioni 16 kwa kipindi cha miaka 10 ambapo imeshabihiana na wananchi kuvamia mapori yasiyoendelezwa kwa muda mrefu.

"Serikali haioni kuna haja ya kutoa maeneo ambayo hayajaendelezwa ili wananchi waendeleze na kurasimishiwa,"alihoji.

Kikwete akijibu swali hilo, alisema wizara imepokea taarifa ya sensa na yako mambo ambayo serikali itafanya ili kuondokana na maeneo ambayo hayajapangwa vizuri na kurasimisha maeneo yaliyoiva kwa urasimishwaji.




**Habari zote: Augusta Njoji**

**DODOMA**



## Kiteto kutatua kero madawati

**Na Cynthia Mwilolezi,** KITETO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, imejipanga kufanya harambee ya kupata fedha za ununuzi wa madawati ili kukabiliana na upungufu wa samani hizo kwenye shule za msingi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, John Nchimbi, akizungumza jana, alisema harambee hiyo inatarajiwa kufanyika kesho kwenye uwanja wa mpira Kibaya.

Nchimbi alisema wananchi wa Kiteto wamejipanga kwa hali na mali kwenye harambee hiyo iliyowekwa kwa mpango mkakati wa kukabiliana na upungufu wa madawati katika shule za msingi. "Bei ya dawati moja ni Sh. 80,000 na mahitaji ya madawati kwenye shule za msingi Kiteto ni 21,069. Yaliyoko ni madawati 12,046 upungufu ni 9,023," alisema Nchimbi.

Mkurugenzi huyo aliwakaribisha wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya Kiteto kushiriki shughuli za maendeleo ya kuchangia madawati ya wanafunzi wa shule za msingi.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kiteto, Dennis Mwita, aliwataka wananchi na viongozi kujitoa kwa hali na mali ili kuondoa upungufu madawati na wanafunzi kusoma kwa kujinafasi.

"Jambo limeiva ni wajibu wa wananchi wakiongozwa na sisi viongozi wa kada mbalimbali kujitoa kwa hali na mali kuchangia madawati ya watoto wetu," alisema Mwita.

Mkazi wa Kijiji cha Partimbo, James Leyani, alisema wilaya hiyo ina utajiri mkubwa wa mifugo na mashamba hivyo anategemea watu watajitoa kwa wingi kuchangia madawati hayo.

# Wapewa wajibu utekelezaji wa ilani

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Kiria Laizer, ameagiza wakuu wa idara wa halmashauri hiyo kuwa na ilani ya chama hicho ili iwe rahisi kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

Laizer alisema hayo juzi wakati akitoa hotuba yake ya kwanza kwa watumishi wa serikali, wakiwamo maofisa tarafa, watendaji wa kata, vijiji na wenyeviti wa vijiji na vitongoji tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo.

Alisema ilani inayotekelezwa ni ya CCM, hivyo itapendeza kama kila mtaalam atakuwa na nakala kwa kuwa ni sawa na Mkristo au Mwislamu kutokuwa na Biblia au msahafu.

"Nitoe wito kwa kila mkuu wa idara ni vyema akawa na kitabu hiki mezani kwake akijikumbusha eneo lake anapaswa kufanyia kazi likoje," alisema.

Hata hivyo, alisema ametumia lugha rahisi na nyepesi kuwakumbusha ili watimize wajibu kwa kila mmoja wao, kwa kuwa wanapodai haki zao wakumbuke kutimiza na wajibu pia.

"Kasoro yoyote utakayoisababisha ujue unaijengea mazingira magumu CCM, jambo ambalo chini ya uongozi wangu hatutakubali alisema Kiria.

"Wananchi wetu hawana shida wanahitaji kuhudumiwa vizuri tena kwa wakati, tukasikilize na kutatua matatizo yao kwa kuwa wilaya yetu ni ya wafugaji, wakulima, wachimbaji na wafanyabiashara wakubwa na wadogo wote wanategemeana," alisema.

Kadhalika alisema katiba ya CCM imeweka wazi kila baada ya miezi sita serikali ngazi husika itawasilisha kwa chama tawala taarifa ya miradi iliyotekeleza hivyo wanatakiwa kujitathmini kama wanafanya hivyo.

"Nitumie nafasi hii kumpongeza Mkuu wetu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera na wasaidizi wake, kwa kuwa aliwasilisha utekelezaji wa ilani kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2021 kwa umahiri wa hali ya juu," alisema.

Laizer alisema utaratibu huo, usiishie wilayani humo, kwa kuwa umeelekezwa ufanyike ngazi ya matawi na kata na Mfuko wa Jimbo hilo nao unatakiwa utolewe taarifa yake na mbunge wa jimbo.

"Viongozi wa siasa na uchumi kwa karne ya sasa haviachani naelekeza ombeni viwanja, mashamba, mkaanzishe miradi ya kiuchumi na kuiboresha dhana kwa kila kiongozi wa chama aache alama katika kipindi cha uongozi wake," aliongeza Kiria.

Aidha, alisema amekutana na viongozi wenzake, ili kuweka mpango mkakati wa kwenda pamoja kwa kuwa watumishi hawatakiwi kuwa Mungu watu hasa wa serikalini hususani vijijini.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) Mkoa wa Tanga, Zainabu Bakari, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Tanga juzi, kuhusu kubaini udanganyifu uliofanywa na wahudumu wa afya Wilaya ya Muheza, kwa kufanya usajili hewa wa wagonjwa 313 wa VVU hivi karibuni kwa lengo la kuongeza takwimu ili kujipatia kipato kupitia posho. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Hatima ya mgogoro Bondo kujulikana leo

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

HATIMA ya uhalali wa wananchi wanaoishi katika msitu wa Bondo ulioko mtaa wa Kwaluala wilayani Handeni Tanga utajulikana leo baada ya mgogoro wa kugombania mpaka kati ya wilaya za Handeni na Kilindi kufukuta kwa muda mrefu.

Hayo yalijiri jana baada ya wananchi hao kutoa malalamiko kwa Mkuu wa Mkoa huo, Omary Mgumba, wakidai kuwa wameishi kwenye eneo hilo kwa zaidi ya miaka 70 kwa kuwa wengi wao waliuziwa maeneo hayo na Mwenyekiti wa Kijiji na wengine waliotoka mikoa ya jirani waliuziwa na wenyeji wao.

"Tumekaa hapa kwa muda mrefu, mimi ni mwenyeji wa Karatu, Arusha mkoani Arusha, nilikuja hapa nikiwa na watoto wangu watatu mpaka sasa nina wajukuu. Tunaomba serikali ituangalie kwa huruma hasa kuna kinamama na watoto wengi ni kama tutaanza kusumbuliwa na hatumjui kama ni kuhama na tutapelekwa wapi," alisema Isabela Khaay.

"Karibu asilimia 90 ya wananchi tunaoishi Bondo tuko katika eneo hili linalosemekana ni msitu. Kwa hiyo tunaomba serikali iangalie kwa kina jambo hili ili siku ya kutoa uamuzi ituhurumie tuendelee kuishi kwa kuwa sisi si wavamizi," alisema Daniel Sulle mwananchi wa Bondo. Kuhusu mgogoro wa mpaka wananchi walioko Wilaya ya Kilindi, waliomba kupata huduma za kijamii kwa kuwa wako mbali na sehemu za kutolea huduma hizo.

"Tunaomba ikupendeza Bondo yote ihamie Wilaya ya Handeni kwa sababu Songe ni mbali. Hata huduma za kiserikali tunazipata kwa shida sana na endapo ikihamia huku tutapata urahisi wa huduma," alisema Sulle.


Akitoa ufafanuzi wa mgogoro huo, Mgumba alisema mgogoro wa mpaka haugusi wananchi kwa kuwa ardhi inalindwa kisheria na serikali, hivyo uamuzi utategemea itakavyoamuliwa, lakini suala la mpaka haimaanishi kwamba kuwahamisha watu mahali aliko.

"Hapa Bondo kuna kero ya kwanza mgogoro wa mpaka kati ya Kilindi na Handeni na mwingine ni ule wa hifadhi, napenda kuwaeleza kuwa mgogoro wa kiutawala nyie wananchi hauwahusu na asitokee kiongozi yeyote akawagombanisha kisa mipaka hii.

"Sioni kitu gani kinachelewesha kutatua migogoro yenu, kwa kuwa kamati za ulinzi na usalama, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi CCM pamoja na wataalamu wilaya zote mbili, tunatakiwa tukutane ofisi kwangu, tumalize tatizo hili na tukishapitia taarifa za wataalamu tutakuja kuwaletea majibu mpaka uko wapi, alisema."

Mkuu huyo wa Mkoa alisema wakazi wanaoishi eneo hilo sio wenyeji wa asili bali wamehamia kutoka mikoa mingine, lakini kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine hakina shida kwa kuwa ni Mtanzania.

"Si dhambi kwa Mtanzania kuishi mahali popote ili mradi asivunje sheria. Pia kwa mujibu wa mwenyekiti wa mtaa, sheria hazijafuatwa ndiyo maana nimeomba muwe wavumilivu kwa kuwa uamuzi utakwenda kutolewa," aliongeza.





## TAKUKURU yajipanga usimamizi fedha miradi

**Na Oscar Assenga,** TANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tanga imeanza mikakati ya kuhakikisha fedha zilizopelekwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, zinafuatiliwa kwa ukaribu ili kuhakikisha taratibu zinafuatwa na ujenzi unafanikiwa kwa wakati.

Kutokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu na kuleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, tayari kwa mkoa wa Tanga imeelekezwa utapokea zaidi ya bilioni 4.9.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga, Zainabu Bakari, alisema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya kipindi cha Julai hadi Septemba, 2022 na kuelezea mikakati ya kipindi cha Oktoba – Desemba, 2022.

Alisema wanafanya hivyo ili kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwenye matumizi yaliyokusudiwa yanafanyika ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kusoma bila vikwazo.

Katika hatua nyingine, taasisi hiyo kwenye jukumu lao la kuchunguza tuhuma au makosa ya rushwa ambapo kwa mkoa huo, wamepokea taarifa 107 na kati ya hizo 61 ni za vitendo vya rushwa na taarifa 46 si taarifa za vitendo vya rushwa.

Alisema katika taarifa 61 zilizohusu rushwa zilifunguliwa majalada ya uchunguzi ambapo 43 zinaendelea kuchunguzwa na taarifa 18 zimefungwa katika hatua za awali za uchunguzi kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa kuthibitisha tuhuma.

Hata hivyo, alisema pia kati ya taarifa 46 ambazo hazikuhusu vitendo vya rushwa, taarifa 35 wateja walishauriwa namna mbadala za kutatua kero zao na nyingine 9 zimehamishwa idara nyingine kwa hatua zaidi.

Alitoa mchanganuo wa taarifa hizo za malalamiko kisekta, alisema Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) utawala ni 22, elimu 12, afya 9 na uvuvi moja.

Zingine ni ardhi 15, mahakama saba, ujenzi nne, vyama vya siasa nne, sekta binafsi nane, wakala wa serikali tatu, mabaraza ya kata tatu, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii mbili, ushirika na SACCOS nne, TASAF mbili, Fedha mbili, Takwimu tatu, mashirika ya umma moja, NGO moja na bima mbili.

Katika kipindi husika TAKUKURU mkoa huo imefungua shauri moja na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea mahakamani mpaka sasa kufikia 32 lakini katika kipindi hicho Jamhuri ilishinda kesi moja mahakamani.

# Mgogoro sugu wa ardhi KIA, wananchi kupatiwa suluhisho

**Na Mary Mosha,** HAI

MGOGORO wa ardhi kati ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) wilayani Hai, umeanza kupatiwa suluhisho.

Hatua hiyo inatokana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, kutangaza kuwa kuanzia Novemba 9, mwaka huu, tathmini ya madai ya wananchi hao itaanza kufanyika rasmi.

Babu alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye kikao malumu kilichofanyika katika Kata ya Kia, wilayani hapo ambacho kilihudhuriwa na wataalamu wa ardhi na viongozi wa wilaya hiyo.

Kiongozi huyo alisema lengo kuchukua hatua hiyo ni jitihada za serikali za kuhakikisha inatatua mgogoro huo uliodumu kwa zaidi ya miaka 20.

Alisema eneo hilo lilitengwa kimkakati kwa kuwa lina hati ya miaka 99 kwa ajili ya kupanua na kuendeleza uwanja wa ndege ili kuwa katika mfumo wa kuvutia utalii.

"Kwanza naomba acheni maneno ya upotoshaji uwanja wa ndege ni mali ya serikali na Kilimanjaro Airports Development Company (KADCO ) kwa kuwa wasimamizi wa uwanja huo ni watumishi ambao wameajiriwa na serikali. Naomba mwondoe dhana kuwa ni wa mtu binafsi. Rasilimali zinazopatikana hapa ni kwa ajili ya manufaa ya taifa," alisema Babu.

Alisema shughuli hiyo itasaidia kutambua idadi ya wananchi waliojenga makazi na kuendeleza shughuli mbalimbali ndani ya eneo la uwanja na serikali itawalipa fidia ili kuhama kupisha maeneo hayo.

Mkuu wa Mkoa alisema lengo la serikali si kuwahamisha wananchi wote wa kata ya hiyo, bali ni kwa wale watakaokuwa ndani ya eneo la uwanja lenye hati miliki. "Wako baadhi ya watu kwa kujua au kutokujua wameingia katika eneo la uwanja wa ndege. Kazi ya upimaji wa eneo la uwanja itaanza Novemba 9, mwaka huu, kwa ushirikiano kati ya timu ya wataalamu, viongozi wa vijiji, vitongoji na diwani husika. Naomba wananchi mtoe ushirikiano ili kazi hii ifanyike na watu waishi kwa amani," alisema Babu.

Aidha, Babu alisema Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda wananchi wake wote, ndiyo sababu amechukua jukumu la kuagiza walipwe fidia kupisha eneo la uwanja.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, alisema imefika hatua kwa mgogoro huo kutatuliwa na kufikia mwisho ili wananchi waendelee na shughuli za maendeleo.

Boisafi alisema mgogoro huo, ni wa muda mrefu sasa, hivyo ifike mahali wananchi wakubali kuwaachia wahusika wafanye shughuli yao na kutoa majibu ili haki iweze kupatikana.

"Tunapaswa kuunga mkono maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia kupitia serikali lakini kama mtaleta ubishi mtasababisha serikali ifanye uamuzi mwingine ambao utasababisha kufikia sehemu ambayo hatupendi kufika huko," alisema Boisafi.

Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro, Willy Machumu, alisema eneo hilo lilitengwa mwaka 1969 kama la kimkakati kwa ajili ya shughuli za uendelezaji wa uwanja.

Machumu alisema taarifa zinazoenezwa kuwa KADCO si mali ya serikali ni uongo na kuwataka wananchi kutambua kuwa wasimamizi wa uwanja ni shirika linalomilikiwa na serikali kwa asilimia mia moja.



Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe (kushoto), akizungumza katika mkutano wa hadhara eneo la Bondo, Mtaa wa Kwaluala, Kata ya Kwamagome, wakati Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba (wa tatu kulia), alipokwenda kusikiliza kero za wananchi kuhusu Hifadhi ya Msitu wa Bondo, ambayo maamuzi ya kuwa hifadhi au makazi yatatolewa leo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wadau wa elimu wasisitizwa ubora masomo sayansi kuzalisha wataalam

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

WADAU wa elimu mkoani Kilimanjaro, wameishauri serikali kuboresha mazingira ya elimu katika shule za mchepuo wa sayansi ili kuzalisha wataalamu wengi wa masomo hayo.

Ushauri huo ulitolewa na Meneja wa Shule ya Mchepuo wa Sayansi ya Mtakatifu Joachim iliyoko wilayani Same, Deogratias Mchagi, wakati wa mahafali ya saba ya shule hiyo.

Alisema uwazi na upendo kwa wanafunzi wa sekondari ni moja ya njia thabiti katika kuhakikisha wanafanya vizuri katika masomo yao na mtihani wa kuhitimu kidato cha nne

Hata hivyo, alisema shule hiyo imekuwa ikisimamia maadili, uadilifu na nidhamu hali ambayo imesababisha wanafunzi kuendelea kufanya vizuri katika mitihani ya kidato cha nne.

Alisema siri ya shule hiyo kufanya vizuri kila mwaka ni nidhamu kwa wafanyakazi, upendo na uwazi kwa wanafunzi.


Meneja huyo alisema uaminifu na nidhamu kwa wanafunzi wa shule hiyo,ndio siri iliyosababisha kufanya vizuri kila mwaka tangu kuanzishwa kwake miaka 10 hadi sasa.

Akizungumza kwa niaba ya wazazi waliohudhuria mahafali hayo, mzazi wa mwanafunzi Anjela Kessy, alisema watoto wanaotoka katika shule hiyo mara nyingi wanaendelea kuwa na nidhamu, uaminifu na maadili waliyojifunza shuleni na wanakuwa mfano bora katika jamii.

"Sasa hivi huko mtaani kuna kikundi kinachoitwa 'panya road'. Tunatarajia nyie ndio mkawe walimu wazuri wa kukomesha wimbi hilo," alisema.

Mmoja wa wanafunzi waliohitimu katika shule hiyo, Godfrey Kipande, alisema shule hiyo inakabiliwa na ukosefu wa bwalo na jiko la kisasa.

Pia alisema wanakabiliwa na tatizo la mabadiliko ya tabianchi, wanafunzi waliotesha miti 1,000 ili kukabiliana na ukame ulioko wilayani humo.




Ukurasa 17

Wanahabari tuache uchawa wetu kwa wanasiasa

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 4, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**DK. TUMAINI GURUMO WA DMI**
**Mwanamama aliyebobea katika taaluma ya bahari, akianika namna kufikia uchumi buluu**

Ukurasa 16

# Ushuhuda kazi za binadamu zinavyoua utalii, kutoweka wanyama sita duniani

**Na Mwandishi Wetu**

KULINGANA na Hazina ya Wanyamapori wa Asili Duniani (WF), shirika lisilo la kiserikali linalofanya kazi kulinda wanyamapori, takriban spishi 10,000 hutoweka milele kila mwaka.

WWF linasema idadi halisi haijulikani kwa sababu bado hatujui ni spishi ngapi zinapatikana kote duniani.

Kwa kuwa dunia huadhimisha Siku ya Viumbe Vilivyo Hatarini kila Novemba 30, baadhi ya wanyama waliokuwa wengi katika sayari hii na sasa hawapo tena.

Wafuatao ni wanyama wanane ambao wameangamia kutokana na shughuli za binadamu katika makazi yao asilia:

1: Miss Waldron's Red Colobus anayepatikana Ghana na Ivory Coast, huku Zanzibar Red Colobus ndiye jamaa wa karibu zaidi wa Miss Waldron red colobus aliye hatarini kutoweka



Aina ya tumbili wanaotoweka duniani. **PICHA: MTANDAO.**

Zanzibar Red Colobus ndiye jamaa wa karibu zaidi wa Miss Waldron red colobus aliye hatarini kutoweka. Ni Tumbili mwenye ukubwa wa kadri na mwenye nywele nyekundu, anasadikiwa kutoweka tangu mwanzoni mwaka miaka ya 2000.

Miss Waldron's Red Colobus, anayeishi kwenye mpaka wa Ghana na Ivory Coast, alikuwa mmoja wa wanyama wa ajabu kwa sababu hakuwa na vidole gumba.

Mnyama huyo anaishi na wenzake kwenye makundi makubwa juu ya miti na ni mpole na akalazimika kubadili mtindo wake wa maisha kutokana na ukataji miti unaofanywa na wanadamu.

Misitu ilipoanza kupungua, idadi ya tumbili hao pia ilipungua, na kuwafanya kuwa hatarini kuliwa na wanyama wenzao.

2: Pomboo ya Mto Yangtze (China); Pomboo wa Mto Yangtze wa China, anayeitwa Baiji, alifikiriwa kuwa mmoja wa mamalia wa zamani zaidi ulimwenguni.

Anadhaniwa kuwa mmoja wa mnyama wa zamani zaidi ulimwenguni.

Pomboo wa Mto Yangtze aliyetangazwa kutoweka mwaka wa 2006,alikuwa rangi ya kijivu asiye na nguvu ambaye alionekana kuwa na udhaifu kuliko wanyama wenzake wanaoogelea baharini.

Chini ya mwili wake laini alikuwa na mfumo wa hisia wakusaidia kuna vitu ambao ulikuwa bora zaidi kuliko ule wa pomboo wengine.

Mfumo wake uliweza kufanya kazi vizuri sana hivi kwamba ungeweza kupata eneo la samaki hata mmoja.

Lakini pomboo hao wakakabiliwa na tishio la kuangamia wakati mto boti za uvuvi zilipofurika katika mto huo, meli za kontena, meli na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na mwanadamu.

Kutokana na msongamano huo mkubwa wa vyombo majini, hawakuwa na na uwezo wa kuendelea kuishi.

3: Caribbean Monk Seal (Serranilla kati ya Jamaika na Nikaraguall; Mnyama huyo wa asili wa mto wa eneo la Caribean, alipatikana kwenye pwani ya mashariki ya Amerika ya Kati, pwani ya kaskazini ya Amerika Kusini, na Ghuba ya Mexico.

Walisakwa kwa ajili ya mafuta yaliyopatikana katika miili yao, ilhali uvuvi wa samaki wao wa chakula kupita kiasi ulisababisha uhaba wa chakula kwa ndama wa mto waliosalia.

Walionekana kwa mara ya mwisho mnamo 1952 karibu na pwani ya Serranilla kati ya Jamaika na Nikaragua.

4: Alabama Pigtoe (Marekani); Oyster hizi za mto zinapatikana katika Jamhuri ya Czech. Konokono huyu wa kipekee alipatikana katika mto wa Alabama nchini Marekani hadi mwaka wa 2006.

Alipewa jina hili kwa sababu alikuwa na muonekano kama wa mguu wa nguruwe, lakini ilikuwa ikichuja maji ya mto yaliyochafuliwa. Lakini uchafuzi wa mto ulikuwa mwingi kiasi kwamba Pigto hakuweza kustahimili tena.

Kuangamizwa kwa kiumbe huyo mdogo kulifichua mambo mengi ya kutisha kuhusu maji hayo, ambayo yalikuwa yakichafuliwa na sumu kutoka viwandani na kusababisha magonjwa hatari katika jamii ya Waamerika wenye asili ya Afrika wanaoishi kando ya mto huo.

5: Dodo (Mauritius); ndege maarufu, lakini anayetoweka kunaweza kuwa heshima isiyo ya kawaida, lakini mbali na dinosauri, dodo ni spishi iliyotoweka kwa muda mrefu ambayo kila mtu anawafahamu.

Ndege huyo anayefanana na mhusika wa katuni Daffy Duck, aliachiliwa mara moja kwenye kisiwa cha Mauritius. Hakukuwa na wanyama waliowawinda asili ya ndege hii isiyoweza kuruka. Watu walipofika Mauritius, walikuja na wanyama wengine waliokuwa na hamu ya nyama. Dodo hakuweza kuishi mbele yao kwa muda mrefu. Dodo wa mwisho alikufa mwanzoni mwa karne ya 18.

6: Ng'ombe wa Bahari (Steller); Ng'ombe hawa wa baharini waliokuwa wanafanana na manatee na dugongs, lakini walikuwa wakubwa zaidi kuliko viumbe hivyo. Ng'ombe wa baharini wa Steller wanaweza kukua hadi mita tisa kwa ukubwa.

Ni shabaha ya wawindaji kwa sababu ya sura yake ya kupendeza, manyoya na mafuta yake yenye thamani. Inaaminika kuwa walikufa muda mfupi baada ya kutoweka kwa dodo kutokana na uwindaji na mabadiliko ya mazingira ya chakula chao.

• ***Kwa mujibu wa BBC.***

UCHUMI

## WAJUE TAHA WA SHAMBANI ...

# Wataalamu kilimo wanaomfungulia mama 'kutoka' umwagiliaji wa mboga bustanini

**NA WOINDE SHIZZA, ARUSHA**

KUNA wakati zaidi ya muongo mmoja, zilitolewa takwimu za ushiriki wa wanawake kwenye kilimo nchini, kukitajwa asilimia ni 54. Pia, asilimia 81 yao jinsia hiyo, inatajwa kuhusika na shughuli zenye unasaba na kilimo. Lakini, je wananufaikaje?

Eneo la kilimo cha mboga na matunda, sasa Iinatajwa ni kipaumbele, huku kinakuwa kwa kasi nchini kufikia asilimia nane, hadi kufika mwaka jana. Pia, ni eneo lililoko juu katika kuiingizia mapato serikali katika sekta ya kilimo.

Leo, kijana Irene Mollel, ni mnufaika, ambaye ameweza kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo cha maua, mboga, matunda na mimea itokanayo na mizizi na viungo .

Anasimulia kilichomvutia ni pale alipotembelea moja ya maonyesho ya kilimo - Nanenane mkoani Arusha, ikampa funzo na sasa amekuwa mkulima mzuri na mkubwa wa nyanya.

Irene anaeleza kwamba, alikiangalia kilimo cha nyanya, vitunguu na vingine katika maonyesho hayo ya Nanenane na akavutiwa zaidi alipotembelea banda lenye maonyesho ya mazao kama maua, mboga, matunda, mimea itokanayo na mizizi na viungo.

Anasimulia kwamba kihistoria, kabla ya kufika katika maonyesho hayo, alishajaribu kilimo hicho, lakini hakufanikiwa hata akakata tamaa, akaamua kufuatilia madarasa kupitia mitandao ya jamii, hasa kwenye ukurasa wa mtandao uliohusu asasi ya TAHA, akiona fursa ya vijana kusaidiwa, akajiunga na kuanza kilimo rasmi.

**KIJANA WA MBOGA**

Mwanamama Irene Mollel, anasema akaanza kupata mafunzo kutoka kwa Bwana Shamba, akipata darasa analolitaja la 'kilimo cha matone.'

Pia, anasema akaandaliwa ratiba nzuri ya kuweka mbolea ya kisasa aina tofauti katika nyanya zake shambani, huku akitembelewa na kushauriwa na mwalimu wake ambaye ni Bwana Shamba, kuhusu namna ya kusafisha shamba kila mara.

Hapo Irene anakiri ushauri huo umemsaidia kupita hatua ya kuzalisha mazao mengi na yenye ubora.

Mama huyo kijana anaenda mbali kwamba, upande wa masoko amenufaika, kwa sababu amepata mwongozo kwa kulima bidhaa inayonunulika kwa bei bora, inayomuwezesha mkulima, wateja kuwauata shambani na kunjunuia bidhaa kwa bei nzuri kwake na wakulima wenzake.

"Kipindi kilichopita nilipoanza, nililima ekari moja, lakini sikupata kitu, maana sikuwa na elimu. Lakini, kipindi kilichofuata nimelima ekari hiyo hiyo moja, na nimepata mazao mengi ambayo yamenisaidia kuongeza mtaji wangu wa kilimo" anaeleza.

Irene anasema kipato anachokipata kila msimu kikemuinua na kumhamasisha hata akaongeza ekari zingine mbili, pia idadi ya wafanyakazi wa kumsaidia, akilenga kuwa mfanyabashara mkubwa.

Irene anawataka wanawake wanaolima, waachane na mtindo wa mazoea, hasa kuegemea katika mvua na badala yake waingie katika kilimo cha kisasa cha umwagiliaji, sambamba na mbinu za kisasa.

**WA NANASI**

Mkulima mwingine wa zao la nanasi, anayejitambulisha kwa jina Eva John (24), kutoka Kiwangwa Bagamoyo, mkoani Pwani, naye anasimulia mwanzo wake kama huo.

Eva anaeleza awali alishindwa kuendelea na masomo baada ya kumaliza kidato cha nne kutokana na kipato kidogo, lakini hakukata tamaa, akaamua kujiingiza katika kilimo cha nanasi .

Anasema baada ya hapo ndipo mwaka 2018 akafikia uamuzi wa kujiunga na kilimo katika shamba la ekari moja, akiwa na ujuzi mdogo wa uzalishaji wake, pia hata kusaka masoko, hata akajikuta mazao yake yanaharibika shambani, hata akakatya tamaa.

Kijana huyo anasimulia, mara baada ya kukutana na wataaalamu wa kilimo hicho waliompa elimu, hata akaanza kuona faida za kilimo hicho na sasa ana shamba la jumla ya ekari sita

Anasimulia katika kijimarisja zaidi, akajiunga na huduma za asasi Tanzania Horticultural Association (TAHA), mwanzoni mwa mwaka 2020 inayojishughulisha na kukuza kilimo cha Horticulture nchini kinacho husisha maua ,mboga, matunda, viungo na mimea.

Kwa mujibu wa Eva, amekuwa akipokea ushauri wa kitaalamu kuhusu mbinu bora za kilimo, upatikanaji masoko na usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao anayolima, huku ikidhibiti upotevu wa mazao.

Sasa anatajka kupata masoko ya mazao yake katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro na awali alikuwa akiuza nchini, Kenya kabla ya kuibua karatni ya maradhi Uviko - 19.

"Sasa hivi natarajia kuvuna ekari tano za nanasi, natarajia faida ya zaidi ya shilingi milioni 10 za Kitanzania. Pia, kupitia kilimo hiki hiki cha 'horticulture' nimeweza kuipatia familia yangu mahitaji ya msingi kama kujenga nyumba yangu , pia kuwajengea wazazi wangu.

"Nimejenga fremu za maduka ya kukodisha na naninasaidia wanafunzi 13 kwenye eneo ninaloishi mahitaji ya shule, ili waweze kutimiza ndoto zao na wasiishie njiani kama mimi," anaelezea Eva

Rai yake Eva, anawasihi wanawake kutokata tamaa hata kama wameangika kimasomo, wana fursa ya kujiwekezea katika kilimo cha uwagiliaji akitamba' kinalipa.'



Kinamama katika kilimo cha umwagiliaji wanaoungwa mkono na TAHA. **PICHA: MTANDAO.**

**MTAALAMU TAHA**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ssasi kilele ya TAHA, Dk.Jacqueline Mkindi, anawataka wanawake kuwa mstari wa mbele kuchangamkia fursa zinazotokana na kujihusisha na uzalishaji na mnyororo mzima wa mazao ya hayo wanayoyasimamia.

Anasema kilimo hicho kina fursa nyingi, lakini wanawake wengi wamekuwa wakiachwa nyuma, akiwahakikshia kuwa masoko yapo, ila tatizo kubwa ni uchache wao kinamama washiriki katika mnyororo mzima wa kuzalisha mazao hayo.

"Wanawake wengi wamekuwa wanalalamika ajira hazipatikani, wakati yapo maeneo mengi ya uwekezaji ambayo yanaweza kumkomboa mwanamke kiuchumi na niseme fursa ni nyingi sana za mazao," anasema Dk. Mkindi.

Anaeleza mbinu mojawapo ni wanawake wanaweza kujiunga katika vikundi na kukodi mashamba na wakazalishaji mazao kama nyanya, vitunguu na viazi, yote yakiwa ni mazao ya muda mfupi na yako chini ya miongozo ya wataalamu wa TAHA, hata wakapata mavuno, pia masoko ya uhakika.

Kiongozi na mtalamau huyo wa TAHA, anafafanua kwamba, kinamama hao wanam fursa nyinginezo za kuuza mazao hayo, pia fursa ya kuyaongezea thamani mazao kama vile ndizi na viazi kwa kusindika; pia uuzaji wa miche ya mbegu; na kutengeneza bustani za maua.

Akirejea juhudi za TAHA kumkwamua mwanamke, Dk. Mkindi anaesema wanatoa elimu ya kilimo cha kisasa, elimu ya ujasiriamali kwa wanawake, kuwaunganisha na huduma za mitani na masoko, mengki yakifikishwa Afrika Mashariki na kusini mwa Afrika.

Eneo lingine la utaalamu analolitaja ni kwenye lishe na afya bora, akisema ni zaidi ya asilimia 40 ya wanufaika wa TAHA wameweza kupata elimu hizo.

BIASHARA

# Mabadiliko tabianchi yanavyoathiri uchumi wavuvi wanawake ufukweni

**Na Jenifer Gilla**

SAA sita na robo mchana, Mwajabu Mohamed (54), mkazi wa Buyuni katika Manispaa ya Kigamboni, Dar es Salaam, amekaa nje ya nyumba yake, akimsubiri mume wake aliyeenda kuvua samaki, arudi wapate mboga na hela kwa ajili ya chakula cha mchana.

Jambo linalomsikitisha Mwajabu ni kuwa miaka mitatu iliyopita muda kama huo asingekuwa hapo, pamoja na kinamama wenzake. Daima angekuwa baharini akivua samaki kwa ajili ya kuuza na chakula, hivyo kumsaidia na mumewe majukumu ya nyumbani.

"Uvuvi kwetu kinamama umekuwa mgumu sasa hivi, kwa sababu tunatega nyavu kwenye maji mafupi ambako samaki wamehama, kwa sababu jua limekuwa kali na kusababisha maji kuwa ya moto na hakuna matumbawe ya kujificha," anasema Mwajabu.

Shughuli za uvuvi kwa wanawake katika mwalo wa Buyuni, Dar es Salaam, imekuwa ikizorota kadri siku zinavyosogea, kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuharibiwa makazi ya samaki hao, kwa shughuli za uvuvi haramu.

Utafiti uliofanywa na mwansayansi bahari, Frocklin na wenzake mwaka 2013, unaonyesha kuwa hakuna usawa katika upatikanaji wa rasilimali, mitaji, mawasiliano na masoko ya samaki kati ya wavuvi wanawake na wanaume, hali inayowarudisha nyuma wanawake katika shughuli hiyo.

Taarifa hiyo inaongeza kuwa tofauti na wanaume, wanawake hawapo katika kamati za usimamizi wa uvuvi wa kijiji au vikundi vya wafanyabiashara rasmi wa samaki hali inayochangia sauti zao kutosikika duniani.

**WANAVYOELEMEWA**

Kumrejea mume wa Mwajabu, Mahesabu Mohamedi, anasema tangu mke wake aachane na shughuli hiyo, amekuwa akielemewa na mzigo wa majukumu, kwa sababu hata upande wake, biashara hiyo haijakaa vizuri kutokana na kuadimika samaki hao.

"Zamani ilikuwa tukizamia mita 24 chini, tunapata samaki ambao tunawauza Sh.300, 000. Hivyo, kila mmoja anapata mgawo wa Sh.80,000, lakini sasa upatikanaji samaki umekuwa mgumu, tunazamia mita 32 na bado tunapata samaki wa kuuza Sh.100,000 tu, hivyo tunagawana Sh. 25000 kila mmoja," anasema.

Fatuma Mwalimu, kwake pamoja na changamoto zilizopo, bado anaendelea na shughuli hiyo, kwa kuwa ndio yenye uhakika wa kumpatia fedha kidogo kwa ajili ya kuhudumia familia yake.

Mama huyo wa watoto wanne, anasema anashirikiana na wenzake watatu kuvua samaki ambapo wanapata samaki wa kuuza Sh.20, 000 kugawana Sh.5000 kila mmoja.

"Japokuwa kipato ni kidogo, lakini sio sawa na kukaa tu nyumbani, hasa kwa mimi ambaye nina watoto wananitegemea, nikipata hiyo 5000 kwa siku inanisaidia kununua chakula cha watoto," anasema.



Wavuvi kinamama wa Buyuni, Dar es Salaam wakiwa kazini.

**SAMAKI KUTOWEKA**

Uchunguzi uliofanywa na wanasayansi ya bahari nchini Uingereza (New Scientists), mwaka juzi, unaonyesha halijoto duniani itaendelea kuongezeka kwa nyuzi joto tano na asilimia 60 ya aina mbalimbali za samaki zitatoweka.

Sababu kuu inaelezwa ni mahitaji makubwa ya hewa oksijeni inayoyeyuka zaidi katika maji baridi na kidogo katika maji yenye joto, hali inayoathiri uzalishaji.

Ukosefu wa samaki si changamoto pekee wanayokumbana nayo wanawake wavuvi 15 katika mwalo huo. Amles Selemani, anasema amekuwa akin'gatwa na samaki wenye sumu, wakiwamo manyangale, chofu na nyenga katika shughuli hiyo, hali iliyompa ulemavu wa mguu mpaka leo.


"Samaki hao wanatung'ata mikononi tunavyowashika na miguuni kwa sababu hatuna vifaa vya kujikinga. Alining'ata samaki anaitwa nyenga, nilikaa nyumbani wiki mbili nauguza mguu, kwa sababu ulivimba na kuweka usaha, mpaka sasa huu mguu ikifika kipindi cha baridi unauma hivyo nasimamisha shughuli za uvuvi hadi utakapoacha," anasema.

**KATIBU WAVUVI**

Katibu wa Wavuvi Mwalo wa Buyuni (BMU), Mussa Kayanda, anataja shida nyingine wanayopitia kinamama, ni kukosa nyavu zenye viwango kwa ajili ya uvuvi, hata kuwafanya kupata samaki wachache.

"Kwa wale wanaookota samaki baharini, pia hawana zile miwani maalum za kuangalia ndani ya maji na hiyo husababisha kung'atwa kwa sababu kwa kutumia macho, huwezi kuona vizuri samaki kwa hiyo tahadhari inakuwa ndogo," anasema.

Kayanda anasema, kwa kushirikiana na viongozi wenzake, sasa wanaendelea kutafuta misaada kuwasaidia wanawake hao na hivi karibuni walifanikiwa kupata mabuti ambayo sasa kinamama hao wanayatumia, kutoka taasisi ya wanasayansi wa viumbe bahari - Aquafarm (AFO).




Takwimu zinazoonyesha kiwango cha uvuvi na tija yake. **PICHA ZOTE: JENIFER GILLA.**

**NINI KIFANYIKE?**

Mkurugenzi wa AFO, Jerry Mang'ena, anasema jitihada za lazima zinahitajika kuandaa mazingira bora kwa viumbe bahari kuzaliana na kuwanufaisha wavuvi, hasa wanawake wanaovua kwenye maji kina kifupi.

"Huko Buyuni kunahitajika kuwekwa matumbawe ya kutengeneza kwenye maeneo ambayo yameharibiwa na shughuli za binadamu, ili kuwavutia tena samaki kurudi na kinamama wataweza kuvua tena," anasema.

Vilevile anasema, ni muhimu kuwaelimisha wananchi utunzaji mimea baharini, ambayo sasa inaelekea kutoweka, ikiwamo matumbawe na mikoko inayosaidia kuleta kivuli na makazi ya samaki.

"Hapo Buyuni wanakata sana mikoko, wanatengeneza mkaa kwa ajili ya kuuza, jambo linalohatarisha usalama wa eneo lao. Pia, kwa sababu mikoko inasaidia kuzuia mafuriko pale bahari inapojaa, wakiendelea hivyo makazi yao yanaweza kuvamiwa na maji," anasema.

Mang'ena ana maoni kwamba, wametoa vifaa vya kujikinga na madhara yatokanayo na uvuvi, ikiwamo mabuti kwa kinamama wanaochokoa samaki aina ya pweza pamoja na mafunzo ya ujasiriamali.

**MANISPAA YAZUNGUMZA**

Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa ya Kigamboni, Joshua Bullu, anaeleza kuwa manispaa inatoa mikopo kwa wanawake wavuvi, kwa ajili ya kununua vifaa vya vya uvuvi, ikiwamo mabuti, miwani, neti na boti za kukodisha ziwaingizie kipato.

"Wanachotakiwa kufanya ni kuunda makundi, kuyasajili na kuja kuomba mikopo," anasema Bullu na anaendelea: "Kuna vikundi vya vijana na wanawake wavuvi watatu katika manispaa hii, ambavyo tumeshawapa mikopo ya dhana, ikiwamo boti na neti na kisasa za kuvulia, ili kuwaongezea ufanisi katika shughuli zao, ikiwamo Buyuni na bado tunaendelea."

Fatuma Mwalimu, Mwenyekiti wa Kikundi cha Wanawake cha Buyuni Yetu, anasema baada ya kuona shughuli za uvuvi zinayumba, waliunda kikundi chao kinamama chenye wanachama 15, wakapatiwa mafunzo ya kutengeneza kofia za ukindu viatu na urembo unaotokana na mabaki ya samaki.

***" Tangu tumepatiwa mafunzo hayo ni miezi sita sasa na tumeshaanza kutengeneza bidhaa zetu, sasa kazi kubwa ni kutafuta masoko, tunashukuru sasa tunaona mwanga ingawa hatujaanza kupata faida, lakini tunajua mambo yatakuwa mazuri" anaeleza Fatuma.***

UCHUMI

## DK. TUMAINI GURUMO WA DMI

# Mwanamama aliyebobea katika taaluma ya bahari, akianika namna kufikia uchumi buluu

• Amkuna Balozi wa India, akaribisha Watanzania wakasome

**Na Romana Mallya**

"MABAHARIA siku zote wamekuwa kitovu cha biashara duniani na kazi yao inagusa maisha ya kila mtu, iwe ni chakula kinawekwa mezani kwetu, dawa zinazodumisha afya ya kila mtu, kompyuta zinazotumika kwa kazi au kujiburudisha au magari yanayotusafirisha kila siku," anatamka Katibu Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Masuala ya Bahari (IMO), Kitack Lim.

Hiyo ilikuwa Juni 25 mwaka jana, katika Siku ya Mabaharia Duniani, huku akikumbusha kuwa vitu vyote hivyo husafirishwa na meli kupitia baharini.

Wakati Kim anakumbusha hilo, Tanzania haiko nyuma sasa, inaendelea kuwekeza kwenye rasilimali mafunzo kwa kuzalisha wataalamu kutumikia ukanda wa bahari, ambao watumishi wake wanaitwa mabaharia. Dhima hapo ni kuhakikisha dhamira yake ya kutumia uchumi wa bluu kuongeza pato la taifa.

Hapo ndipo, inapotajwa uchumi wa bluu na mambo ya bahari, ni ngumu kukiweka kando Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), ambacho pamoja na mambo mengine kinahusika kuwapika wataalamu wa baharini.



**MKUU WA CHUO**

Hali ikoje? Kaimu Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk. Tumaini Gurumo, anabainisha kuwapo uhitaji mkubwa wa walimu wa mabaharia na wataaluma wengine waliobobea wa bahari, kutoa majibu ya mahitaji ya kitaifa, kwani hadi sasa elimu hiyo kwa kiasi kikubwa inatolewa nje ya nchi.

"Kuipata ni mpaka mtu awe na uwezo au apate ufadhili na gharama za kuwasomesha huko nje ya nchi si ndogo, huhitaji kuanzia Sh. milioni 60, Sh. milioni 100 mpaka Sh.milioni 150, sasa utasomesha wangapi?" anasema.

Anafafanua kwamba, uhitaji huo hauishii chuoni aliko, pia kwa upande wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), ambao ndiyo wasimamizi wa masuala ya bahari kitaifa, nao wana uhaba wa watumishi wenye weledi wa masuala ya bahari.

Dk. Gurumo anasema, kwa sasa taifa linapoingia katika zama za uchumi wa bluu, ni ngumu kufikia malengo, kama hakutakuwapo rasilimali watu ya kutosha iliyobobea na yenye weledi katika maeneo hayo.

Anasema, kutokana na miaka mingi Tanzania hakukuwapo na msukumo wa kutosha kuinua taaluma katika eneo la bahari, umefanya nchini si wengi wenye uelewa wa kutosha kuhusu eneo hilo la kitaaluma.

"Kazi kubwa iliyopo wengi wanakimbilia kwenye sheria, madarasa ya sheria yamejaa, wengi wanakimbilia kwenye udaktari, lakini kumbe kuna fursa pana zaidi katika eneo la mambo ya bahari.

"Chuo chetu tunachokifanya ni kusisitiza utoaji elimu kuwajulisha wazazi, walezi, wanafunzi wa kidato cha nne na sita wafahamu wigo mpana uliopo katika masuala ya bahari ili waweze kusoma," anaeleza.

Anabainisha kwamba, katika chuo hicho cha DMI, walimu waliopo ni nusu ya uhitaji na katika kuziba pengo hilo, wamekuwa wakiwatumia walimu wa muda na wengi wao wameshastaafu.

"Ili nimpate baharia tunayemuita ofisa, huenda mpaka miaka mitano, akisoma darasani miezi sita, anakwenda baharini miezi 12, akirudi anafanya mtihani wa majadiliano mezani anapata cheti cha TASAC, anarudi darasani mwaka mzima, anaenda baharini mwaka mzima.

"Kwa sasa pale DMI tuna programu zinazosimamiwa na NACTE (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi), anapata Shahada ya Kwanza, mfano ya Uhandisi Bahari na Teknolojia, akimaliza miaka yake minne darasani anapewa cheti, zaidi ya hapo anakwenda baharini mwaka mmoja, anapata sifa ya kufanya mtihani wa majadiliano mezani au 'TASAC', hata anakuwa ofisa wa melini.

Mafunzo mengine anayataja yanayotolewa nchini kuanzia mwaka mmoja, miaka miwili, mitatu na minne. Hali kadhalika, anasema yapo mafunzo ngazi shahada ya uzamili, kati ya mwaka moja na miwili.

Pia, anazungumzia fursa za mafunzo ya muda mfupi ambazo hutolewa na baadhi ya nchi, akitaja mojawapo ni ya nchini India, akizisifu zina msaada mkubwa hasa kwenye kutumikia bahari.

**WANAWAKE JE?**

Dk. Tumaini anasema hakujawahi kuwapo uwiano mzuri kati ya wanawake na wanaume wanaotumika katika sekta ya bahari. Anaendelea:"Kuanzia miaka hiyo ambako masuala ya bahari au usafirishaji baharini ulianza, sekta hii imekuwa ni ya wanaume.

"Kwanini wanaume? Mazingira yaliyokuwapo huko nyuma yalikuwa magumu kuliko leo. Huko nyuma, meli ilikuwa inaondoka bandari moja hadi nyingine kwa miezi sita, ilikuwa vigumu mzazi kuruhusu binti yake.

"Hata sasa tunapata kazi kuwaambia wazazi au walezi mambo yamebadilika na kwamba zipo meli za utalii na ndani yake wanafanya kazi watu wa hoteli na hubeba watu 8,000, wanawake na wanaume.

"Lakini, hata sasa bado hatujafanikiwa bado, meli nyingi hazijaweka vifaa kwa ajili ya wanawake. Kwa upande wa chuo, idadi ya wanafunzi nilio nao chuoni hasa upande wa baharini, wanawake ni asilimia moja ya wanafunzi wote ninaowafundisha. Wengi ni wa nchi kavu.

"Tukitoa, wapo wanaoendesha vyombo vijana wa kike wazuri, tunao wahandisi wa meli, siwezi kufika, lazima apambane atakutana na changamoto zake," anaeleza.

**HISTORIA YAKE**

Dk. Tumaini anatumia mfano wake binafsi, kwamba hakufikiria kutokea siku moja angekuwa kwenye sekta ya bahari, lakini baada ya fursa kutokea aliipokea na akaifanyia kazi.

"Tangu nimeingia kwenye sekta hii sijawahi kutamani kutoka. Hata leo hii, sitamani kwenda kufanya kazi nyingine yoyote nje ya sekta ya bahari. Ni sekta ambayo ni pana na nzuri.

> **"Kuipata ni mpaka mtu awe na uwezo au apate ufadhili na gharama za kuwasomesha huko nje ya nchi si ndogo, huhitaji kuanzia Sh. milioni 60, Sh. milioni 100 mpaka Sh.milioni 150, sasa utasomesha wangapi?" anasema.**

"Wazazi tusiwazuie zipo meli, siyo lazima waende kwenye masafa marefu, zipo meli Dar es Salaam na Zanzibar wanaweza kufanya kama mhandisi au kapteni (nahodha)."

Anasimulia kwamba, baada ya kumaliza kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Zanaki mwaka 2000, alichukua mafunzo ya mwaka mmoja ya Diplomasia na Uhusiano wa Kimataifa katika Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam.

Kwa hatua iliyofuata, anasimulia wazazi wake wakamshauri kwenda kusoma Shahada ya Sheria katika Chuo Kikuu Tumaini Iringa, ambako alipohitimu mwaka 2005, akaajiriwa kufundisha chuoni DMI.

"Wapo vijana wanafeli shuleni, anafanya uzembe anasema kwamba hili halikuwa chaguo langu. Kama ulikubali kwenda wazazi au walezi wakakulipia ada, lazima ufanye bidii ufaulu, ndicho nilichokifanya nikiwa chuoni.

"Baada ya kupata kazi mwaka mmoja mbele, Mkuu wa Chuo aliniita akaniambia, 'sijawahi kuwa na mwanasheria hapa chuoni kwangu. Ninataka uende shule, ninaamini ukienda utafanya kazi zako vizuri'.

"Alinipa fomu na nilienda katika chuo cha World Maritime University nchini Sweden, baada ya kupata ufadhili wa asasi ya Nikon Foundation ya Japan." anasimulia.

Anasema elimu aliyoipata nchini Sweden, imemuwezesha kubaini fursa kubwa zilizopo kwenye eneo la bahari na alipomaliza akajiendeleza, hata mwaka 2009 alirudi shule na kuchukua Shahada ya Uzamivu (PhD) kwa miaka mitatu na nusu nchini China katika chuo kiitwacho Dalian Maritime University.

Baada ya hapo anasema, kiu yake kubwa ikawa ni kueneza masuala ya bahari na namna ambavyo Tanzania inaweza kunufaika nayo.

Katika kutimiza azma hiyo na kuhakikisha vijana wengi nchini wanapata fursa ya kuelimika na mambo ya bahari, mnamo Oktoba Mosi mwaka huu, Dk. Tumaini akiwa katika kongamano kimataifa baina ya Tanzania na India lililofanyika Dar es Salaam, akawa na mada yake.

Hapo akaanika angalizo lake kitaaluma kuhusu haja ya kuwa na fursa ya elimu ya bahari kwa vijana wa Kitanzania, jambo ambalo likaungwa mkono na Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan.

Balozi Pradhan akasema, nchi yake imejitolea kuisaidia Tanzania kufikia malengo ya uchumi wa buluu kwa kuwasaidia Watanzania wanaotaka kusoma eneo la mambo ya bahari, wapelekwe India katika vyuo vyenye ubora huo.

Katika hoja hiyo, Balozi Pradhan anasema India inatambua dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha Tanzania inafikia uchumi wa bluu, hivyo wako tayari kuwasaidia wanaotaka kusoma mambo yanayohusiana na bahari.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wanahabari tuache uchawa wetu kwa hawa wanasiasa






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

SASA hivi Mtanzania mwenzangu ukitaka kujua nchi inakwendaje na iko wapi, usikose taarifa ya Kikosi Kazi cha Chifu Hangaya kilichotafiti masuala ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Mimi leo kwa heshima na unyenyekevu, nijikite kwenye hili linalotuhusu la uandishi wa habari, unapofika wakati wa uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushauriana na vyombo vya habari vya umma, wagombea na vyama vya siasa huandaa mwongozo kwa vyombo vya umma, kwa mujibu wa kifungu cha 53 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Mwongozo unalenga kutoa fursa sawa kwa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa vyama vyote vya siasa, kueleza ilani, sera za vyama vyao na kutangaza habari za mikutano ya kampeni kwa kutumia vyombo vya habari vya umma.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TEMCO) ya mwaka 2015, masuala ya habari husimamiwa na sheria, lakini hakuna chombo kinachosimamia vyombo vya habari kwa ujumla na vyombo binafsi haviwajibiki kisheria kufuata Mwongozo huo.

Hali hiyo imezaa malalamiko kwa wanasiasa, vyama vya siasa (upinzani), watazamaji na waangalizi wa uchaguzi, kuwa baadhi ya vyombo huwa na upendeleo wa wazi, kwa kuchapisha au kufifisha habari za baadhi ya wagombea na vyama.

Kukua kwa teknolojia ya mawasiliano, kumesaidia wanasiasa kuanzisha akaunti za mawasiliano ya kijamii kama vile Facebook, Twitter, instagram, telegram na mingine ambayo huitumia kufikia wafuasi wao moja kwa moja na kirahisi, bila kupitia kwa wanahabari wanaowalalamikia.

Ukuaji huo wa teknolojia, umekuja na changamoto zake, mathalani baadhi ya wanasiasa na wadau wamekuwa wakitumia mitandao kusambaza habari za kughushi, kutoa lugha za kuudhi, kejeli, matusi na upotoshaji kwa baadhi ya wagombea.

Hayo sasa, yakasababisha kutungwa kwa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015 na Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2018. Hivi ndivyo, tunavyolizwa sasa na sheria hizo zinazokanyaga uhuru wa habari nchini na kilio kinapazwa ili ziboreshwe.

Sasa basi, pamoja na hali hiyo, kilichobainika kwetu wanahabari ni cha kusikitisha, mathalani tunasemwa kwamba tunakandamiza wapinzani kwa kuwanyima uhuru wa kutumia vyombo vyetu, kutokana na vitisho kutoka serikalini; je hiyo ni kweli?

Sai ni tunatumiwa na wanasiasa kutoa matusi na kejeli kwa wanasiasa wengine badala ya kujadili hoja, pia hatuko huru, kwani tunakuwa na upendeleo wa wazi kwa chama tawala, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi; mnasemaje hapo wananzengo?

Kingine, eti vyombo vya habari vya umma havitoi habari kwa usawa kwa vyama vyote vya siasa nchini; mpo? Halafu tunatuhumiwa kula mulungula mchana kweupe au kujipendekeza tukitarajia kuteuliwa tunapoandika au kutangaza habari katika kipindi cha uchaguzi; mnakataa hilo?

Kumbe watu wamegundua kuwa sisi na wanasiasa hatuaminiani, kwani baadhi yetu hatutangazi kampeni za wagombea wote kwa usawa na eti ndiyo sababu, uhusiano kati ya vyombo vya habari, vyama vya siasa na wanasiasa huimarika wakati wa uchaguzi na kufifia baada ya uchaguzi; mnaionaje hii, lakini kaukweli kapo. Lakini kumbe, kuna madai, kuwa baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa huelekeza wafuasi wao kushambulia wanahabari au kutotoa ushirikiano kwa baadhi ya vyombo vya habari, wakati wa kampeni; hii si sawa kwa kweli.

Hii sasa ni baba lao, kwamba baadhi ya wanahabari hujinasibisha na vyama vya siasa au kushiriki siasa, huku wakiendelea kufanya kazi ya uandishi wa habari, hali inayoondoa imani ya wananchi kwa vyombo vya habari; nani anabisha hapa, wakati wengine tumewakuta ndani ya magwanda kabisa!

Kwa kweli, kuna haja ya kukaa chini na kuangalia nini cha kufanya, ili kuondokana na makandokando haya yanayotuzingira mpaka tuonekane wachafu mbele ya jamii, na hivyo kukosa imani nasi.

Tunashauriwa kuunda chombo cha kusimamia maadili ya wanahabari na vyombo vya habari; ukiwapo pia utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa sheria husika, ili vyombo vya habari vya umma vitoe fursa sawa, ya kutangaza habari za wagombea na vyama vya siasa wakati wa uchaguzi bila upendeleo.

Lakini la msingi, ni kuandaliwa kanuni zitakazoelekeza vyombo vya habari kuheshimu maadili ya taaluma ya uandishi wa habari, ikiwamo mwanahabari kuhakikisha anahakiki habari kabla ya kuitoa. Tukikosea hapa tumekwisha na tutaendelea kuitwa chawa wa wanasiasa. Alamsiki!

UCHUMI

# Jiji Tanga 'linavyowatoa' wakazi kwa mikopo mtaji waanzie safari mpya

**Na Boniface Gideon, TANGA**



Meya wa Jiji la Tanga Abdulrahman Shiloo ( wa pili kushoto mwenye kofia) akiwakabidhi wana vikundi mikopo isiyokuwa na riba yenye thamani ya Sh. mil.377 hivi karibuni.

JIJI la Tanga linaendelea kukua kwa kasi zaidi kila uchwao, japo wengine husunsani Wazee wetu waliokuwepo miaka ya 1970-2000 wanasema jiji hilo lilikuwa moto wakuotea mbali kwenye uchumi hasa wa viwanda, maelezo ya wazee wetu wanadai kuwa wao pia ni wahamiaji kutoka mikoa ya bara na walikuja Tanga kutafuta ajira kwenye viwanda wakati huo.

Ujio wa bomba la mafuta na ujenzi unaoendelea wa Barabara ya Tanga-Pangani-Pwani unaonekana kuliamsha Jiji la Tanga Kibiashara kutokana na ongezeko kubwa la Watu na mzunguko mzuri wa fedha kupitia biashara,

Kwa sasa, Tanga Mjini kupata chumba cha kulala wageni ni shida kubwa sana na inakulazimu kuweka oda mapema kabla ya kuja Tanga Mjini kwa walio nje ya mji huu .

Vijana wa Jiji hilo lenye mpangilio mzuri wa ujenzi wa majengo kwa kufuata mlolongo wa barabara, vijana wengi wanaonekana hawataki kuwa vibarua kwenye miradi hiyo mikubwa miwili, inayoendelea, bali wanataka kuwa wafanyabiashara

Ujio huo unaonekana kuwaamsha vijana wengi ili wazitumie fursa za kibiashara kutokana na ujio wa wageni wengi kutoka ndani na nje ya nchi, vijana wengi wamechangamkia fursa hiyo kwa kuchukua mikopo Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Halmashauri hiyo ya Jiji la Tanga nayo ipo mstari wa mbele kuhakikisha vijana, wanawake na wenye ulemavu wanatimiza ndoto zao tena kwa wakati kupitia uwekezaji.

**HALMASHAURI YATOA MKOPO**

Ili kutimiza ndoto zao Halmashauri hiyo ya Jiji la Tanga, hivi karibuni imekabidhi Sh.Mil.377 ukiwa ni mkopo kwa Vikundi 43 vya uzalishaji mali kwa kipindi cha mwaka 2022/23. Lengo ni kuhakikisha vijana wanaitumia fursa ya kiuchumi katika mradi huo wa bomba la mafuta ambao tayari umeshaanza kazi kwa baadhi ya kampuni zilizopewa tenda ya mradi.

Katika mikopo hiyo, wapokeaji wengi wanatoa ahadi ya matumizi sahihi ya mkopo na marejesho kwa wakati na kwamba hawatorudia makosa ya watangulizi wao ambao wengine wametokomea kusikojulikana na halmashauri hiyo inafanya mpango wa kisheria, kuchukua hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria na taratibu za mikopo nchini.

**ONYO LA HALMASHAURI**

Meya wa Jiji la Tanga, Abdulrahman Shiloo, anatoa angalizo la kurudisha kwa wakati ili kuviwezesha vikundi vingine pia viweze kukopeshwa.

"Niwaombe nyie mliopata bahati kupata mikopo hii isiyokuwa na riba mkaitumie kwa malengo yaliyokusudiwa, hatutarajii mtu amepata mkopo anaenda kufanya anasa" anasisitiza Shiloo

Meya Shiloo, anavipongeza vikundi vyote vilivyokamilisha marejesho ya mikopo yao ya awali na hivyo kustahili kuongezewa, na pia kuvitaka vikundi vipya vilivyofanikiwa kupata katika awamu hii kuitumia kwa makusudio yaliyoorodheshwa katika mikataba yao.

"Natoa wito kwenu wote kuzitumia fedha hizo kwa uangalifu, uaminifu ili ziweze kuleta tija kwa wanavikundi wote na hatimaye muweze kurudisha mikopo hiyo kwa wakati", anasema Shiloo.

Mstahiki Meya anawakumbusha wana - vikundi kwamba mikopo hiyo ni mtihani kwao kwani ni kipimo kitakachowapima uwezo wao wa kuongezwa au kupunguziwa mkopo.

Shiloo anasema, katika kipindi kilichopita cha mwaka 2021/22, Halmashauri ya Jiji la Tanga ilitoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh milioni 980 kwa vikundi visivyopungua 20, vikundi hivyo vinajumuisha Vijana, Wanawake na Walemavu.

**MKURUGENZI HALMASHAURI**

Mkurugenzi wa Hamashauri ya Jiji, Tanga, Dk.Spora Liana, anasema kwamba vijana 70 waliokopeshwa pikipiki kwa ajili ya kazi ya bodaboda kutoka kundi la vijana wametoroka na kwamba hatua za kisheria zinatayarishwa wabanwe kuzirejesha.

Kwa mujibu wa Dk. Liana, kitendo cha kutoweka vijana hao wa bodaboda, tayari wamejiondoa katika stahiki ya kukopesheka katika awamu ijayo, akisema: "Hawa vijana 70 wamejiondolea sifa za kupata mikopo, wameingia mitini.

**WANUFAIKA MIKOPO**

Nao wafaidika wa mikopo hiyo, waliipongeza Serikali kwa kuwajali Wananchi kwa kutoa mikopo ili wajiendeleze.

Rashidi Hussein wa kundi la Vijana kutoka Kindi Farmers Youth Group kikundi kinachojihusisha na biashara ya kuuza mchele wa jumla na reja reja anasema wamepewa mkopo wa Sh.milioni 40 ukilinganisha na kipindi

kilichopita ambapo walipata mkopo wa Sh.milioni 20 na kumudu kurudisha katika kipindi kifupi tu cha miezi saba na kwamba wanaitumia fursa ya 'ongezeko la watu wa bomba la mafuta kama sehemu kubwa ya kiuchumi.'

"Unajua sisi wateja wetu wakubwa ni 'Mamantilie' na tunauza mchele kwa bei ya chini sana na kwa sasa mji wetu una wageni wengi sana hasa wa bomba la mafuta na mafundi wa Barabara ya Tanga Pangani- Pwani.

"Hii imerahisisha sana mzunguko mzuri wa fedha, 'Mamantilie' na hoteli zipo 'bize' sana hivyo hata sisi tunauza sana mchele na malengo yetu ni kuongeza kiwango cha mtaji wetu hadi shilingi milioni 100 kwa muda mfupi," anaeleza Rashid Seif Ally kutoka kundi la walemavu anasema, mkopo wao waliopata

watanunua bajaji watakazotumia kama bodaboda, Bora Charles Mkassa, kutoka kundi la wanawake,anasema watatumia mkopo wao kuendeleza biashara ya kufuga kuku wa mayai.

"Lengo ni kutumia fursa za Mradi wa Bomba la Mafuta ambapo tayari wameanza kazi na hapa mjini, kuna ongezeko kubwa sana la watu ndio maana hata kupata hoteli au gesti ya kulala ni 'ishu' kubwa sana. Kwa hiyo na sisi tunataka tuitumie fursa hiyo tukafanye biashara huko huko kwenye Mradi wa Bomba la Mafuta" anasisitiza Seif



Baadhi ya wanufaika wa mikopo wakisubiri kukabidhiwa na Halmashauri ya Jiji la Tanga hivi karibuni. **PICHA ZOTE: BONIFACE GIDEON.**

## UCHUMI

### MARIA WATEYE;

# Mwanafunzi anayeonyesha makuu ya kipaji cha kujiajiri yungali darasani shule

**Na Mary Mosha, MWANGA**




Maria Wateye mwanafunzi wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondani Kifaru, akionyesha sehemu za kazi zake katika maonyesho ya Siku ya Ubunifu/ vipaji yaliyofanyika shuleni hapo. **PICHA: MARY MOSHA.**

KUTEGEMEA kuajiriwa mara baada ya kuhitimu masomo katika ngazi mbalimbali, bado ni kilema kilichowasonga wahitimu kwa takribani asilimia 89 nchini.

Ni hali imechangia kuwepo malalamiko mengi ya ukosefu wa ajira kwa wengi na wengi wao wakiendelea kuilalamikia serikali kwenye mitaala iliyopo nchini na wengine kuangusha mzigo huo kwa walimu kushindwa kuwafundisha wanafunzi mafunzo kwa vitendo.

Wakati mzigo huo wa lawama unapoangushwa kwa walimu, walimu nao wameurudisha kwa wazazi kwa kuwadekeza watoto na kushindwa kuwapa kazi za mikono zinazowasaidia kujitambua huku baadhi yao wakitumia lugha zisizo na staha kwa walimu mara wanapowa adhibu na kuwapanga kazi mbalimbali za mkono.

Pia, bado wapo watoto na vijana wachache walioweza kujitambua baada ya kuwezeshwa na wakafundishika.

Katika mada hiyo, Nipashe imekutana na Maria Wateye, mwanafunzi wa kidato cha sita mkondo wa EGM , aliyeibuka kinara katika mashindano ya ubunifu(Career day) yaliyojumuisha shule ya sekondari Msangeni na shule ya sekondari Kifaru zilizopo wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Anasema, ndoto yake ya uchoraji imepaliliwa na baba yake Christian Wateye, ambaye siku zote aliweza kumnunulia vifaa mbalimbali vya kuchorea zikiwemo rangi ili kufanikisha ndoto yake.

Maria ni mwanafunzi wa kidato cha sita shule ya sekondari ya Kifaru, anasema kwa sasa ana uwezo wa kuchora majengo, nyumba na watu kwa kuwatazama au kwa vipimo.

Anasema, pia anachora katuni na mazingira zinaoelezea mambo mbalimbali anazoziweka kwenye mfululizo maalumu bila ya kuwa na maneno kwa ajili ya kuchangamsha ubongo wa watoto katika kufikiri na kujua nini kinaendelea.

"Vitabu hivi vinakuwa na mfululizo wa picha mbalimbali zikiwemo za miti wanyama, mito, maziwa na midoli mithili ya watu itakayo wasaidia watoto kuwa wabunifu katika kuelezea kilichopo ndani, hii itawasaidia watoto maarifa zaidi," anasema

Anajitambulisja kwamba, yeye ni mtoto wa pili kati ya wanne wa Christian, baba yake ni mwalimu jijini Tanga, akisema:

"Kumchora mtu kwa nusu mithili ya 'Passport' inanichukua saa tatu hadi nne ambapo anakuwa amekaa sehemu moja bila kusogea, nimeweza kumchora rafiki yangu kwa kunipa picha yake, ingawa kwa sasa muda mwingi nawekeza kwenye masomo ili kuweza kufanya vizuri zaidi katika mitihani yangu ya kidato cha sita.

Ninaporejea nyumbani, baada ya shughuli ninazopangiwa /zilizopo huchukua muda mwingi kujichorea picha mbalimbali zinazotolewa kwenye magazeti na vitabu mbalimbali hii ni kutokana na kuwa sina simu janja ya kunisaidia kuona picha nyingi zaidi, "

Anafurahishwa na mchoraji gani mkubwa hapa nchini?

Anasema hadi sasa hajaona msanii wa uchoraji anaoutaka hasa mwanamke na kuongeza kuwa huvutiwa sana na mchoraji Masoud Kipanya.

Anasisitiza kuwa amekuwa akifurahishwa sana na wachoraji wa katuni hasa zisizo na maelezo zinazompa mtu nafasi ya kufikiri ili kujua maana ya kitu alichotaka kumaanisha.

"Navutiwa sana na uchoraji wa Kipanya, na siku nikipata fursa ya kukutana naye nitazungumza mengi na nadhani atakuwa na uwezo mkubwa wa kunisahihisha kazi zangu," anasema Maria.

Anasema, yawezekana wapo wachoraji wengine wanafanya vizuri na tunaweza kushirikiana tukatatua matatizo yaliyopo kwenye jamii zetu kwa kuchora ila mimi siwafahmu na hajaona kazi zao kutokana na kukosa simu janja.

**FAIDA ZA KUCHORA**

Maria anasema uchoraji unasaidia kutatua matatizo yalipo kwenye jamii kwa haraka na kubadilisha hali hasa katika matumizi ya madawa ya kulevya utoro mashuleni, wizi na utunzaji wa mazingira.

"Unaweza kuchora namna ambavyo wananchi wanakata miti kwa matumizi ya kibinadamu na baadaye jamii itakavyoteseka kwa kukosa maji ya kutumia. Pia namna ambavyo wizi umetokea na watu kuchoma moto, utoro shuleni unavyoweza kuadhiri vibaya kesho ya mwanafunzi.

"Hii inasaidia hasa kwa baadhi ya jamii wasiopenda kusoma wasiojua kusoma kuingia kwenye uongo kwa haraka, ikiwa anahusika upo uwezekano mkubwa wa kuacha na kumshauri mwingine kuacha,"anasema.

Pia, anafafanua kwamba, sasa ni wajibu wa jamii kutambua kuwa uchoraji sio lazima uwe wa majengo makubwa, ramani tu na kwa kufanya hivyo anaona namna ambavyo kutumia vipaji vidogo kutatatua matatizo.

**USHAURI KWA WANAFUNZI**

Maria anasema dunia kwa sasa imebadilika ni wajibu wa kila mwanafunzi awe msaada kwenye jamii yake katika kutatua matatizo kwa kujitengenezea ajira na kuwaajiri wengine.

Anawataka wahitimu kuacha kusoma kwa kukariri na kuweka dhana ya kuajiriwa na badala yake kuwa wabunifu kwa kupata maarifa na kuwekeza katika kujiajiri.

"Umefika wakati wahitimu ngazi zote tuanze kujitafakari kama tuna msaada kwenye jamii zinazotuzunguka, ni lazima kila mmoja

INAENDELEA UK. 20

UCHUMI

## MARIA WATEYE;

# Mwanafunzi anayeonyesha makuu ya kipaji cha kujiajiri yungali darasani shule

**INATOKA UK. 19**

kuwa na zaidi ya kile alichosomea ili kuhakikisha anaweza kujiajiri na kuajiri wenzake,

"Mfano mtu amemaliza chuo kikuu akirudi mtaani aweze kuwaongoza vijana waliomaliza shule ya msingi kufanya shughuli ndogo ndogo zinazowaletea kipato, kwa kufanya hizi tutatokomeza umasikini, "anasema.

Anasema ikiwa kila mmoja amejikita katika ubunifu, tatizo la utoro shuleni litageuka historia, mimba na mporomoko wa maadili hautakuwepo na kutakuwepo na ongezeko la ufaulu hapa nchini.

Anasema ni wajibu wa kila mzazi na mlezi kutazama mwanawe na kuona kipaji alichonacho na kumsaidia katika kufikia malengo na si kuweka matakwa yake kwenye maisha ya mtoto.

"Wazazi wengi wamewekeza nguvu nyingi kwenye kutafuta pesa na kuwaacha watoto bila kuwahudumia wala kujua maendeleo yao hasa ya shule, hii inapelekea watoto kukosa maelekezo/muongozo sahihi wa namna bora ya kukuza alichonacho.

Pia, wazazi umefika hatua kuacha kuwalazimisha watoto kufanya /kusoma mnachokitaka hii hupelekea watoto kushindwa kusimamia/kuwajibika vyema nafasi hasa wanaopata ajira".



Mwanafunzi anayeonyesha kipaji kinachomfungulia njia za kujiajiri. **PICHA: MARY MOSHA.**

Aidha Maria ameomba wizara kwa kushirikiana, mashirika yasiyo ya kiserikali (Ngo) pamoja na wadau wa elimu wakati wanaendelea kufanya mabadiliko katika mfumo wa elimu, waanze na kuwasaidia vijana kujitambua na kujiamini.

"Pamoja na baba yangu kuwa bega kwa bega katika kuhakikisha anakuza kipaji changu lakini nimekuja kufundisha mengi na shirika la Glami kupitia mradi wa Kisa linalofafundisha mwanafunzi wa kike namna ya kujitambua na kujiamini, ikiwa ni pamoja na kutambua vipaji vyetu na kutuletea watu wa kutusaidia.

**MSHAURI**

Mratibu wa Ushauri Walezi kutoka shirika la Glami, Aikande Muro, anasema kwa mkoa wa Kilimanjaro wanafanya kazi katika shule 22 kwenye miradi miwili, wa binti shupavu na kisa ambao una zaidi ya wanafunzi 7000.

Anafafanua kuwa, lengo la miradi hiyo imejikita katika kuwasaidia wanafunzi kujitambua, kuwa stahimilivu na wavumilivu wanapokabiliwa na changamoto, kujiongoza na kuongoza wengine kufikiri zaidi ya kuajiriwa hasa wanapohitimu masomo katika ngazi yoyote.

"Kwa mkoa wa Kilimanjaro katika mradi wa Kisa wana shule 15 na wanafunzi zaidi ya 700 kwa mwaka 2022 /23 ambao ni wa kidato cha tano na sita, na katika Wilaya ya Mwanga tuna shule ya Mwanga, Kifaru na Msangeni, anasema Aikande.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kifaru Abdallah Mwambuka anasema mwaka 2015 katika shule hiyo kulikuwepo na vitendo vingi vya utovu wa nidhamu ikiwemo utoro pamoja na mimba zaidi ya nane na kuongeza kuwa baada ya kuanzishwa kwa elimu ya kujitambua matatizo hayo yamegeuka kuwa historia katika shule yao.

"Kwa sasa wanafunzi wa jitambue, wanawekeza muda mwingi kwa kubuni na kushauriana juu ya vipaji walivyonavyo, mfano huyu mchoraji mara nyingi utamkuta anajichorea picha mbalimbali zikiwemo za majengo na watu, miti na mazingira, na sio yeye tu wapo na wengine wengi, "anasema

Aidha Ofisa Elimu Taaluma wilayani Mwanga, Emmanuel Kipele akiwa katika hafla fupi ya uonyeshaji wa vipaji anasema vijana wanavipaji vingi ikiwa vitaendelezwa na kulelewa baada ya miaka michache ijayo,tatizo la ajira litapungua.


---

## CHEMSHABONGO NA -00 20 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. Nairobi ni mji wake mkuu
3. piga ramli 5. Shikwa
9. eleza 11.mzazi wa kiume
12.tengeneza kitu
13.nyuzi zinazotokana na viwavi vya nondo 15.idadi ya watumishi inayohitajika katika idara
17.funga nikaha 19.daima
21.desturi 23.kauli aitoayo mtu juu ya mali zake kabla ya kufa
25.kauka kwa nguo iliyofuliwa
26.Ijapokuwa


Chini:
1. kinyume cha dada
2. tarakimu
3. heshima 4. karo ya shule
6. pengine 7. fedheheka 8. tarabu
10.zao la mti itumikayo kujengea
13.kasirika ghafla 14.madhubuti
16.Mwanaume wa kwanza
18.vunja kanuni za nchi
20.alka mtu kwako
22.omba ruhusa ya kuondoka
24.yenye kuishi




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

UTAKATIFU
THAMANI
DAMU
MBABANE
AGUA
ANWANI
GAIDI
KUJIKWAA
MTUMWA
DHANA
UHABA
LIBERIA
ANGUKIA
IDADI

DUA
JUA
BIA
MKUU
MAMA




Majibu toleo lililopita







## Fundi ujenzi jela miaka 30 kwa kunajisi mwanafunzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi mkoani Mbeya, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela Gabriel Mbilinyi (28), fundi ujenzi na mkazi wa Mbalizi wilayani Mbeya kwa kupatikana na hatia ya kubaka mwanafunzi wa kidato cha tatu mwenye umri wa miaka 16.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi, Andrew Scout, baada ya kusikiliza mashahidi wa upande wa Jamhuri na utetezi na kuridhika na ushahidi kuwa mshtakiwa alifanya kitendo hicho.

"Ushahidi wa upande wa mashtaka uliotolewa na shahidi namba moja ambaye ndiye mlalamikaji alisema mwanafunzi huyo alimpigia simu na kwenda katika chumba anachoishi (mshtakiwa) ambako alimfanyia kitendo hicho hali iliyomsababishia maumivu makali ndipo muda mfupi baadaye wazazi kwa kushirikiana na walimu wake walimpeleka hospitalini Ifisi kwa matibabu," alisema Scout.

Kwa mujibu wa ushahidi wa mtoto huyo, mshtakiwa alikula chakula cha usiku na mwanafunzi huyo kisha kwenda kulala naye majira ya saa mbili usiku.

Mshtakiwa Gabrieli Mbilinyi alikiri kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanafunzi huyo tangu Januari 2022 na kumnunulia simu kwa ajili ya mawasiliano.

Daktari aliyemfanyia uchunguzi mwanafunzi huyo, alitoa ushahidi na kuthibitisha kuingiliwa na kuondolewa bikra yake.

Akitoa utetezi wake, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo na kudai siku ya tukio akiwa anarudi nyumbani kwake aliwakuta watu watatu wa jinsi ya kiume na wawili wa kike huku mmoja akiulizia chumba cha kupanga na yeye kuwajibu kuwa hakuna chumba eneo hilo, maelezo yaliyoungwa mkono na shahidi wa pili wa utetezi Augustino Christopher (20), fundi ujenzi aliyemtetea rafiki yake huyo kutomnajisi mwanafunzi huyo.

Mahakama iliridhia kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili.

Alipotakiwa kujitetea, aliomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa ni kijana anayetegemewa na ndugu zake.

Hakimu Scout alimhukumu kwenda kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela na kuweka wazi haki ya kukata rufani kwa upande usioridhika na maamuzi ya mahakama.

# TANAPA yajenga nyumba ya mganga kituo cha afya Ifupa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limejenga nyumba ya mganga katika Kituo cha Afya cha Ifupa kilichoko katika Kata ya Ilungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuunga mkono juhudi za wananchi waliojenga kituo hicho kwa nguvu zao.

Kituo hicho ni ambacho kilichangiwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa IPP, Hayati Dk. Reginald Mengi, Sh. milioni 25 baada ya kuona kupitia vyombo vya habari wananchi wakichangishana vitu mbalimbali kwa ajili ya mradi huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alikabidhiwa nyumba hiyo kwa niaba ya serikali na Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, Theodola Batiho, mwishoni mwa wiki alipofanya ziara kwenye kituo hicho kwa ajili ya kukagua mradi huo.

Batiho alisema shirika hilo lilitoa mchango huo kama sehemu ya kurejesha kwenye jamii kinachopatikana kutokana na hifadhi hiyo ambayo ipo jirani na kata ya Ilungu.

Alisema walichangia baada ya mazungumzo na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambao walikuwa wameanza utekelezaji wa mradi huo. "Tumekuwa tukishirikiana na wananchi hawa kwenye shughuli mbalimbali za uhifadhi na ndio maana baada ya kutuomba hatukusita kushiriki, jengo hili limekamilika na liko tayari kuanza kutumika," alisema Kamanda Batiho.

Alisema awali walikuwa hawana ushirikiano mzuri na wananchi wa vijiji hivyo kutokana na migogoro ya mipaka, lakini kwa sasa hali ni tofauti wanaelewana vizuri na wanashirikiana kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.

Akipokea jengo hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera alilishukuru Shirika la TANAPA kwa kujenga jengo hilo ambalo alisema ni la kisasa na linafaa kwa ajili ya matumizi ya mganga na ni zuri kuliko hata yaliyojengwa mjini.

Alisema ili wananchi hao waendelee kunufaika na misaada kama hiyo, wanatakiwa kuendelea kushirikiana na wahifadhi kulinda mipaka ya hifadhi ili isivamiwe na wahalifu ambao wanaoingia kwenye hifadhi hiyo.

Alisema wapo majangili wanaoingia kwenye hifadhi hiyo na kuchimba maua aina ya chikanda na kwenda kuyauza kwenye baadhi ya mataifa jambo ambalo alisema linasababisha uharibifu wa hifadhi.

"Nawapongeza sana ninyi wananchi kwa ushirikiano ambao mnauonyesha kwa wenzetu wa TANAPA na ndiyo maana wameguswa hata kuwajengea jengo hili ambalo ni zuri sana, endeleeni kutoa taarifa za wanaochimba chikanda," alisema Homera.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Stephen Katemba, alisema kituo hicho kilianza kwa kujengwa na wananchi na baadaye halmashauri iliwaunga mkono kwa kuchangia mapato yake ya ndani.

Alisema awali wananchi hao walikuwa wanajenga chini ya usimamizi wa maofisa wa serikali ambao waliandaa ramani na baadaye wadau wengine walichangia.

Ilungu ni miongoni mwa kata zinazopakana na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo inayovutia kwa maua ya asili yaliyoifanya ipewe jina la 'Bustani ya Mungu'.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamin Kuzaga, akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo juzi, baadhi ya silaha haramu ambazo zimesalimishwa na wananchi waliokuwa wanamiliki kinyume cha sheria. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Watumishi wawili TANESCO wafariki, 16 wajeruhiwa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WAFANYAKAZI wawili wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Wilaya ya Ileje mkoani Songwe, wamepoteza maisha papo hapo na wengine 16 kujeruhiwa baada ya ajali kutokea kwenye mteremko wa Shuba ulioko Kata ya Mbaba.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya jana alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo juzi saa tatu usiku.

"Chanzo cha ajali hii kinadaiwa ni kufeli kwa breki baada ya gari hilo kuwa kwenye mwendo kasi na kusababisha kutumbukia kwenye daraja la Mto Mwati wakati watumishi hao wakielekea kwenye matengenezo ya umeme," alisema Gidarya.

Alisema ndani ya gari hilo kulikuwa na watumishi wa TANESCO 18, wawili kati yao walipoteza maisha papo hapo huku wengine 16 wakijeruhiwa.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Ileje, Joyce Ongati alikiri kupokea miili miwili na majeruhi 16 kati ya hao, sita walipata matibabu na kuruhusiwa na wengine wanaendelea kupata matibabu.

Dk. Ongati aliwataja walipoteza maisha kuwa ni Juma Mbelwa (29) na Kanut Msafiri (32) na kati ya majeruhi hao 16, wawili ni wanawake.

"Majeruhi wawili walipewa rufani kwenda Hospitali Kanda ya Mbeya na wawili Hospitali ya Vwawa kwa matibabu zaidi baada ya kupata majeraha makubwa sehemu mbalimbali ya miili yao," Dk. Ongati alisema.





# Watanzania wafundwa matumizi ya taarifa za utabiri hali ya hewa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amewataka Watanzania kujenga tabia ya kuzitumia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa ajili ya mipango ya shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo kilimo badala ya kubahatisha.

Msigwa alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya TMA kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/22 na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema Watanzania hawana budi kutumia taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa na mamlaka hiyo ili kufanya shughuli kwa ufanisi badala ya kuendelea kubahatisha.

"Naomba nitoe wito kwa Watanzania kuzitumia taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ili kuachana na tabia ya kubahatisha kwenye kilimo pamoja na mambo mbalimbali," alisema. Kadhalika, alisema kutumia taarifa za mamlaka hiyo kutasaidia kuwa na uhakika na kile mtu anachokifanya katika shughuli zake.

"Taarifa zinazotolewa na mamlaka hii hivi sasa zina uhakika kwa zaidi ya asilimia 70, hivyo zitasaidia kujua msimu wa mvua na kiasi cha mvua na kupitia wataalamu wa kilimo, mkulima anaweza kushauriwa alime nini lakini pia ni muda gani sahihi wa msimu," alisema Msigwa.

Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri wa TMA, Dk. Hamza Kabelwa, alisema katika mwaka huu wa fedha, wamepanga mikakati itakayosaidia utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini.

Alisema moja ya mikakati hiyo ni kupanua wigo wa utoaji elimu kwa wananchi na wadau wengine juu ya umuhimu wa huduma za hali ya hewa na kuendelea na utekelezaji wa Sheria Na. 2 ya Mwaka 2019 na kanuni zake.

"Mkakati mwingine ni kuimarisha uangazaji wa hali ya hewa katika bahari na maziwa makuu ili kuimarisha usalama wa abiria na kwenye maji, shughuli za uvuvi pamoja na kusaidia shughuli mbalimbali zikiwamo upakuaji wa mizigo bandarini na uvunaji gesi asilia," alisema.

Alisema mkakati mwingine ni kufanya ufuatiliaji kwa makandarasi wanaotengeneza rada na vifaa vya hali ya hewa ili vikamilike na kuwasili nchini.

Dk. Kabelwa aliongeza kuwa mkakati mwingine ni kuongeza vyanzo vya mapato kwa lengo la kuboresha huduma za hali ya hewa na kuhakikisha wadau wote wenye vifaa vya hali ya hewa nchini wanavifunga kwa kuzingatia Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akimsikiliza mchuuzi anayefanya biashara zake kando ya barabara ya Mtaa wa One Way, jijini Dodoma jana, eneo lililopigwa marufuku na kumshauri kuhamia katika Soko la Machinga Complex lililotengwa kwa shughuli hizo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC aagiza wasiolipa mikopo kushtakiwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ameziagiza halmashauri kuzifungulia mashtaka mahakamani vikundi vinavyokopeshwa mikopo ya asilimia 10 na kushindwa kurejesha.

Alisema halmashauri zote za Dodoma zinazotoa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa vikundi vikiwamo vya watu wenye ulemavu, wanawake na vijana wanaotoroka na fedha hizo wafunguliwe mashtaka mahakamani.

Senyamule alisema hayo alipokuwa akikabidhi mfano wa hundi ya fedha zilizotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa wanufaika wa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.38 kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mkuu huyo wa mkoa alisema fedha hizo zimekopeshwa ili kuwainua wanufaika kiuchumi, hivyo ikitokea vikundi vimetoroka na kushindwa kulipa, halmashauri ziangalie namna ya kutoa adhabu itakayowabana ikiwamo ya kufungua kesi mahakamani.

"Nitoe wito kwa halmashauri zote za Dodoma ambazo zimekuwa zikikopesha vikundi vya wajasiriamali wakiwamo watu wenye ulemavu, vijana na wanawake, wakishindwa kurudisha fedha hizo, waburuzeni mahakamani," alisema.

"Fedha hizo hazitolewi kama zawadi bali ni mkopo ambao malengo yake ni kuinua mitaji na kukuza uchumi, hivyo mnaopewa mnatakiwa kuwa waaminifu na kurudisha kwa wakati," alisema.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akitoa taarifa fupi ya ugawaji wa mikopo hiyo kwa wanufaika, alisema halmashauri yake imetoa Sh. bilioni 1.38 zinazotokana na mapato ya ndani.

Alisema mikopo hiyo imetolewa kwa ajili ya vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na kwamba mikopo hiyo ni ajili ya kununua vyombo vya usafiri vya moto zikiwamo bajaji na pikipiki.

Mafuru aliwataka wanufaika hao kuhakikisha wanalipa mikopo hiyo kwa wakati pamoja na kuitumia kwa malengo husika ili wengine wapate fursa ya kukopeshwa.

## Shule zasaidiwa vifaa TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHULE tatu kongwe nchini ikiwamo Shule ya Sekondari Dodoma zimepewa msaada wa vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutoka Asasi ya Misaada ya Vodacom (VTF) vikiwa na thamani ya Sh. milioni 160.

Shule zingine zilizopokea msaada huo ni Sekondari ya Kutwa Mbeya, Sekondari ya Tunduma ikiwa ni hatua endelevu ya kusaidia ajenda ya sekta ya elimu ya kujifunza kidijitali na kuongeza upatikanaji wa habari.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliishukuru VTF katika jitihada za kusaidia elimu ya TEHAMA.

Alisema utoaji wa zana za TEHAMA katika shule ni hatua muhimu katika kuelekea mageuzi jumuishi ya kidijitali.

"Serikali ina sera ya kuunganisha TEHAMA katika elimu na kuwa na vifaa shuleni ni muhimu katika kufanikisha hili. Matumizi ya kompyuta shuleni hasa zilizounganishwa na mtandao ni mojawapo ya njia zinazotarajiwa kuboresha ubora wa elimu," alisema.

Alisema uwapo wa kompyuta shuleni zitawasaidia wanafunzi kupata rasilimali na taarifa ili kuwawezesha kufaulu katika mitihani yao, mfano mzuri ukiwa ni kupitia tovuti ya e-fahamu.

Alisema walimu wanaweza pia kutumia kompyuta kutafuta maarifa bora na kuboresha ustadi wao wa kufundisha.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo mjini Dodoma, Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania PLC, Philip Besiimire, alisema msaada huo ni sehemu ya mradi wa VTF unaolenga kuanzisha shule za urithi wa e-Fahamu kote nchini.

"TEHAMA ni muhimu katika kuboresha ufundishaji na kujifunza katika shule za sekondari na taasisi hiyo ina ajenda ya kufikia shule 1,500 za sekondari. Mchango huu utasaidia sana katika kuhakikisha wanafunzi wetu wanapata elimu ya kidijitali pia wanapata maudhui kupitia tovuti ya Vodacom ya kujifunzia (e-Fahamu) ambayo inatoa maudhui ya elimu ya kidijitali bila malipo," alisema.

Kupitia msaada huo, shule hizo zitapokea madawati 15 ya kompyuta, seti moja ya televisheni, viti 15, meza 15 na bando la mwaka mmoja kila moja kwa ajili ya kuunganishwa kwenye intaneti.

Tangu kuanza kwa programu ya e-Fahamu mwaka 2017, Vodacom Tanzania Foundation imewekeza katika shule 509 za sekondari za umma na kutumia zaidi ya Sh. bilioni 1.1.



## Vyama vya siasa vyaunga mkono maoni ya kikosi kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SIKU moja baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kupokea ripoti ya kikosi kazi, baadhi ya vyama vya siasa Zanzibar vimesema kuwa vinaunga mkono mapendekezo yote yaliotolewa katika ripoti hiyo ya kikosi kazi ikiwamo kura ya mapema ambayo ni muhimu.

Wawakilishi wa vyama vya siasa waliyasema hayo wakati wakizungumza na waandishi wa habari mjini hapo na kumtaka Rais Mwinyi kuyafanyia kazi mapendekezo hayo ambayo yataimarisha maridhiano ya kisiasa.

Akizungumza kwa niaba ya wawakilishi wa vyama 14 vya siasa, Katibu Mkuu wa Chama cha UPDP, Hamadi Muhammed Ibrahim, alisema vyama hivyo vimeridhia mapendekezo yote na kukipongeza kikosi kazi kwa kufanya kwa weledi.

Akizungumzia kura ya mapema, alisema kuwa ni vyema kura hiyo ikaendelea kuwapo lakini yaongezwe makundi mengine yenye mahitaji maalum ambayo hayakuorodheshwa.

Aliyataja makundi hayo kuwa ni wajawazito, wazee wenye umri mkubwa, wagonjwa na watu wenye ulemavu.

Alisema suala la matokeo ya urais yahojiwe mahakamani wanaunga mkono pamoja na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ianzie ngazi za chini katika mgawanyo wa nafasi za uongozi badala ya kuwapo katika uongozi wa Baraza la Mapinduzi pekee.

Alisema pia wanaunga mkono hoja ya Muungano iliyoelezwa katika ripoti hiyo ikiwamo mikataba inayopangwa katika Jamhuri ya Muungano itekelezwe ili Wazanzibar wafaidike na viongozi wanakubaliana kwa maslahi ya taifa.

Alisema kwa muda mfupi Rais Mwinyi aliokaa madarakani amefanya mambo mengi mazuri ikiwamo la kuona Wazanzibar wanahitaji kuendesha nchi yao kwa mustakabali mzuri bila ya kujali itikadi za kisiasa.

"Kikosi kazi kilichoundwa kilijumuisha vyama vyote vya siasa na kilizingatia ushirikishwaji wa vyama vya siasa kwa hiyo matarajio yetu ni kwamba yaliozungumzwa na kikosi kazi tutayaunga mkono kwa dhati tukijua ya kwamba kuipa nafasi serikali kutekeleza mapendekezo hayo," alisema.

Naye Peter Magwira kutoka Chama cha Demokrasia Makini, alisema wataungana na rais kwa kile anachokisimamia, umoja na mshikamano wa taifa unasonga mbele na kuenzi Muungano ambao ni tunu ya taifa.

# Mwinyi aiomba Sweden kuita wawekezaji Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameiomba Serikali ya Sweden kushajihisha wawekezaji wa nchi hiyo kufika Zanzibar kuwekeza katika sekta za nishati ya umeme na utalii ili kuunga mkono juhudi za kuinua uchumi wa visiwa hivyo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipozungumza na Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Charlotta Ozaki, aliyefika kwa ajili ya kujitambulisha.

Alisema katika juhudi za kuinua uchumi, Zanzibar inakabiliwa na changamoto ya umeme wa uhakika kwa kukosa vyanzo vyake binafsi vya nishati hiyo na kulazimika kutegemea huduma hiyo kutoka Tanzania Bara, huku mahitaji ya huduma hiyo yakiongezeka kutokana na kuwapo kwa shughuli nyingi za kiuchumi, ikiwamo uwekezaji katika sekta mbalimbali.

Alisema hivi sasa serikali inaangalia namna ya kupata wawekezaji kupitia nishati ya umeme wa jua, nguvu za upepo na vyanzo vingine.

Aidha, alisema Zanzibar imekuwa na ongezeko kubwa la watalii wanaokuja nchini kila mwaka, jambo linaloifanya kuwa na mahitaji ya hoteli kubwa za kisasa pamoja na maeneo ya mapumziko.

Alimweleza Balozi huyo kuwa Zanzibar imeipa kipaumbele sekta ya uchumi wa buluu katika kukuza uchumi kwa kuzingatia kuwa ni eneo lenye fursa nyingi za kiuchumi pamoja na kuibua ajira.

Hata hivyo, alisema sekta za uvuvi pamoja na kilimo cha mwani zinakabiliwa na changamoto, ikiwamo ya kiwango kidogo cha bei ya zao la mwani, akabainisha azma ya serikali ya kuona bei ya zao hilo inapanda ili kuleta tija kwa taifa na wakulima.


Dk. Mwinyi alisema Zanzibar inakabiliwa na tatizo la vijana wengi kukosa nafasi ya kujiunga na vyuo vikuu kutokana na idadi ndogo ya vyuo.

Alisema ili kutatua changamoto hiyo, vinahitajika vyuo vingi vya mafunzo ya amali vitakavyowezesha vijana wengi waliokosa nafasi ya vyuo vikuu kujiunga na kupatiwa mafunzo mbalimbali yatakayowasaidia kuendesha maisha yao. Dk. Mwinyi alisema Zanzibar pia ina mahitaji ya mafunzo kwa walimu wa elimu ya msingi na sekondari.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Mwinyi alishukuru hatua ya mashirika na wadau mbalimbali wa maendeleo kutoka nchi za Umoja wa Ulaya (EU) kuunga mkono juhudi za Zanzibar kuwaletea wananchi wake maendeleo baada ya kumalizika Uchaguzi wa Mkuu wa Oktoba 2020 na kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU) na kuomba hali hiyo iendelee.

Aliipongeza Sweden kwa misaada mbalimbali ya kiuchumi na kijamii inayoipatia Zanzibar katika sekta mbalimbali.

Naye Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Charlotta Ozaki, aliipongeza Zanzibar kwa hatua kubwa iliyofikiwa kukuza demokrasia na kuheshimu misingi ya haki za binadamu. Balozi Ozat alimhakikishia Rais Mwinyi kuwa Sweden itaendelea kudumisha ushirikiano mzuri wa muda mrefu katika nyanja mbalimbali kati ya nchi yake na Zanzibar pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akifurahia jambo na mgeni wake, Balozi wa Sweden nchini, Charlotta Ozaki Macias, baada ya kumaliza mazungumzo yao Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# KMKM yahamasishwa ufugaji mazao ya baharini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, amekitaka Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), kuendelea na ufugaji wa mazao ya baharini kwa sababu mazao hao yana soko kubwa duniani.

Aliyasema hayo juzi Kambi ya KMKM Kibwengo, Mkoa wa Kaskazini Unguja wakati akizindua mradi wa ufugaji wa vitango bahari unaoendeshwa na kikosi hicho.

Alisema zao hilo lina faida kubwa kwa sababu virutubisho vyake vinasaidia kupunguza kasi ya maradhi ya saratani.

Alikipongeza kikosi hicho kwa jitihada zake katika kuitekeleza kwa vitendo sera ya uchumi wa buluu na kwa ufugaji huo wa vitango bahari utabadilisha hali ya KMKM kwa kujiendesha wenyewe bila ya kutegemea bajeti ya serikali.

Alisema Pemba kuna maeneo mazuri ya ufugaji wa kaa na Zanzibar imeshasafirisha tani 200 za kaa na soko lake kubwa ulimwenguni na kwamba ni vyema KMKM ikaitumia fursa hiyo.

Alisema lengo la KMKM ni kuwa na matango bahari yasiopungua milioni moja.

"Upatikanaji wa fedha serikalini ni mgumu, lakini mmejiongeza wenyewe sio tu kulinda mipaka na maji ya Zanzibar, lakini ipo kibiashara na kiuchumi zaidi," alisema.

Aliwataka wananchi kuitumia bahari kwa maendeleo endelevu na kuilinda na uchafuzi wa mazingira kwa maendeleo endelevu.

Luteni Kamanda wa KMKM, Haji Mussa Kambi ya Kibwengo, alisema uzalishaji wa shughuli za kiuchumi unaenda sambamba na kauli ya kikosi hicho na kwa juhudi kubwa za mkuu wa kikosi hicho imeanzisha mradi wa ufugaji vitango bahari ulioanza Novemba, mwaka jana kwa lengo la kuhakikisha kikosi hicho kinajitegemea kiuchumi.


Alisema katika mradi huo wamejenga mashamba 10 ya vitango bahari katika bahari iliyomo kambini hapo yenye ukubwa wa mita 60 na wanashirikiana na wataalamu wa ufugaji huo ikiwamo kituo cha utotoaji wa vifaranga vya mazao bahari ili kuendeleza ufugaji huo.

Alisema wameshafanikiwa kuingiza jumla ya vifaranga 32,000 vya matango bahari na lengo ni kuingiza vifaranga laki moja katika bahari ya kambi hiyo.

Kwa upande wake, Mkuu wa kikosi hicho, Komodoo Azan Hassan Msingiri, alisema visiwa vya Zanzibar lazima viwe na ulinzi uliotimia na ndio maana kikosi hicho hushirikiana na taasisi zingine kuilinda bahari na rasilimali zake.

Alisema dhamira ya KMKM ni kuendelea na ufugaji huo wa vitango bahari katika kambi zake zingine ikiwamo Tumbatu, Bwefumu na kisiwani Pemba ili kupata tija katika ufugaji huo.

Alisema kitango kimoja cha bahari kina uwezo wa kutoa mayai milioni moja na kuwezesha kuwa na mazao mengi na uwezo wa kupata milioni 32.





# Mawakala mbaroni tuhuma za udanganyifu usajili laini simu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MAWAKALA watano wa kampuni za simu za mkononi (majina yamehifadhiwa) wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Kagera kwa tuhuma za kuwasajili watu laini za simu kwa kutumia majina na vitambulisho vya watu wengine.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Kagera, John Joseph, alisema juzi kuwa watu hao walibainika katika uchunguzi wa taasisi hiyo, uliofanyika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka huu.

"Tumebaini kuna baadhi ya namba zimesajiliwa kwa kutumia majina ya watu wengine na ukifuatilia unakuta picha ni ya mtu mzima na wengine ni marehemu lakini laini hizi zipo zinaendelea kufanya kazi," alisema Joseph.

Kutokana na udanganyifu huo, aliwataka wananchi kuwa makini pindi wanapokwenda kusajili laini zao za simu ili kuepuka vitambulisho vyao vya taifa kutumika kusajili watu wasiowafahamu.

"Kwa hiyo niwaombe wana Kagera waende kwa mawakala wa simu na kuangalia namba zao za NIDA (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa) kujua zimesajili namba ngapi za simu. Ukikuta kuna namba huzifahamu waharifu watu wa mitandao ya simu wakazifute kwa sababu zinaweza kutumika kufanya uhalifu," alisema.

Alisema kwa sasa uchunguzi juu ya suala hilo unaendelea na kwamba baada ya kukamilika, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Amos Simon, mkazi wa Manispaa ya Bukoba akizungumza na Nipashe, aliomba serikali kuwachukulia hatua kali mawakala watakaobainika kuhusika na tatizo hilo ili kuwaepusha na madhara yanayoweza kuwakumba ikiwamo kuhusishwa na uhalifu hasa wa mtandaoni.

Simon aliiomba serikali kuhakikisha wananchi wanapewa elimu na maelekezo zaidi, ili waweze kuwabaini watu waliosajiliwa kwa vitambulisho vyao ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza ukiwamo utapeli wa kimtandao.



Mwenyekiti wa Chama cha wenye Kisukari Tanzania, Prof. Andrew Swai (kushoto), akitoa elimu ya namna ya kutoa taarifa zenye kuelimisha jamii kuhusu magonjwa yasiyoambukiza kwa waandishi wa habari wa Kanda ya Ziwa, jijini Mwanza juzi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Magonjwa yasiyoambukiza tishio nchini

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MWENENDO mbovu na mtindo wa maisha ya binadamu, vimeendelea kusababisha ongezeko la vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukizwa ambavyo vimefikia asilimia 34 ya vifo vinavyotokea nchini.

Hatua hiyo imesababisha magonjwa hayo kuwa tishio zaidi duniani kutokana na kuwa chanzo cha zaidi ya asilimia 70 ya vifo vyote.

Akitoa elimu ya magonjwa yasioambukiza kwa waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali Kanda ya Ziwa, Mwenyekiti wa Chama cha Wenye Kisukari (TDA), Prof. Andrew Swai, alisema magonjwa hayo kwa sasa yamekuwa tishio yakizidi yale yanayoambukiza.

Alisema asilimia 75 ya vifo vyote vinavyohusu watu wenye umri kati ya miaka 30 -70 hutokana na magonjwa hayo yanayosababishwa na mabadiliko ya mtindo wa maisha.

Prof. Swai alisema utafiti wa mwaka 1986/87 unaonyesha mtu mmoja kwa kila watu 100 alikuwa na kisukari na watu watano kwa 100 walikuwa na shinikizo la juu la damu huku sababu za kuongezeka kwa magonjwa hayo zikiwa ni mabadiliko ya mtindo wa maisha ikiwa ni pamoja na ulaji usiofaa.

Alisema sababu nyingine ni pamoja na kutojishughulisha mwili, matumizi ya tumbaku na pombe, utawala duni wa msongo wa mawazo, kutopata usingizi wa kutosha, ajali, matukio ya ukatili, unyanyasaji na utekelezaji wa majanga.

Prof. Swai aliyataja magonjwa hayo ni kisukari, saratani, shinikizo la juu la damu, mafuta mengi kwenye damu, magonjwa ya moyo na mishipa ya damu na mfumo wa hewa. Aliwataka Watanzania kudhibiti magonjwa hayo kwa kuepuka ulaji usiofaa wa vyakula.

Alitaja mwenendo unaofaa kuwa ni pamoja na ulaji wa mlo kamili, upimaji wa afya na kufanya uchunguzi mara kwa mara ili kuyagundua mapema, kupunguza msongo wa mawazo, kufanya mazoezi na kuepuka kukaa muda mrefu ili kulinda afya.

"Mtu anaweza kuwa na magonjwa yasiyoambukiza kwa miaka kadhaa bila dalili huku mwili ukiendelea kuathirika. Mfano shikizo kubwa la damu, pia ugonjwa wa kisukari unaweza usiwe na dalili hadi macho, figo, moyo au mishipa ya damu au fahamu inapokuwa imeharibika vibaya," alisema.

Alisema kila mtu ahakikishe uzito unakuwa katika kiwango kinachofaa, kupunguza unywaji wa pombe na matumizi ya tumbaku kwa sababu matibabu ya magonjwa ya moyo na kisukari ni ya gharama kubwa na yanatumia asilimia 4 ya pato la taifa pia wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) wanatumia asilimia 20 ya mfuko.

Naye Dk. Waziri Ndonde, mtaalamu wa mazoezi alisisitiza ili kulinda afya na kuifanya kuwa imara na lazima kufanya mazoezi ya viungo mara kwa mara.

Naye Leon Bahati kutoka Chama cha Magonjwa Yasiambukiza, alisema lengo la chama hicho ni kuwafanya watu waelewe vizuri magonjwa hayo na madhara yanayosababishwa na mtindo wa maisha kwani kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na jamii isiyo na magonjwa yasiyoambukiza.

Kilele cha Siku ya Magonjwa Yasiyoambukiza kinatarajia kufanyika kitaifa mkoani Mwanza Novemba 12, mwaka huu, huku maadhimisho hayo yakibebea kaulimbiu ya "Tutembee Pamoja Katika Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza".

# Waacha masomo ili kutafuta maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TATIZO la ukame katika baadhi ya maeneo ya Kahama mkoani Shinyanga, limesababisha wanafunzi wa Shule ya Msingi Mwanzwagi Kata ya Mondo, kuacha masomo na kuhangaika kutafuta maji katika nyumba za watu kwa ajili ya matumizi ya shuleni na nyumbani.

Hayo yalibainishwa juzi na Diwani wa Mondo, Kija Peja, katika kikao cha kawaidia cha Baraza la Madiwani cha manispaa hiyo cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23. Alisema suala hilo lisipotatuliwa kwa wakati wanafunzi watashindwa kufanya vema katika masomo yao.

Alisema, wanafunzi hao wamekuwa wakisambaa kwenye makazi ya watu kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya shuleni na kwamba tatizo hilo limekuwa kubwa ndani ya kata ya Mondo hali inayohatarisha kufungwa kwa shule mpaka huduma hiyo itakapopatikana.

"Tusipotatua tatizo hili wanafunzi hawatakuwa na uwezo wa kufanya vema katika mitihani yao ya mwisho ikiwa ni pamoja na kufungwa kwa shule hizo," alisema.

Katika hatua nyingine, Diwani Peja alisema wananchi wa kata hiyo wanalazimika kwenda hadi katika kata jirani ya Kinaga kwa ajili ya kutafuta maji katika visima vilivyoko na kushauri viongozi kushirikana na mamlaka za maji kutenga bajeti ya dharura na kuwanusuru wananchi wa eneo hilo hususani wanafunzi.

Nay Diwani wa Iyenze, Lucas Makulumo, aliitaka manispaa kuangalia jinsi ya kuwasaidia watu wa eneo hilo na kutathimini hali ya hasara ikoje ikiwa ni pamoja na mifugo ambayo imekuwa na hali mbaya kutokana na hali hiyo ya ukame iliyoko.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA), John Mkama, alikiri kuwapo kwa tatizo kubwa la maji na kuahidi kuangalia namna ya kupeleka maji katika eneo hilo kupitia mradi wa Kagongwa- Isaka uliopita sehemu ya kata hiyo.

Alisema mpaka sasa tayari wamefikisha maji katika senta kubwa ambayo ni Mondo na kuwaomba wasimamizi wa elimu kuangalia namna bora ya kufikisha maji katika shule za msingi na sekondari kwa kutenga fedha sehemu ya bajeti zao ili wanafunzi wasiendelee kukosa masomo wakitafuta maji.

Awali Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Clemence Mkusa, alisema kwa kushirikana na mamlaka za maji zilizoko, wataangalia namna bora ya kutatua tatizo hilo ili wananchi wapate maji na kunusuru mifugo isipoteze maisha kwa kukosa maji.

## HABARI KIMATAIFA



Ujumbe maalumu wa Umoja wa Afrika ukishuhudia wawakilishi wa pande zinazohasimiana wakiweka saini makubaliano yaliyofikiwa kati ya serikali ya Ethiopia na Tigray jana. **PICHA: REUTERS**

# Dunia yapongeza makubaliano Ethiopia

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

VIONGOZI mbalimbali duniani wamepongeza makubaliano yaliyofikiwa na pande hizo mbili katika vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Ethiopia.

Makubaliano hayo yanamaliza uhasama katika mzozo huo uliodumu kwa miaka miwili.

Utiliaji saini wa makubaliano yalifanyika Jumatano nchini Afrika Kusini na kusimamiwa na Umoja wa Afrika.

Rais wa Senegal ambaye ni mwenyekiti wa AU Macky Sall, alielezea tangazo hilo kama habari njema.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres alikaribisha makubaliano hayo na amewataka Waethiopia wote na jumuiya ya kimataifa kuunga mkono hatua ya ujasiri iliyochukuliwa na pande hizo mbili zinazopigana.

"Mkataba huo ni hatua muhimu ya kwanza ya kumaliza mzozo mbaya wa miaka miwili ambapo maisha ya Waethiopia wengi yamepotea,"alisema Guterres.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, alipongeza hatua hiyo muhimu, na kubainisha kuwa nchi yake itaendelea kushirikiana kwa karibu kuunga mkono juhudi zinazoendelea kuongozwa na AU katika wiki zijazo.

Rais wa Kenya William Ruto, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani Annalena Baerbock na EU, wote walipongeza juhudi za pande hizo mbili za kurejesha amani nchini Ethiopia.

Lakini wasuluhishi wameonya kuwa bado kuna kazi ya kufanya.

"Suluhisho la kudumu linaweza tu kuwa kwa ushirikiano wa kisiasa na kuweza kustahimili tofauti zetu, utofauti wetu, huku tukibaki Ethiopia iliyoungana," rais wa zamani wa Kenya Uhuru Kenyatta, ambaye alisaidia kufanikisha mpango huo, alisema. **BBC**

# Mataifa ya Afrika kuamua usafirishaji nafaka Ukraine

**ANKARA,** UTURUKI

RAIS wa Uturuki Recep Erdogan amesema makubaliano ya kusafirisha mauzo ya nafaka kutoka Ukraine yatazingatia mahitaji ya mataifa ya Afrika yanayokabiliwa na njaa.

Alisema yeye na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky wamejadiliana jinsi ya kupeleka nafaka katika nchi za Afrika.

"Hali ya Djibouti, Somalia na Sudan si nzuri hata kidogo. Iwapo kutakuwa na tatizo katika nchi nyingine ambazo hazijaendelea, tutafanya usafirishaji hadi nchi hizi," alisema Erdogan katika mahojiano na kituo cha utangazaji cha Uturuki ATV. Mkataba huo wa nafaka uliratibiwa na Umoja wa Mataifa na Uturuki mwezi Julai, na hivyo kuhitimisha mzingiro wa miezi mitano wa Russia dhidi ya bandari za Ukraine ambao ulinasa mamilioni ya tani za nafaka na mafuta ya alizeti na kusababisha bei ya vyakula kupanda.

Mkataba huo unamalizika tarehe 19 Novemba na wale wanaohusika bado wanapaswa kukubaliana kurefusha muda huo.

Russia ilikuwa imejiondoa katika mpango huo, lakini ilikubali wiki hii kuanza tena ushiriki wake katika makubaliano hayo.

Jumuiya ya kiarabu yakataa

Viongozi wa kiarabu wamekuwa makini kutochukua msimamo katika vita kati ya Russia na Ukraine, badala yake wametoa wito wa suluhu ya kisiasa katika mgogoro huo.

Katika mkutano wa kilele wa Jumuiya ya nchi za kiarabu Arab League, uliofanyika nchini Algeria kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka mitatu kufuatia janga la Corona, viongozi hao kwa pamoja walisema suluhu ya kisiasa katika mgogoro huo inapaswa kuendana na sheria ya Umoja wa Mataifa na kuzingatia usalama wa mataifa husika.

Mataifa kadhaa ya kiarabu yamewahi kusema yanaweza kuchukua jukumu la kuwa mpatanishi katika vita hivyo, katika jitihada za kudumisha uhusiano mzuri kati yao na Russia.

**VIONGOZI G7 WAKUTANA**

Mawaziri wa mambo ya nje wa kundi la nchi saba zilizostawi kiviwanda, G7 wanakutana kujadili namna watakavyoratibu msaada zaidi kwa Ukraine.

Mkutano huo unafanyika kufuatia mashambulizi yanayoendelea ya Russia nchini humo yakilenga mitambo ya kuzalisha nishati ya umeme na maji.

Uvamizi wa Russia nchini Ukraine unatarajiwa kuwa ajenda kuu katika mkutano huo wa siku mbili unaomjumuisha Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken na wenzake wa G7, unaofanyika mjini Muenster Magharibi mwa Ujerumani.

Jukumu au ushawishi wa China duniani na maandamano yanayoendelea nchini Iran pia ni mambo yatakayojadiliwa katika mkutano huo.

Ujerumani mwenyeji wa mkutano huo wa G7 na inayoshikilia urais wa kupokezana wa kundi hilo, inatoa nafasi kwa mataifa hayo tajiri duniani, kujadili zaidi kuhusu China na usalama wa eneo la Indo-Pasifiki, hasa baada ya Rais Xi Jinping kupitishwa kuongoza kwa muhula wa tatu.

**DW**

# Korea Kaskazini yazidi kurusha makombora

**SEOUL,** KOREA KUSINI

KOREA Kaskazini imezidi kuleta hofu kwa jirani yake baada ya kurusha kombora la masafa marefu (ICBM) lakini halikufaulu.

Kulingana na jeshi la Korea Kusini, uzinduzi wa makombora ya ICBM, umeiweka hadhari Korea Kusini na Japani, hata hivyo haukufaulu baada ya kutua baharini.

Mvutano unaongezeka huku kukiwa na hofu kwamba Kaskazini itafanya jaribio la nyuklia hivi karibuni.

Jumatano Korea zote mbili zilirusha makombora karibu na maji ya kila mmoja. Majibishano hayo yalishuhudia idadi kubwa ya makombora yaliyorushwa na Korea Kaskazini kwa siku moja.

Majaribio mengi ya Korea Kaskazini yanakuja wakati Marekani na Korea Kusini zikifanya mazoezi yao makubwa ya angani kuwahi kutokea.

Siku ya Alhamisi Korea Kaskazini ilirusha kombora la masafa marefu mwendo wa 07:40 saa za huko (23:40 GMT), kulingana na taarifa kutoka kwa Wakuu wa Pamoja wa Wafanyakazi wa Korea Kusini. Chanzo kimoja kilithibitisha kwa BBC.

Kombora hilo liliruka kwa takriban km 760 sawa na maili 472 na kufikia urefu wa karibu kilomita 1,920.

Hata hivyo, jeshi la Korea Kusini lilieleza uzinduzi huo ulidhaniwa kuwa ulimalizika kwa kushindwa.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA MOROGORO

KITUO CHA MJINI MKOA WA MOROGORO

Usimamizi wa Mirathi Na......81/2022

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: RAMADHANI RASHID MTAKAHELA WA AREA FIVE

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA MOHAMED RAMADHANI MTAKAHELA

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 18 Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 11 mwaka 2022

..............................................
HAKIMU

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(LAND DIVISION)
AT DAR ES SALAAM

LAND CASE NO. 97 OF 2022

MICHAEL MAKANIKA NYAMIKA...............................PLAINTIFF

VERSUS

TATU SELEMANI TULIENI & OTHERS...............RESPONDENTS

TO: (1) ERICK AUCTION MART & COURT BROKER
(2) NOEL ESTATE COMPANY LIMITED

**WHEREAS:** The above named PLAINT has/have instituted PLAINTIFF against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or Agent duly authorized **16th NOVEMBER, 2022 at 09:00 hrs BEFORE HON. A. MSAFIRI, JUDGE,** to answer the claim: and you are directed to bring any document which you wish to rely in support of your defence.

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day before mentioned, the **APPLICATION** will be heard and determined in your absence.

Given under my Hand and the Seal of this Court, this **31st day of OCTOBER, 2022.**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT LAND DIVISION

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA MOROGORO

KITUO CHA MJINI
MKOA WA MOROGORO

Usimamizi wa Mirathi Na......80/2022

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ALLY RAMADHANI NGALAWA WA BOMA B

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA ABDALLAH ALLY NGALAWA

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 04 Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 01 mwezi 11 mwaka 2022

HAKIMU MFAWIDHI

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

---

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA

MAHALI DODOMA
LILILOKO DODOMA

MAOMBI NA. 153 YA mwaka 2022

AGNESS KUSAJA.............................................MDAI 1

VERSUS

NGHONOLI MASAKA ................................................MDAIWA

**KWA: NGHONOLI MASAKA**
**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 02.12.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANAGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 01 ya mwezi wa November,2022.

..............................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA
NYUMBA LA WILAYA YA
DODOMA
TANZANIA

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MBEYA

SHAURI LA MAUAJI(CR.SESSION) NA. 05/2016

(Asilia Shauri la Uchunguzi wa Awali(PI) Na.44/2015.
Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)

JAMHURI

DHIDI YA

1.GEOFREY S/O NTAPANYA
2.NDONGOS/O MBESHI
3.CHUPA S/O UPOLO..........................................WASHITAKIWA
4.IDDI S/O RASHID

KWA BWANA: 1. CHUPA S/O UPOLO
2. IDDI S/O RASHID.

**POPOTE MLIPO TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani 07/11/2022 siku ya Juma tatu Saa3:00 Asubuhi bila kukosa.

ELEWA KWAMBA Mkikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa upande mmoja bila nyinyi kuwepo na Uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 19/10/2022.

NAIBU MSAJI MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

## KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI

**Peter Benedict Mgassa** anatangaza kupotea kwa Cheti cha usajili cha **MIRIAM ODEMBA FOUNDATION** chenye namba **000484.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/429367/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KASSIMU SALUMU** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 291 CMT.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Contro No. **9910834815391.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CHRISTER ADABATI ALFRED** anatangaza kupotolewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC. 173 CSR** aina ya **SINERAY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya polisi. **MAJ/RB/7214/2022.**

## KUPOTELEWA NA CHETI

Taasisi ya **Tanzania Alliance People's Organization (TAPO),** inatangaza kupotelewa na Cheti chenye usajili **no. 00005341,** na jina **Tanzania Alliance People's Organization.** Cheti kimepotea mkoa wa Dar es Salaam 15/10/2022. Atakae kiona au kukiokota tunaomba awasiliane nasi kwa namba zifuatazo. **0623 870197, 0768 540154**
Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/424900/2022**

## KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA UHUMA FINANCIAL SERVICES TUTAFANYA MNADA WA HADHARA TAREHE 07/12/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA KIWANJA NO. 1139 KITALU ZC ENEO LA NALA CHIHONI MALI YA EVANCE JOSEPH PAWASA BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA UHUMA FINANCIAL SERVICES MNADA UTAFANYIKA MAHALI AMBAPO KIWANJA KIPO.

**KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN BARIATI PARMWAT** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 104 AMB – TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba **JTELB71J207048013.** Engine namba **IHZ0484573.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/428434/2022.**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***




## BURUDANI




# TOWN CLASSIC RASMI MITAANI WIKI IJAYO

BAADA ya kufanikiwa kuteka mioyo ya mashabiki wa muziki wa dansi katika onyesho maalum la listening Part, bendi mpya ya Town Classic, inatarajia kuanza rasmi kufanya maonyesho katika kumbi mbalimbali wiki ijayo.

Kiongozi wa bendi hiyo Greyson Semsekwa, aliliambia gazeti hili, jijini Dar es Salaam jana kuwa walikuwa waanze maonyesho wiki hii, lakini kutokana na sababu zilizo juu ya uwezo wao, wataanza wiki ijayo.

"Nitumie nafasi hii kuwaomba radhi mashabiki wetu kwa kuahirisha onyesho la wiki, kwani ni kwa sababu ambazo ziko juu ya uwezo wetu, ila wiki ijayo tutaanza rasmi kutoa burudani," alisema Semsekwa.

Semsekwa alisema; 'Tumekuja kuleta upinzani ili kurejesha dansi kwenye kilele chake kama ilivyokuwa zamani, hivyo bendi nyingine zijipange vizuri Town Classic Band tunakuja kuongeza joto la ushindani."

Aidha, alisema bendi hiyo itaendelea na maonyesho huku ikijiandaa kwenda mjini Morogoro kwa ajili ya onyesho maalum wakati wa pambano la ngumi kati ya Twaha Kiduku na bondia mwenzake kutoka nchini Argentina.

Bendi hiyo ilifanya onyesho la listening Part Jumamosi iliyopita, katika ukumbi wa Gwambina Lounge (TCC Club) Chang'ombe jijini Dar es Salaam na kufanikiwa kujizolea mashabiki wengi wa muziki wa dansi.

Katika onyesho hilo, bendi hiyo ilitambulisha vibao vipya vinne vya 'No Stress, Shem Darling, Ngayo na Fitina', waimbaji wakiwa ni Semsekwa, Dipirone, Dogo Rama, Muu Bella, Totoo Kalala na kimwana Angel.

Mbali na hao, kwenye safu ya wapiga vyombo walikuwa ni Victor Mashine drums, huku wapiga magitaa wakiwa ni Tshims Kamanyola, Sele Muhumba, Acoustic, Loso, katika vinanda walikuwa ni Thabit Abdul na Zanda.

## MUUMIN: MIMI NA CHOKI HATUJAWAHI KUWA MAADUI

MWIMBAJI wa muda mrefu wa muziki wa dansi, Mwinjuma Muumin amefunguka kuwa malumbano yake na hasimu wake Ally Choki huwa ni ya mdomoni tu yenye lengo la kutaka kufurahisha mashabiki.

"Sisi tumetoka mbali sana na tumepiga bendi moja ndani na nje ya nchi, hivyo watu wasidhani kwamba, tuna ugomvi, mkiona tunashambuliana kwa maneno basi jueni kuwa ni kutaka kufurahisha," amesema Muumin.



Amesema wamewahi kuhojiwa kwa nyakati tofauti katika vituo vya redio, huku kila mmoja akimshambulia mwenzake kwa maneno, hali iliyowafanya baadhi ya watu waamini waimbaji hao wana ugomvi.

"Mimi na Choki ni maswahiba, hatuna ugomvi kwani hadi sasa huwa tunaalikwa na bendi mbalimbali na kufanya vitu vyetu kwa pamoja, hivyo wadau wa muziki watuelewe hivyo," amesema.

Waimbaji hao, walishawahi kumiliki bendi zao, Choki akiwa na Extra Bongo, wakati Muumin akiwa na Double M Sound, lakini kwa sasa Muumin ana mpya iitwayo Special Band, huku Choki amerejea Twanga Pepeta.

## MASHAUZI CLASSIC WAJIPANGA UPYA HADI 2023

KUNDI la muziki wa taarab la Mashauzi Classic, limesimamisha maonyesho yake, kwa ajili ya kujipanga upya hadi Januari mwaka ujao wa 2023 litakapoibuka upya na kutoa burudani.

Mkurugenzi wa kundi hilo Isha Mashauzi aliliambia gazeti hili jana kuwa ni muda mrefu tangu wasimamishe maonyesho kutokana na sababu ambazo ziko juu ya uwezo wao na kuamua kujipanga upya.

"Kwa ujumla ni kwamba tumesimamisha maonyesho kutokana na sababu ambazo ziko juu ya uwezo wetu, hivyo hadi Januari mwaka 2023 panapo majaliwa ya Mwenyezi Mungu tutaanza kutoa burudani," amesema Mashauzi.

Mwimbaji huyo ameongeza kuwa si kundi lake tu bali kwa sasa karibu makundi yote ya muziki huo yanakabiliwa na changamoto mbalimbali na kusababisha maonyesho mengi kukwama.

"Unapoona kuna hali huielewi, huna budi kutulia na kujipanga upya, hivyo nasi tumeona ni wakati mwafaka wa kutulia na kujipanga upya ili tukiibuka mwaka kesho tuwe na vitu vingi vya kuwashtua mashabiki," amesema.



Nyota huyo wa mipasho, amesema kimya kingi kina mshindo mkuu, na kwamba anaamini wataibuka kwa kishindo baada ya kumalizika kwa mwaka huu wa 2022 ambao wameamua kuupisha upite kwanza.

# DARTS WATAKIWA KUJITANGAZA

**Na Saada Akida**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha amekitaka chama cha Darts Tanzania (TADA) kujitangaza zaidi ili kupata udhamini.

Mbali na hilo amewataka wanapoandaa maombi ya udhamini wahakikishe wanaainisha wadau wao ambao wanauhakika wa kuwasaidia ili kuiwezesha BMT kuwasaidia kwa namna ya kufanya mazungumzo, kuwandikia barua au kikao cha pamoja na wadau hao.


Neema alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana katika hafla ya kukabidhi vikombe na kuwapongeza washindi wa mchezo huo katika mashindano ya PDC Africa yaliyomalizika Oktoba 30 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Aliwataka viongozi kuhakikisha mchezo huo unachezwa na watoto na utaweza kuonekana na kupa nguvu kabla ya kupelekwa katika mitaala ya skuli.

**"Nimesikia changa moto zenu, lakini kuna suala la vifaa hili linajadilika na tutalifanyia kazi mje tukae mezani kujadili zaidi," alisema Neema.**

Kwa upande wa Katibu Mkuu TADA, Victor Kimambo aliiomba serikali isaidie kutafuta wadhamini waweze kushiriki kikamilifu katika michuano ya ndani na nje ya nchi pamoja na upatikanaji wa vifaa vya mchezo wa vishale.

Kimambo alisema ombi lingine ni kuingizwa kwa vifaa vya mchezo huo kwenye mitaala kama somo ili uweze kuwasaidia watoto na utasaidia kupata vipaji kutoka skuli na kukuza mchezo huu kusambaza haraka.



Mkurugenzi wa Manunuzi wa Benki ya CRDB, Pendason Philemon (wa pili kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya safari iliyolipiwa kwenda Doha Qatar kushuhudia mashindano ya Kombe la Dunia mmoja wa washindi, Haji Msangi (katikati), wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi wa jumla wa hitimisho la awamu ya kwanza ya kampeni "Tisha na TemboCard", jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati, Bonaventure Paul (kulia), Mkuu wa Kitengo cha Masoko, Joseline Kamhanda (wa pili kulia) na Mkuu wa Biashara ya Kadi Benki ya CRDB, Farid Seif. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Marioo apewa ubalozi wa Parimatch*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya kubashiri ya Parimatch Tanzania imemtangaza rasmi mwanamuziki maarufu wa kizazi kipya Omary Ally Mwanga, maarufu kama Marioo, kuwa balozi wao nchini.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya kumtambulisha msanii huyo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Parimatch Tanzania, Eric George, alisema uwezo na kukubalika kwa Marioo ndani na nje ya nchi kumewafanya wavutike kuingia naye makubaliano ya mkataba wa mwaka mmoja wa kumfanya awe balozi wao hapa nchini.

"Tumechukua hatua ya uthubutu na kumchagua Marioo kuwa balozi wetu kwa ajili ya kuzidi kupata burudani. Yeye ni mtu ambaye amepambana na ameweza. Ila kikubwa pia ni kwamba kuwezi kuongelea burudani Tanzania bila kumtaja Marioo," alisema mkurugenzi huyo.

"Kupitia balozi wetu huyu tuna uhakika atai-peperusha vyema Chapa ya Parimatch kila eneo pamoja ba kusaidia kutoa uelewa kwa wachezaji wa michezo yetu maana hasa ya kubeti ili wote tuweze kufurahi na kucheza kistaarabu," aliongeza kusema George.

Akizungumzia michuano ya Kombe la Dunia inayotegemewa kuanza baadaye mwezi huu, mkurugenzi huyo alisema kampuni hiyo imewaandalia ofa kabambe wateja wao pamoja na wadau wote wa michezo ya kubashiri ambapo kwa kushiriki katika promosheni hizo kutamfanya mchezaji ajishindie zawadi nono ambazo zitamfanya ajihisi kama yupo Qatar. "Nipende kuwakumbusha Watanzania pamoja na wadau wote wa kubeti kwamba Kampuni ya Parimatch, ambayo imekuwepo nchini tangu mwaka 2019 imekuwa ikitoa huduma nzuri ikijumuisha malipo ya haraka, odds kubwa na promosheni za kusisimua kwenye soka, kasino na michezo mingine.

"Mbali na soka, kampuni pia hutoa mamia ya matukio kila siku kwenye tenisi, UFC, mpira wa kikapu, kriketi na michezo mingine," alisema mkurugenzi huyo.

Kwa upande wa Marioo, mwanamuziki aliishukuru Kampuni ya Parimatch kwa kufikia nao makubaliano hayo na kusema anaichukua fursa hiyo ya kuwa Balozi wa Parimatch kwa mikono miwili.

"Wengi mnajua kwamba mimi nimetokea mtaani kwa hiyo nitatumia nafasi hii kuwashikirisha watu wangu kuhamasisha na kushiriki kucheza na Parimatch.

"Nimefikia uamuzi huu kwa kuwa nina imani na Kampuni ya Parimatch na nitashiriki vizuri kuitangaza kwa vile mimi pia hivi sasa ni mwanafamilia ya Parimatch."

Kwa upande wa kiasi cha fedha kilichofikiwa kwenye makubaliano hayo ya mwaka mmoja, pande zote mbili zilidai hilo ni suala ambalo walikubaliana kutoliweka wazi wakati wa majadiliano yao kabla kusainiwa kwa mkataba huo.

## Wateja wa CRDB wajishindia safari ya Kombe la Dunia

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imehitimisha awamu ya kwanza ya kampeni yake ya "Tisha na TemboCard" kwa kuwakabidhi tiketi za kushuhudia mashindano ya Kombe la Dunia wateja wake watatu walioibuka washindi wa jumla wa kampeni hiyo.

Hafla hiyo imefanyika katika ukumbi uliopo makao Makuu ya Benki ya CRDB yaliyopo barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wateja na waandishi wa habari.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Manunuzi wa Benki ya CRDB, Pendason Philemon amewapongeza washindi hao kwa kuibuka katika kampeni hiyo kwa kufanya miamala mingi zaidi kupitia kadi zao za TemboCard.

"Kwa niaba ya benki niwapongeze kwa kuibuka washindi katika kampeni hii ambayo lengo na madhumuni yake ilikuwa ni kuwajengea Watanzania utamaduni wa kutumia kadi zao kufanya malipo," alisema Pendason.

Akielezea kuhusiana na zawadi hiyo Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati wa Benki ya CRDB, Bonaventure Paul, alisema pamoja na tiketi hizo za kushuhudia mechi za mpira, safari nzima ya washindi hao itagharamiwa kuanzia tiketi za ndege kuelekea Doha Quatar, malazi, pamoja na fedha za matumizi wakifika huko.

Washindi walioibuka kidedea kwenye safari ya kushuhudia Kombe la Dunia ni; Haji Athumani Msangi, Erick Boniface Kashangaki, Kelvin Jackson Twissa, na Rajabu Dossa Mfinanga wote wakazi wa Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo Benki ya CRDB pia ilikabidhi zawadi za fedha taslimu kwa washindi wengine watatu wa kampeni hiyo ambapo, Janeth Nyingi amejishindia shilingi milioni moja, na Benedict Tilisho na Marsh Bakari wamejishindia shilingi laki tano kila mmoja.

## IIT yaandaa matembezi kuelimisha kuhusu bima

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Bima Tanzania (IIT), imeandaa matembezi kesho Jumamosi kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu bima.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja Uendeshaji wa taasisi hiyo, Elizabeth Brown alisema matembezi hayo yataanzia kwenye ofisi za taasisi hiyo jengo la Maktaba ya Taifa na kuishia kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja.

Alisema matembezi hayo yatapitia mitaa ya Ohio kuelekea Shaban Robert na Samora hadi kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja ambapo yatapokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala.

Alisema siku hiyo ya Jumamosi kutakuwa na bahati nasibu ambapo washindi watatu watapewa bima ya afya ya mwaka mmoja kutoka makampuni matatu ya bima ambayo ni Assemble Insurance, Strategies Insurance na Jubilee Insurance.

"Tunawakaribisha wananchi wote waje kwenye matembezi haya lakini pia Mnazi Mmoja kutakuwa na mahojiano kuhusu masuala ya bima wananchi watauliza masuala mbalimbali ya bima ambayo ni fursa," alisema

Alisema makampuni mbalimbali ambayo yatafanya maonyesho na kutoa elimu kuhusu bima wnazotoa hivyo itakuwa fursa ya bure kwa wananchi watakaofika kwenye matembezi hayo kupata elimu ya bima.

Alisema taasisi hiyo inafanyakazi ya kukuza masuala ya bima nchini na imekuwa ikiendesha mafunzo mbalimbali kwa wananchi ili wafahamu vyema umuhimu wa kuwa na bima.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**GUNDOGAN AWANIWA BAYERN**
KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 32, anasakwa na Atletico Madrid. Mshindi huyo mara nne wa Ligi Kuu ya England ambaye pia anaivutia Bayern Munich, mkataba wake unamalizika msimu ujao. (***Mundo Deportivo***)

**KVARATSKHELIA AWINDWA**
WINGA wa Napoli na Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, ambaye anavutiwa na Liverpool na Chelsea, anaweza kugharimu hadi pauni milioni 86. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ameisaidia klabu yake kufuzu hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. (***London Evening Standard)***

**BELLINGHAM ATAKIWA MAN**
KLABU ya Manchester United imemfanya kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham kuwa mchezaji wanayemlenga huku kocha Erik ten Hag akitarajia dau la pauni milioni 100 kumnunua mchezaji huyo wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 19. (***Daily Mirror***)

**CHOUPO-MOTING AWANIWA MAN**
MANCHESTER United inafikiria kwa umakini kumnunua fowadi wa Bayern Munich raia wa Cameroon, Eric Maxim Choupo-Moting mwenye umri wa miaka 33. (***Media***)

**MAN HAIFUATILII**
MANCHESTER United haifuatilii mapato yoyote katika dirisha la usajili la Januari baada ya kuvunja rekodi yao ya uhamisho wa majira ya joto kwa kuwekeza pauni milioni 225.4 kwa wachezaji watano. (Manchester Evening News)

**DALOT KIPENGELE**
MANCHESTER United wanapanga kuanzisha kipengele katika mkataba wa Diogo Dalot kumzuia beki huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 23 kuondoka kama mchezaji huru msimu ujao. Barcelona na AC Milan wanamfuatilia Dalot. (***The Sun***}

**JORGINHO KUBAKI**
KIUNGO wa kati wa Chelsea na Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 30 anataka kubaki katika klabu hiyo licha ya kuripotiwa kuhusishwa na Barcelona. Mkataba wa Mchezaji huyo wa zamani wa Napoli mkataba unamalizika msimu ujao. (***Fabrizio Romano on Twitter)***

**ZIYECH ATAKIWA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inapigiwa upatu kumsajili winga wa Chelsea kutoka Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29, ambaye ameanza mara moja tu kwenye ligi kuu msimu huu. (***Express)***

**ARSENAL ILIPEWA OFA**
ARSENAL ilipewa nafasi ya kumsajili beki wa kushoto wa Benfica Mhispania Alejandro Grimaldo mwenye umri wa miaka 27, msimu wa joto lakini ilikuwa na kipaumbele kingine. (***CaughtOffside on Twitter)***

**MARTINELLI KUSAINI**
MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Brazil, Gabriel Martinelli mwenye umri wa miaka 21 amesema anakaribia kusaini mkataba mpya na Arsenal baada ya kufunga mara tano katika mechi 12 za ligi kuu msimu huu. (***Mirror)***

**MESSI HATAKI**
LIONEL Messi hataki kuondoka Paris St-Germain bila kushinda taji kubwa na mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 35 anajadili kuongeza mkataba wake hadi mwisho wa msimu. (***L'Equipe)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SON HATARINI KUKOSA KOMBE LA DUNIA QATAR

**Kufanyiwa upasuaji wa jicho la kushoto baada ya...**

**LONDON,** England

UWEZEKANO wa Heung-Min Son kucheza Kombe la Dunia uko shakani baada ya Tottenham kufichua kuwa alipasuka sehemu ya jicho katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Marseille, Jumanne.

Fowadi huyo alijeruhiwa baada ya kugongana juu dakika ya 23 na beki wa Marseille, Chancel Mbemba, na kusababisha mapumziko marefu kwenye mchezo.

Akiwa katika maumivu yanayoonekana na kuhangaika kutembea, Son alisaidiwa kutoka nje ya uwanja na madaktari wa Spurs wakati timu yake ikiendelea kujihakikishia nafasi ya kufuzu hatua ya mtoano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mabao ya Clement Lenglet na Pierre-Emile Hojbjerg.

**Spurs walitangaza Juma tano kwamba, Son amepata jeraha kwenye jicho lake la kushoto na anahitaji ku fanyiwa upasuaji.**

Katika taarifa yake kwenye tovuti rasmi ya klabu, Spurs ilisema: "Tunaweza kuthibitisha kwamba, Son Heung-min atafanyiwa upasuaji ili kurekebisha jeraha kwenye jicho lake la kushoto."

Tangazo hilo linatia shaka juu ya upatikanaji wa Son kwa Kombe la Dunia, huku Korea Kusini ikitarajiwa kuanza michuano hiyo kwa kucheza na Uruguay ndani ya siku 22 zijazo.

Jeraha la Son pia ni pigo kubwa kwa Spurs, huku washambuliaji wenzake Dejan Kulusevski na Richarlison wakiwa bado nje wakati wakikabiliwa kucheza na Liverpool Jumapili kwenye Ligi Kuu ya England.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,046,4

MECHI KALI

MBEYA CITY
VERSUS
NAMUNGO

1 | 2.11
X | 2.78
2 | 3.75

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.


tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA HANA MPANGO WA KUINOA BARCELONA



**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesisitiza furaha yake katika uwanja wa Emirates huku kukiwa na ripoti kuwa huduma yake inatakiwa na wababe wa Ligi Kuu ya Hispania, Barcelona.

Wiki hii, iliripotiwa kwenye vyombo vya habari vya Hispania kwamba, Barcelona licha ya kuridhika na kocha wao wa sasa, Xavi, wanamtolea macho Arteta baada ya kuvutiwa sana na mafanikio yake ya kuijenga upya Arsenal.

Alipoulizwa mawazo yake kuhusu uvumi huo, Arteta - ambaye alitumia muda katika akademi ya Camp Nou kama mchezaji - alipuuza uvumi huo haraka.

"Ninachoweza kusema nina furaha na fahari kuwa hapa nilipo," aliuambia mkutano wa waandishi wa habari.

"Nadhani Barcelona sasa wako kwenye njia nzuri sana, nadhani wana kocha wa ajabu - kocha ambaye amekuwa gwiji wa klabu na ameinuka sehemu nzima. Nadhani unapaswa kuheshimu sana hilo."

Akiwa amesajiliwa na Barcelona akiwa na umri wa miaka 15, Arteta hakuwahi kucheza katika klabu hiyo na badala yake alipelekwa kwa mkopo Paris Saint-Germain Desemba 2000, na baada ya hapo akasaini mkataba wa kudumu kwenda Rangers ya Scotland.

Baada ya kucheza vizuri, Arteta alifanya kazi chini ya kocha wa zamani wa Barcelona Pep Guardiola katika klabu ya Manchester City kabla ya kuchukua hatua yake ya kwanza katika uongozi wa juu akiwa na Arsenal mwishoni mwa 2019.

Arteta alikabiliwa na ukosoaji mkubwa katika hatua za mwanzo za utawala wake huku maswali yakiulizwa juu ya utayari wake kwa kazi hiyo kubwa, lakini baada ya miezi kadhaa ya mapambano, amejiimarisha kama kocha mkuu na amekiongoza kikosi chake cha washikabunduki hao kileleni mwa Ligi Kuu.

Barcelona nao wametolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya makundi na kujikuta wakiwa nyuma kwa pointi moja dhidi ya mabingwa wa Ulaya, Real Madrid kwenye LaLiga.

# Wakala wa Jorginho afichua ukweli

**LONDON, England**


WAKALA wa kiungo wa Chelsea, Jorginho amepuuzilia mbali uvumi kwamba mteja wake anatakiwa na Barcelona msimu ujao wa joto.

Huku mkataba wa Muitaliano huyo ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, hatma ya Jorginho imekuwa ikizungumziwa na ripoti nyingi, baadhi zikidai kuwa amepewa ofa moja kwa moja na Barcelona huku Blaugrana wakijiandaa kutafuta soko la wakala huru msimu ujao.

Hata hivyo, wakala Joao Santos alisisitiza kuwa hakuna mawasiliano yoyote na Barcelona hadi sasa.

"Sijawahi kukutana na mkurugenzi wa Barcelona, Mateu Alemany," alisema.

"Kipaumbele chetu ni kusaini mkataba mpya na Chelsea. Klabu pekee ambayo nimezungumza nayo wiki za hivi karibuni ni Chelsea."



90min ilifichua Oktoba kwamba mustakabali wa Jorginho na kiungo mwenza N'Golo Kante, ambaye mkataba wake pia unamalizika majira ya joto yajayo, ni gumzo la kawaida kati ya wasimamizi huko Stamford Bridge.

Tofauti za maoni kuhusu mishahara na urefu wa mkataba zinazopendekezwa zimeonekana kuwa na matatizo katika mazungumzo, huku Chelsea ikizingatia kuwapa mikataba ya gharama kubwa na ndefu wachezaji hao wa kati.

Declan Rice wa West Ham ndiye anayelengwa sana na dirisha la usajili la majira ya joto, wakati Chelsea pia wanajulikana kuwa wanamuwania Jude Bellingham wa Borussia Dortmund na Edson Alvarez wa Ajax.

## HABARI MICHEZO

433,814/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/11/22 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.83 | 3.23 | 2.48 |
| 02. 05/11/22 | 18:00 | QPR vs West Bromwich | 2.44 | 3.29 | 2.84 |
| 03. 05/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Brentford | 2.73 | 3.28 | 2.54 |
| 04. 05/11/22 | 19:00 | AC Ajaccio vs Strasbourg | 2.73 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 05/11/22 | 20:00 | Galatasaray vs Besiktas | 2.43 | 3.33 | 2.83 |
| 06. 05/11/22 | 20:30 | Everton vs Leicester | 2.33 | 3.27 | 3.03 |
| 07. 05/11/22 | 21:00 | PAU FC vs Amiens | 2.79 | 3.14 | 2.64 |
| 08. 05/11/22 | 21:00 | Bastia vs Paris FC | 2.49 | 3.11 | 3.01 |
| 09. 05/11/22 | 21:00 | Dijon vs Guingamp | 2.50 | 3.16 | 2.96 |
| 10. 05/11/22 | 22:30 | Arminia Bielefeld vs Kaiserslautern | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 06/11/22 | 14:30 | Bologna vs Torino | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 12. 06/11/22 | 15:00 | Chelsea vs Arsenal | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 13. 06/11/22 | 15:30 | KAA Gent vs Brugge | 2.54 | 3.59 | 2.54 |
| 14. 06/11/22 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Greuther Furth | 2.54 | 3.28 | 2.73 |
| 15. 06/11/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Montpellier | 2.31 | 3.52 | 2.83 |
| 16. 06/11/22 | 19:05 | Lille vs Rennes | 2.48 | 3.48 | 2.63 |
| 17. 06/11/22 | 19:30 | Tottenham vs Liverpool | 2.88 | 3.53 | 2.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 04/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:45 | 4983 | Melbourne Victory vs Newcastle Jets | 1.75 | 3.78 | 4.18 |
| 12:30 | 5256 | Shanghai SIPG vs Dalian Aerbing | 1.25 | 5.06 | 9.53 |
| 14:00 | 5283 | Turan Tovuz vs Keshla FK | 2.16 | 3.30 | 3.30 |
| 14:30 | 3168 | Beijing Guoan vs Henan Jianye | 2.41 | 3.30 | 2.62 |
| 15:00 | 5723 | Ethiopian Medhin vs Bahir Dar Kenema FC | 2.70 | 2.90 | 2.80 |
| 15:45 | 3036 | Masafi vs City Football Club | 1.68 | 4.00 | 4.50 |
| 15:50 | 1744 | Baynounah vs Gulf FC | 3.16 | 3.50 | 2.01 |
| 16:00 | 1928 | Mbeya City vs Namungo | 2.11 | 2.78 | 3.75 |
| 16:00 | 3138 | Shabab AL Amari vs Thagafi Tulkarem | 2.67 | 3.44 | 2.30 |
| 16:05 | 2985 | Al Nasr Salalah vs AL Bashair | 1.59 | 3.41 | 5.65 |
| 17:00 | 1981 | Jazeera Amman vs Faisaly Amman | 5.65 | 3.36 | 1.60 |
| 18:00 | 1894 | FK Mladost Gat vs FK Vozdovac | 2.82 | 3.11 | 2.36 |
| 18:00 | 3383 | Al Seeb vs Al Suwaiq | 1.57 | 3.44 | 5.81 |
| 18:00 | 5491 | Urartu vs Bkma Yerevan | 1.21 | 5.61 | 10.63 |
| 19:00 | 1935 | FK Khimki vs Gazovik Orenburg | 3.82 | 3.77 | 1.81 |
| 19:00 | 2281 | Rayon Sports FC vs Sunrise | 1.85 | 3.12 | 4.19 |
| 20:00 | 2534 | Apoel Nicosia vs EN Paralimni | 1.25 | 5.60 | 10.99 |
| 20:00 | 2621 | Novi Pazar vs Javor Ivanjica | 1.57 | 3.66 | 5.27 |
| 20:00 | 2704 | Umraniyespor vs Alanyaspor | 2.93 | 3.53 | 2.22 |
| 20:00 | 4126 | Kasimpasa vs Ankaragucu | 2.18 | 3.38 | 3.13 |
| 20:00 | 4232 | Istra vs HNK Gorica | 2.58 | 3.22 | 2.49 |
| 20:00 | 4768 | Stal Mielec vs Zaglebie Lubin | 2.97 | 3.31 | 2.16 |
| 20:30 | 2401 | SV Darmstadt vs Hannover | 1.75 | 3.71 | 4.16 |
| 20:30 | 5567 | Hansa vs Sandhausen | 1.99 | 3.32 | 3.62 |
| 21:00 | 4235 | Horsens vs Randers | 2.75 | 3.49 | 2.36 |
| 22:00 | 3978 | Cambuur vs NEC Nijmegen | 2.42 | 3.33 | 2.73 |
| 22:00 | 4425 | ADO Den Haag vs VVV Venlo | 1.84 | 3.85 | 3.56 |
| 22:00 | 4984 | Den Bosch vs De Graafschap | 3.21 | 3.50 | 2.05 |
| 22:00 | 5955 | FK Napredak vs Cukaricki St | 4.19 | 3.56 | 1.72 |
| 22:15 | 1572 | FC Aarau vs Yverdon-Sport FC | 2.07 | 3.51 | 3.02 |
| 22:15 | 2536 | FC Thun vs FC Wil | 1.82 | 3.59 | 3.69 |
| 22:15 | 4703 | Luka Koper vs Domzale | 1.89 | 3.50 | 3.50 |
| 22:15 | 5764 | FC Schaffhausen vs Lausanne-Sport | 3.01 | 3.30 | 2.15 |
| 22:30 | 1871 | Legia Warszawa vs Lechia Gdansk | 1.63 | 3.74 | 4.56 |
| 22:30 | 1875 | Aberdeen vs Hibernian | 2.50 | 3.35 | 2.65 |
| 22:30 | 3570 | Monchengladbach vs Stuttgart | 2.01 | 3.76 | 3.17 |
| 22:45 | 1033 | Galway United vs Waterford Utd | 2.57 | 3.49 | 2.36 |
| 22:45 | 1090 | Kilmarnock vs Livingston | 2.62 | 3.07 | 2.72 |
| 22:45 | 2520 | Udinese vs Lecce | 1.54 | 3.96 | 5.55 |
| 22:45 | 2625 | Ballymena Utd vs Newry City AFC | 1.97 | 3.70 | 3.11 |
| 22:45 | 2692 | Sheffield Wed vs Morecambe | 1.31 | 4.95 | 8.51 |
| 22:45 | 2981 | Cove Rangers vs Queens Park | 2.52 | 3.36 | 2.57 |
| 22:45 | 4824 | Larne vs Crusaders Belfast | 2.06 | 3.35 | 3.16 |
| 22:45 | 5820 | Bala Town vs Aberystwyth Town | 1.30 | 5.04 | 7.56 |
| 22:55 | 1381 | Hereford United vs Portsmouth | 7.93 | 5.15 | 1.31 |
| 23:00 | 3166 | Reading vs Preston | 2.43 | 3.17 | 2.83 |
| 23:00 | 4155 | Troyes vs AJ Auxerre | 1.88 | 3.54 | 3.83 |
| 23:00 | 5401 | Girona vs Athletic Bilbao | 3.55 | 3.40 | 2.02 |
| 23:00 | 5518 | Alaves vs Zaragoza | 2.01 | 3.13 | 3.82 |
| 23:15 | 1839 | Gil Vicente vs Portimonense | 2.14 | 3.34 | 3.24 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MKULIMA MWINGINE ASHINDA SH. MIL 10 ZA JACKPOT BONUS

**Na Mwandishi Wetu**

MKULIMA wa mpunga kutoka Wilaya ya Kaliua, mkoani Tabora, Peter Andrew Dotto, ameshinda Sh. 10,681,562, katika Jackpot Bonus ya Sportpesa ya katikati ya wiki, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya mechi 13.

Akizungumza kwenye hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi ofisi za Sportpesa, Dar es Salaam, Peter anasema alianza kucheza na Sportpesa mwaka 2019

"Nilianza kucheza na Sportpesa miaka mitatu iliyopita baada ya kaka yangu mkubwa ambaye ni wa kwanza kushinda Sh. 600,000 wakati huo ilikuwa ni mwezi wa kumi na mbili na kimaisha kwa wakati ule tulikuwa tunapitia kipindi kigumu sana.

Kwa mujibu wa maelezo yake, Peter amesema tangu ameanza kucheza na Sportpesa au tangu alipofundishwa na kaka yake kucheza amewahi kushinda mara tatu kabla ya ushindi huu na hiyo ilikuwa mwaka 2020.

"Nafikiri ilikuwa bahati yangu kwa wakati ule ambapo nilishinda Sh. 100,000, Sh. 70,000 na Sh. 190,000 kwenye hizi multibet".

Akielezea namna alivyopata ushindi huu wa Jackpot bonus ya kati kati ya wiki, Peter anasema kwanza yeye hana tabia ya kucheza kila siku au mara kwa mara, pili siku akiamua kucheza huwa anaweka mikeka si chini ya saba.

Akimpongeza mshindi, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, alimtaka kuendelea kucheza na Sportpesa na pia kuwafundisha wengine ambao bado wanasita kujisajili na Sportpesa ili na wao washinde kama yeye.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Peter Dotto kutoka Tabora akishikilia mfano wa hundi ya Sh. 10,681,562 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba Queens hesabu zote kwa Green Buffalo

INATOKA UK. 32

Green Buffalo likifungwa na Ireen Kapemba.

Katika hatua nyingine, kikosi cha Simba Queens kinatarajia kuondoka leo hapa Rabat na kuelekea Marrakech kwa ajili ya kwenda kucheza mechi ya mwisho ya hatua ya makundi itakayochezwa kesho jijini humo.

# Nabi mguu ndani, mguu nje Yanga

INATOKA UK. 32

"Niwaombe mashabiki na wanachama wetu kuwa na utaratibu wa kufuatilia taarifa za klabu yetu kutoka kwenye vyanzo vyetu vya habari," alisema.

Wakati huo huo, Makamu Rais wa Club Africain ya Tunisia, Mehdi Gharbi amekiri kukutana na timu nzuri ya Yanga, hasa kwenye upande wa ushambuliaji na viungo, lakini akasema itakuwa ni ngumu kwao kupata ushindi nchini kwao.

Akizungumza juzi baada ya mechi hiyo alisema wanashukuru kwa suluhu waliyoipata kwani ndiyo ilikuwa ni mpango mkakati wao baada ya kuwasoma vizuri wapinzani wao.

"Ilikuwa ni mechi ngumu, tukiri kuwa tumekutana na timu nzuri ya Yanga, kwa hii suluhu tuliyoipata tunashukuru Mungu kila kitu kitafanyika nyumbani kwenye mchezo wa marudiano. Yanga wana mastraika na viungo wazuri sana, na tuliwasoma vizuri, hivyo tulivyokuja huku mpango mkakati wetu ulikuwa ni kuwazuia ili tutoke suluhu na nimefanikiwa," alisema Gharbi.

Kutokana na matokeo hayo alisema wana matumaini makubwa ya kushinda kwenye mechi ya marudiano.

# Michezo

Ijumaa Novemba 4, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Son hatarini kukosa kombe la Dunia



Kiungo wa Simba Queens, Olaiya Barakat (kulia), akipambana kumtoka beki wa Determine Girls katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan juzi usiku. Simba Queens ilipata ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# NABI MGUU NDANI, MGUU NJE YANGA

●●●Abakiza dakika 90 kunusuru kibarua, Makamu Rais Club Africain asifia kiungo, mastraika...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HALI tete Yanga, baada ya matokeo ya suluhu waliyoyapata katika mchezo wa juzi dhidi ya Club Africain ya Tunisia, inamuweka katika wakati mgumu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddin Nabi.

Yanga ilipata matokeo hayo katika mechi ya kwanza ya hatua ya mchujo wa Kombe la Shirikisho Afrika (CAF-CC), iliyochezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Matokeo hayo yamewaweka katika mazingira magumu wanapokwenda katika mchezo wa marudiano, mchezo utakaochezwa Novemba 9, katika Uwanja wa Hammedi Agrebi Olympic nchini Tunisia.

Kabla ya mchezo wa juzi, kulikuwa na taarifa kuwa kocha huyo amepewa dakika 180 dhidi ya Club Africans ili kunusuru kibarua chake hivyo amebakisha dakika 90 tu ambazo anatakiwa kuibakisha timu katika michuano hiyo.

Habari za uhakika kutoka ndani ya klabu ya Yanga, zinadai kuwa kocha huyo akishindwa kuipeleka Yanga katika hatua ya makundi, uongozi umepanga kuvunja mkataba wake.

"Makubaliano ya mwisho ilikuwa ni kuipeleka timu hatua ya makundi, hata yeye aliahidi hivyo," zilieliza habari hizo.

Akizungumzia kuhusu kibarua chake Yanga, Nabi alisema anaamini bado anauwezo wa kuonesha uwezo katika mchezo ujao.

Alisema anaamini mpira unadunda, Club Africain walicheza mpira wa kujilinda zaidi hata wao watakwenda na mbinu mbadala kuhakikisha wanafanya vizuri.

"Tulipania kufanya vizuri katika mchezo wa nyumbani, wenzetu walijilinda sana na naamini hawawezi kucheza hivyo katika mchezo wa marudiano, tunakwenda kupambana kuhakikisha tunashinda ugenini," alisema Nabi.

Alisema walishindwa kupata mabao kutokana na wapinzani wao kucheza zaidi kwa kujilinda, kwa ubora wa kikosi chao wana uwezo wa kupata matokeo mazuri katika mechi ya marudiano.

"Huwezi kupata mabao dhidi ya timu inayocheza na wachezaji tisa nyuma (kujilinda), tunaamini kwao hawatacheza namna hii na watafunguka kwa ajili ya kusaka ushindi.

"Tunaamini ubora wa wachezaji wetu na jinsi tulivyomuona mpinzani wetu na kitu cha kufanya kwenye mechi ya marudiano kuwa makini safu ya ulinzi na ushambuliaji kutumia vema nafasi ili tufuzu na kusonga mbele katika mashindano haya," alisema Nabi.

Mtendaji Mkuu wa Yanga, Adre Mtine, alisema wanamtambua Nabi bado ni kocha mkuu wa timu hiyo na ataendelea kukinoa kikosi chao.

INAENDELEA UK. 31

## Simba Queens hesabu zote kwa Green Buffalo

**Na Somoe Ng'itu, RABAT**

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa kwanza katika fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake zinazoendelea nchini Morocco, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema watacheza kufa na kupona katika mchezo wao dhidi ya Green Buffalo ya Zambia utakaofanyika kesho jijini Marrakech.

Kufuatia ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Determine Girls ya Liberia, Simba Queens iko katika nafasi ya tatu kwenye Kundi A ikiwa na pointi tatu sawa na Green Buffalo huku wenyeji ASFAR wakitangulia nusu fainali baada ya kuwafunga Wazambia na kufikisha pointi sita katika mechi iliyochezwa juzi usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lukula alisema wataongeza umakini na utulivu katika mechi hiyo ambayo anahitaji ushindi tu ili wasonge mbele katika mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Lukula alisema watacheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu wapinzani wao Green Buffalo nao wananafasi sawa ya kutinga hatua ya nusu fainali endapo watapata ushindi au sare ya aina yoyote.

Aliongeza kila timu inayoshiriki mashindano haya ni kubwa hivyo, wataingia katika mechi hiyo wakiwaheshimu wapinzani wakati wote wa mchezo.

"Baada ya kurekebisha makosa na kujua tulipokosea, tuliingia na mbinu tofauti, ilitusaidia, pia baada ya kumtoa Asha (Djafar), ambaye amepoteza nafasi nyingi walizotengeneza, sasa tunahitaji kuongeza bidii, ninajua ushindani utakuwapo," alisema kocha huyo.

Wakati huo huo, kiungo wa Simba Queens, Pambani Falonne, alichaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa mechi dhidi ya Determine Girls huku Fatima Tagnaout wa ASFAR FC alitangazwa Mchezaji Bora katika mchezo dhidi ya Green Buffalo.

Tagnaout alifunga mabao mawili yote kwa penalti na katika mechi iliyomalizika wa wenyeji kupata ushindi wa magoli 2-1, bao pekee la

INAENDELEA UK. 31

Nabi

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >